**Université du Burundi**

**Dépôt institutionnel officiel** **https://repository.ub.edu.bi**

Grenier du Savoir du Burundi Mémoires et Thèses

2025-03

# Tathmini ya Mbinu za Uundaji wa Istilahi za Uwanja wa Tiba: Uchunguzi Kifani wa Kamusi ya Tiba, Toleo la 2003

Burakuvye, Montfort

UB, FLSH

https://repository.ub.edu.bi/handle/123456789/2179

*Téléchargé depuis le dépôt institutionnel officiel de l'Université du Burundi*

UNIVERSITE DU BURUNDI

FACULTE DES LETTRES ET SCIENCES HUMAINES

MASTER EN TRADUCTION ET INTERPRETATION

# TATHMINI YA MBINU ZA UUNDAJI WA ISTILAHI ZA UWANJA WA TIBA: UCHUNGUZI KIFANI WA KAMUSI YA TIBA, Toleo la 2003

**Par :**

**Montfort BURAKUVYE**

**<u>Sous la direction de</u>:**

1. Pr. Ferdinand Mberamihigo
2. Dr. Dieudonné Butoyi

Mémoire présenté pour l'obtention d'un **Diplôme de Master en Traduction et Interprétation.**

Bujumbura, Mars 2025

## IDENTIFICATION DES MEMBRES DU JURY

Muku wa jopo : Dkt. Dénis BUKURU

Wasimamizi : Profesa Ferdinand MBERAMIHIGO

Dkt. Dieudonné Butoyi

Mhariri : Mwal. Enock HAVYARIMANA

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa mke wangu mpendwa Marie Françoise Havyarimana na kwa mama yangu mzazi Oda Ntegirigwa na baba mzazi marehemu Méthode Burakuvye. Mchango wao katika utekelezaji wa kazi hii umezidi kiwango cha kawaida.

**SHUKURANI**

Kwanza, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mweza wa kila kitu, kwa kunijalia afya njema, nguvu, uwezo, akili, busara, maarifa, utulivu na uvumilivu katika kipindi chote cha masomo yangu ya umahiri.

Pili, ninachukua fursa hii kuushukuru uongozi wa Chuo Kikuu Cha Burundi kwa kuniteua miongoni mwa wanafunzi wa shahada ya umahiri katika Tafsiri na Ukalimani mwaka 2021-2022.

Tatu, ninapenda kuwashukuru wasimamizi wangu Prof. Ferdinand Mberamihigo na Dkt. Dieudonné Butoyi kwa kuniongoza vema katika kila hatua ya utafiti huu. Hawakusita wala kuchoka kunishauri na kuiboresha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Wamenilea kitaaluma na kunipa misingi ya nadharia za tafsiri, leksikografia na istilahi na mbinu za utafiti ambazo zimezaa kazi hii. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awabariki na awape afya njema. Shukrani zangu pia ziwafikie walimu wangu wote walionilea kitaaluma katika kitivo cha fani na sayansi za jamii.

Nne, shukrani za dhati zimfikie mama mlezi wa wadau wa Kiswahili nchini Burundi, Mwl. Dorothée Nshimimana ambaye alinipa misingi ya lugha ya Kiswahili. Mchango wake mzuri katika kueneza lugha ya Kiswahili nchini Burundi ulinifanya nielewe kuwa lugha yoyote huwa nyenzo ya kueleza na kueneza sayansi. Tano, siwezi kumsahau mke wangu Marie Françoise Havyarimana na watoto wetu Gladwell Aymar Iraganje, Marie Samira Iraninahaye na Aël Dylan Imukuze walioniwia nguzo wakati wote nilipokuwa nikifanya utafiti huu. Mwisho, shukrani zangu za dhati ziifikie familia ya Bwana Edouard Nziguheba kwa mchango mkubwa ulioniwezesha kuishi jijini Bujumbura kipindi chote cha masomo ya umahiri.

**ABSTRACT**

This study aimed to assess the approaches to creating terminology in the field of medicine. The specific objectives were first to identify terms related to diseases. Second, it sought to define the terminology creation methods used to develop these terms, and third, to provide reasons for the use of the selected methods. This study was guided by the Content Analysis Theory (CAT) established by Krippendorff (2004) as well as the Scientific Terminology Theory (STT) presented by Kiingi (1989) and further developed by Kiingi Mwaro-Were (2000). The investigation revealed the main methods used, such as Borrowing, Loan Translation, Literal Translation, Equivalent Translation, Explanatory Translation, and Semantic Translation. Moreover, the study showed that no single method is sufficient on its own. The Scholars used various methods to achieve their goals. The reasons for using the proposed translation methods include the lack of equivalents in different dictionaries due to globalization and the emergence of new terminology frequently, to fill the gap of missing equivalents, and to avoid proposing terms that would distort the meaning of terminology from SL to TL. The Explanatory Translation, and Semantic Translation tmethod were used because medical language is difficult to understand. By providing more understanding through Explanatory Translation, and Semantic Translation of terms to the audience of the Medical Dictionary, the 2003 edition gains more clarity and comprehension of the meaning of the respective terms. There are other areas that have not been subjected to such research, such as the field of medicine, medical science, and surgery. Researchers can conduct comparative studies of the terminology creation methods used in the process of coining Medical Dictionary.

**Key words:** Dictionary, Terminology development methods, Translation.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kutathmini mbinu za uundaji wa istilahi za uwanja wa tiba. Malengo mahususi yalikuwa kwanza kubainisha istilahi zinazohusu magonjwa. Pili, ulilenga kufafanua mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa kuundia istilahi hizo na tatu kutoa sababu zamatumizi ya mbinu teule. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi wa Maudhui (UMA) iliyoasisiswa na Krippendorff (2004) pamoja na na Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) iliyowasilishwa na Kiingi (1989) na kuendelezwa na Kiingi Mwaro-Were (2000). Uchunguzi ulionyesha mbinu kuu zilizotumiwa kama vile Ukopaji, Utohozi, Tafsiri Sisisi, Tafsiri kwa Usisawe, Tafsiri Kimaelezo na Tafsiri ya Maana. Isitoshe, uchunguzi ulionyesha kuwa hakuna mbinu inayojitosheleza. Waundaji walitumia mbinu chotara kufikia malengo yao. Sababu za matumizi ya mbinu za tafsiri zilizopendekezwa ni ukosefu wa visawe katika kamusi mbalimbali kutokana na utandawazi na kuibuka kwa istilahi mpya kila kukicha, kuziba pengo la ukosefu wa visawe, kujiepusha kupendekeza istilahi ambayo ingepotosha maana ya ujumbe wa istilahi kutoka LC kwenda LL. Mbinu ya tafsiri kimaelezo ilitumika kwa kuwa lugha ya kimatibabu ni lugha gumu kueleweka. Kwa kutoa uelewa zaidi kupitia tafsiri kimaelezo kwa istilahi kwa msomaji wa Kamusi ya Tiba, toleo la 2003 wanapata mwanga zaidi na kuelewa maana ya istilahi husika. Kuna nyanja zingine ambazo hazijafanyia utafiti kama huu. Kama vile uwanja wa dawa, uwanja ya sayansi ya tiba, uwanja wa upasuaji. Watafiti wanaweza kufanya utafiti linganishi wa mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa katika mchakato wa kuitunga *KT*.

**Dhana Muhimu:** Kamusi, Mbinu za Uundaji wa Istilahi, Tafsiri

## CONDENSE DU MEMOIRE

Ce document résume l'étude menée par Montfort Burakuvye en vue de l'obtention d'un diplôme de master en Traduction et Interprétation. Cette étude, intitulée **« Tathmini ya Mbinu za Uundaji Istilahi za Kamusi: Uchunguzi Kifani wa Kamusi ya Tiba, Toleo la 2003»** est structurée en cinq chapitres.

Tout d'abord, le chapitre premier relatif à l'introduction générale présente le contexte, la problématique, les objectifs, les hypothèses, la délimitation de la recherche et l'importance de cette recherche. Ensuite, le second chapitre présente le cadre théorique et la revue de la littérature. Le chapitre trois présente la méthodologie de collecte et d'analyse des données issues du corpus. Le chapitre quatre est l'analyse des données. Dans ce chapitre, hypothèses de la recherche ont été ainsi confirmées. Enfin, le chapitre la conclusion générale résume les principales conclusions du cette recherche et propose des suggestions.

## CHAPITRE UN : INTRODUCTION GENERALE

Contexte de l'étude

Environ 7000 langues sont parlées à travers le monde selon l'UNESCO (2024) bien qu'il ne soit pas facile de déterminer le nombre exact de langues parlées en raison de la difficulté à tracer des frontières précises entre plusieurs langues ou entre une langue et un dialecte. Aucune communauté de personnes ne peut être dans un état d'unicité pour toujours. De plus, lorsque les humains vivent dans leur environnement, ils cherchent tous les moyens de confronter cet environnement en explorant, recherchant, enquêtant et découvrant de nouvelles choses au sein de la communauté, Jilala (2022).

Le traducteur est un utilisateur de la terminologie comme celui qui utilise un vocabulaire courant. Une recherche mérite d'être menée pour découvrir les techniques de création

terminologique dont le traducteur a régulièrement besoin pour rendre son métier de communication en domaines de specialité plus satisfaisant.

**Problématique de Recherche**

Bien que le traducteur soit l'un des principaux utilisateurs de la terminologie, il ne trouve pas toujours, en traduisant des textes scientifiques ou techniques, les termes dont il a besoin et qui sont corrects à ce moment-là, Bwenge (2000). Un grand travail dans la traduction consiste à rechercher des synonymes dans la langue cible (LC). Lorsque les synonymes sont absents, d'autres méthodes de transmission du message vers la LC sont utilisées, Jilala (2021).Pire encore, selon Mabasa (2005) les traductions médicales déforment le sens car de nombreux professionnels de la santé utilisent des concepts généraux pour expliquer des questions médicales spécifiques, comme l'indique. Cela entraîne des ambiguïtés dans la traduction. Par conséquent, le traducteur doit transmettre un message sans ambigüité concernant les instructions et les descriptions des terminologies médicales. De plus, il est difficile de maîtriser les techniques de création de terminologie si le traducteur n'a pas suffisamment de compétences création de terminologique des différentes spécialités comme la médecine. Ainsi, malgré certaines études abordant ce domaine, il n'y a pas d'études qui se sont concentrées sur l'évaluation des techniques de création de terminologique relevant du domaine médical.Dans cette optique, cette recherche vise à évaluer les méthodes de création de terminologique utiliséés dans le processus de la confection du Dictionaire Médical (Kamusi ya Tiba 2003) et à fournir des les motivations de l'utilisation de ces méthodes.

**Objectifs de la recherche**

Les objectifs qui dirigent cette recherche sont les suivants:

**Objectif principal de la recherche :** Evaluer les techniques de création terminologique utilisées dans la création de termes de la LC du DM.

**Objectifs spécifiques :** (i) Identifier la terminologie relative aux maladies présentée dans la LC du DM; (ii) Définir les techniques de création de terminologique utilisées pour la terminologie relative aux maladies présentée dans la LC du DM; (iii) Expliquer les raisons de l'utilisation des techniques de création de terminologique utilisées pour la terminologie relative aux maladies présentée dans la LC du DM.

**Importance de la recherche**

Cette recherche renferme une importance capitale de plusieurs angles. Tout d'abord, elle met en lumière la terminologie liée aux maladies présente dans LM. Les traducteurs qui consulteront cette recherché y trouvera la terminologie y relative et les techniques de création terminologie utilisée par le confectionnaire dudit DM. Deuxièmement, cette recherche éclairera les traducteurs qui doivent maîtriser l'expansion du vocabulaire ou des termes qui pèsent lourdement sur la langue kiswahili. Elle leur permettra d'acquérir et de maîtriser des méthodes de création de terminologiques afin de répondre aux besoins de maintenir le pont de communication.Troisièmement, elle est une contribution académique ; c'est le premier mémoire écrit en langue kiswahili défendu au niveau du master à l'université du Burundi, les résultats de cette recherche constituent une référence aux futures recherches.

**CHAPITRE DEUX : REVUE DE LA LITTERATURE**

Cette section explore les travaux existants pertinents qui se focalisent sur la terminologie et les techniques de création terminologie en langue africaines.

**Elucidation des concepts**

**Le concept de la terminologie :** les spécialistes ont donné diverses définitions concernant le concept de terminologie.Nimessi (2022) définit la terminologie peut être définie comme une discipline de création de mots, comme l'ensemble des mots utilisés dans un domaine particulier. ou comme une base de données de mots utilisés dans une discipline spécifique.

**Le concept de Dictionnaire**

Selon Mdee (1996) un dictionnaire est un livre listant des mots, avec leurs significations. Ainsi, existe- t-il différents types de dictionnaires. Selon le nombre et le statut des langue(s) étudiée(s) dans le dictionnaire nous pouvons distinguer deux grandes sortes de dictionnaire. Selon, Kasar (2008) si l'on traite d'une seule langue dans un dictionnaire, il s'agit d'un dictionnaire monolingue. Lorsque nous traitons de deux ou plusieurs systèmes linguistiques, nous avons un dictionnaire plurilingue.

**Techniques de création terminologique**:

**La dérivation** la néologie terminologique peut faire appel à la dérivation en privilégiant certains suffixes, notamment ation, age, ment, eur, iste, eur, ance, pour les substantifs, el et ique pour les adjectifs et enfin, iser, ifier pour les verbes. Il peut également y avoir dérivation à partir d'une abréviation, d'un sigle ou d'un acronyme : onusien (de ONU), océriser (de OCR). Les préfixes et les suffixes sont porteurs de sens. Les suffixes peuvent également changer la catégorie grammaticale des mots: le verbe citer devient un substantif dans citation.

**L'emprunt au modèle gréco-latin** :c'est ce qu'on a l'habitude d'appeler les mots savants ; ce modèle est lié à la dérivation car les suffixes et les préfixes y jouent un rôle essentiel (cf. La dérivation ci -dessus)

**La composition :** procédée de formation de termes par combinaison de bases lexicales (radicaux ou termes):

**La néologie sémantique ou reprise d'un élément lexical existant** : un mot existant est réutilisé pour dénommer une notion nouvelle du domaine scientifique et technique; c'est ce qu'on appelle « terminologisation »

**Le calque** :il s'agit de la création d'un terme nouveau qui est une copie adaptée du terme de la langue source. Il s'agit en quelque sorte d'une traduction littérale (dog leg, dans l'industrie du pétrole, traduit par patte de chien en français). On distingue le calque sémantique (bogue/bug) qui s'appuie sur une ressemblance et le calque de forme (libre-service/self service).

**L'abréviation : elle comporte deux sous procédés :**

a) **Troncation :** en progression constante en néologie. Soit, on tronque le début du mot : aphérèse, soit on tronque la fin du mot : apocope ou la troncation + composition = mots valise de l'anglais. Mots de formation récente (se développe surtout après1945**).**
b) **Siglaison le sigle** (épelé): d'origine très ancienne (connu des Hébreux et des Romains). Se développe surtout depuis 1945 en raison du développement de la technologie et de la complexité des administrations. L'acronyme (se prononce comme un mot

**Revue de la litérature.**

Pas mal de chercheurs ont traité des sujets proches au notre. En effet, Mdee (1980) a traité des méthodes de création de terminologie telles que le l'emprunt de termes étrangers et leur localisation, l'emprunt de langues africaines, les acronymes et la dérivation. Les résultats de sa recherche ont révélé que les utilisateurs du swahili la création terminologique basée sur des langues indigènes comme étant la meilleure.

Adolph et ses colaborateurs (2024) ont examiné la stratégie de traduction des termes empruntés de l'Anglais vers le Kiswahili et leurs impacts sur le domaine de la biologie, de la physique et de la chimie à travers des extraits choisis du Dictionnaire de Biologie, Physique et Chimie TUKI (2012). L'objectif principal de cette recherche était d'évaluer la contribution de la traduction des termes anglais à l'ensemble du développement de la langue swahili. Les objectifs de cet article ont été réalisés en s'appuyant sur la Théorie des Terminologies Scientifiques (TTS) développée par Kiingi (1998) et poursuivie par Kiingi et Mwaro-Were (2000, 2001).

En résumé, ces écrits ont discuté des méthodes qui ont été utilisées pour la confection de dictionnaires terminologiques dont leur LC est le Kiswahili, des problèmes de lexicographie, de traduction et de science terminologique déjà présentés. Ces chercheurs ont évalué une à une des méthodes telles que l'emprunt et la ses formes. De plus, ils ont évalué le rôle de la traduction dans la création de terminologie.

Bien que les recherches précédentes à cette étude apportent un éclairage à cette recherche de diverses manières, notre étude suggère sa spécificité en menant une une étude approfondie pour évaluer techniques de création terminologique utilisée pour créer la terminologie des dictionnaires spécialisés, en particulier celle de la LC du DM en particulier et les raisons de l'utilisation desdites techniques.

## CHAPITRE TROIS : METHODOLOGIE DE RECHERCHE

**Ce chapitre parle de la méthodologie de la collecte et de l’analyse des données.**

L a cellecte et l’analyse des données a été guidée par la théorie d’analyse de contenu de Krippendorff (2004) et mis en vigueur par White et Marsh (2006) pour collecter et analyser les données la TTS de Kiingi (1998) a été utilisée pour mesurer le caractère scientifique de la terminologie faisant objet de cette recherché.

## CHAPITRE QUATRE : PRESENTATION, ANALYSE ET INTERPRETATION DES DONNEES

L’analyse de données du corpus nous montre l’utilisation des techniques de création terminologique suivant :

**L’emprunt de termes étrangers,** par exemple: abolumania, noma.

**Adaptation graphique et morphologique de l’emprunt,** par ex: abiotrophy: abiotrofi: kuzeeka mapema kutokana na kufa kwa seli na tishu mwilini kwa sababu ambazo hazijulikani.

**Adaptation morphologique l'emprunt,** par ex: leucoderma: lukodema: ugonjwa wa ngozi wa mabaka meupe (kwa kukosa rangi) ambayo huzungukwa na ngozi ya rangi iliyokolea zaidi.

**Le calque,** par exemple: whooping cough: ugonjwa wa kifaduro

**Siglaison** par exemple: AIDS (Acquired immunodeficiency syndrome): UKIMWI (Upungufu wa Kinga Mwilini) ya kupata (SIUKIKU-si ya kurithi).

**L'abréviation:** par exemple: A.P.H (ante partum haemorrhage) : UKIMWI (Upungufu wa Kinga Mwilini) ya kupata (SIUKIKU-si ya kurithi)

**L'emploi de l'equivalence**, par exemple: impotence: hanithi

**L'emploi de l'equivalence+ explication,** par exemple: Lagnesis: ukware: uchu wa kupindukia wa ngono

**L'emploi de l'emprunt+ un équivalent+ Explication**, par exemple: Jackson's epilepsy: Kifafa cha Jackson: aina hii ya kifafa husababishwa na lesheni katika koteksi-mota ya ubongo.

**L'emploi de l'explication**, par exemple: ulgurant: maumivu makali sana na ya ghafla, huja kama vile umeme wa radi.

**Le calque et explication**, par exemple: cystoparalysis: kupooza kwa kibofu cha mkojo: hali ya kukosekana kwa mawasiliano ya neva katika kibofu cha mkojo.

Motivation d'utilisation de ces techniques de création terminologiques:

La recherche a montré que les mots sont empruntés dans les langues pour diverses raisons. Premièrement, il y a le besoin de vocabulaire dans une langue pour exprimer un concept ou une chose qui n'était pas connue dans la communauté linguistique. Deuxièmement, l'emprunt peut résulter de l'interaction des forces politiques qui conduit également la société à utiliser les mots de la langue dominante, augmentant ainsi le vocabulaire dans la langue cible (Robins, 1980;

Chuwa, 1988). Les méthodes de création des termes utilisées ont été combinées avec la méthode de traduction sémantique ou la méthode de traduction explicative. Ces méthodes n'ont pas été utilisées sans raison. La première raison qui a motivé l'utilisation de cette méthode se trouve dans le Diccionnaire de KT (2003) lui-même.

Troisièmement, ce dictionnaire médical est en Anglais et en Kiswahili. Cela signifie que le dictionnaire commence par une liste de termes en anglais, puis leurs équivalents en swahili.

Diverses raisons motivent l'utilisation de la méthode de traduction par équivalence. Tout d'abord, Jilala (2021) explique qu'une tâche essentielle pour les traducteurs est de rechercher l'équivalent dans des dictionnaires de termes ou sur différents sites web . De plus, ces termes sont utilisés par des institutions internationales et leur confèrent reconnaissance et légitimité à l'échelle mondiale.

**Relation entre les résultats et le cadre théorique**

Cette recherche a été guidée par la théorie d’UMA de Krippendorff (2004). Comme indiqué précédemment, l'analyse de contenu a aidé le chercheur à lire le DM et à analyser le contenu lié au domaine choisi afin de créer des données permettant d'évaluer les méthodes de création de terminologie utilisées par les experts pour élaborer la terminologie du DM. Par la suite, la raison de l'utilisation des méthodes identifiées a été déterminée. Dans le processus de ces méthodes, cinq grands groupes de méthodes ont été identifiés: Emprunt total ou transfert, paraphrase, traduction équivalente, traduction contextuelle et traduction explicative, traduction mot à mot et le calque.

Ainsi, cette théorie constituait- elle un guide solide qui a permis au chercheur de trouver des réponses aux hypothèses de cette étude, accomplissant ainsi ses objectifs, et les résultats de cette recherche eux-mêmes démontrent leur cohérence avec cette théorie.

La Théorie des Termes Scientifiques (TTS), présentée par Kiingi (1992) et développée par Mwaro (1993/2000), a également été utilisée. Cette théorie insiste sur le fait que, lors de la création ou de la formation d'un vocabulaire, le terminologue doit prendre en compte ces huit critères, ce qui nous guide dans l'acceptation ou le rejet d'un certain nombre de termes en Kiswahili.

**CHAPITRE CINQ: RESUME, RECOMMANDATIONS ET CONCLUSIONS**

Ce chapitre a pour objectif de conclure en exposant brièvement les résultats de cette recherche intitulée « **TATHMINI YA MBINU ZA UUNDAJI WA ISTILAHI ZA UWANJA WA TIBA: UCHUNGUZI KIFANI WA KAMUSI YA TIBA, Toleo la 2003 »**.

Cette recherche a été menée à l'Université du Burundi, située dans la ville de Bujumbura. Il s'agissait d'une recherche, réalisée à la bibliothèque de l'Université du Burundi. L'objectif principal de cette étude était d'évaluer les méthodes de création de termes en médecine. Cette étude renfermait cinq chapitres. Le tout premier chapitre concernait l'introduction de cette étude. Dans ce chapitre, le contexte du sujet, le problème de recherche, les objectifs de la recherche, incluant l'objectif principal et les objectifs spécifiques, les questions de recherche, l'importance de la recherche et la portée de la recherche ont été discutés. Ce chapitre a clarifié les fondements de cette recherche. Le deuxième chapitre portait sur les travaux préliminaires réalisés par différents chercheurs sur des sujets étroitement liés à cette recherche. Les écrits discutés dans ce chapitre traitent des stratégies et des méthodologies qui ont été utilisées dans l'élaboration des dictionnaires Anglais-Kiswahili dans divers domaines, en utilisant différentes approches et théories. De plus, ce chapitre a présenté le cadre théorique qui a guidé cette recherche. La théorie d'Analyse de Contenu initiée par Krippendorff (2004) et la Théorie des Termes Scientifiques (TTS), dont le fondateur est Kiingi (1992) ont été utilisées afin d'analyser les méthodes de création de la terminologique et de déterminer les raisons de l'utilisation de ces méthodes. Le chapitre trois traitait la méthodologie de cette recherche. Après une brève

introduction, le domaine de recherché et l'échantillonnage ont été discutés. Les méthodes de collecte de données utilisées dans cette recherche sont la méthode de revue documentaire. En outre, ce chapitre a clarifié l'approche d'analyse des données utilisée, à savoir l'approche descriptive. De même, ce chapitre a présenté les valeurs de la recherche. Le chapitre quatre s'est concentré sur la présentation et l'analyse des données où différentes méthodes de création de la terminologique de la LC du DM ont été d'abord identifiées, puis leur utilisation a été examinée à travers les avis de divers chercheurs ayant mené des recherches pertinentes. Le chapitre cinq a traité du résumé de la recherche, des propositions et la conclusion finale de cette recherche.

**CONCLUSION.**

Les résultats de cette étude ont mis en évidence les méthodes de création de terminologique dans le domaine médical en tenant compte du champ des maladies par le truchement de la LC du DM. Cependant, les domaines présentés dans le DM sont nombreux. D'autres études sont nécessaires pour démontrer dans quelle mesure les méthodes utilisées dans le processus de création de terminologique dans le domaine des maladies sont similaires à celles utilisées pour créer la terminologie d'autres sous domaines médicaux les comme terminologie liée aux médicaments, aux opérations, au matériel et au disciplines associées aux sciences médicales. Les concepteurs des dictionnaires spécialisés dans d'autres disciplines peuvent utiliser des méthodes de création terminologique. Ainsi, est –il indispensable de mener d'autres recherches pour faire une comparaison avec la nôtre. De ce fait, je dis bienvenu à tout chercheur qui se sentirait intéressé à en faire un éventuel prolongement.

# YALIYOMO

IDENTIFICATION DES MEMBRES DU JURY ........ **i**

TABARUKU ........ **ii**

SHUKURANI ........ **iii**

ABSTRACT ........ **iv**

IKISIRI ........ **v**

CONDENSE DU MEMOIRE ........ **vi**

YALIYOMO ........ **xvi**

ORODHA YA VIFUPISHO ........ **xx**

MAJEDWALI ........ **xxii**

AVANT-PROPOS ........ **xxiii**

SURA YA KWANZA ........ **1**

UTANGULIZI ........ 1

1.1. Usuli wa Utafiti ........ 1

1.2. Tatizo la utafiti ........ 5

1.3. Malengo ya utafiti ........ 6

1.3.1. Lengo kuu la utafiti ........ 6

1.3.2. Malengo mahususi ........ 6

1.4. Maswali ya Utafiti ........ 6

1.5. Umuhimu wa Utafiti ........ 7

1.6. Mipaka ya Utafiti ........ 7

1.7. Vikwazo vya Utafiti ........ 9

1.8. Mpangilio wa Utafiti ........ 9

SURA YA PILI ........ **10**

MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA ........ 10

2.1. Ufafanuzi wa Dhana Muhimu ........ 10

2.1.1. Dhana ya Istilahi ........ 10

2.1.2. Mbinu za Uundaji Istilahi ........ 12

2.1.2.1. Unyambuaji na Uambishaji ........ 12

2.1.2.2. Uambatanishaji na Uunganishaji ........ 13

2.1.2.3. Ufupishaji ........ 13

2.1.2.3.1. Akronimu ........ 14

2.1.2.3.2. Uhulutishaji ........ 14

2.1.2.3.3. Ukatizaji ........ 14

2.1.3. Uradidi ........ 14

2.1.4. Upanuzi wa Maana za Maneno........ 15

2.2. Dhana ya Tafsiri na Mbinu za Tafsiri ........ 15

2.2.1. Dhana ya Tafsiri ........ 15

2.2.2. Dhana ya Mbinu za Tafsiri ........ 18

2.2.3. Dhana ya Kamusi ........ 20

2.2.4. Dhana ya Kamusi ya Istilahi ........ 21

2.3. Kamusi ya Tiba (2003) ........ 22

2.4. Mapitio ya kazi Tangulizi........ 23

2.5. Pengo la Utafiti ........ 29

2.6. Mkabala wa Kinadharia........ 30

2.6.1. Mihimili ya UMA........ 31

2.6.2. Hatua za Nadharia ya Uchanganuzi wa Maudhui ........ 32

2.7. Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) ........ 32

2.8. Hitimisho........ 33

SURA YA TATU **........ 34**

MBINU ZA UTAFITI........ 34

3.1. Utangulizi........ 34

3.2. Usanifu wa Utafiti ........ 34

3.3. Mkabala wa Utafiti........ 35

3.4. Eneo la Utafiti ........ 35

3.5. Sampuli na Usampulishaji ....................................................................................................36

3.5.1. Sampuli Lengwa ....................................................................................................36

3.5.2. Usampulishaji ....................................................................................................36

3.6. Mbinu za utafiti ....................................................................................................37

3.6.1. Mbinu za Kukusanyia Data ....................................................................................................37

3.6.2. Mapitio ya Nyaraka ....................................................................................................37

3.6.3. Uchanganuzi wa Data ....................................................................................................38

3.7. Maadili ya utafiti ....................................................................................................39

3.8. Hitimisho ....................................................................................................39

SURA YA NNE **.................................................................................................... 41**

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ....................................................................................................41

4.1. Utangulizi ....................................................................................................41

4.2. Uwasilishaji wa Data ....................................................................................................42

4.3. Istilahi za Uwanja wa Magonjwa katika LL ya *KT* na Mbinu za Uundaji Istilahi Zilizotumiwa 50

4.3.1. Ukopaji ....................................................................................................50

4.3.1.1. Ukopaji wa Moja kwa Moja. ....................................................................................................51

4.3.1.2. Utohozi ....................................................................................................52

4.3.1.3. Ukopaji kwa Uhawilishaji. ....................................................................................................55

4.3.1.4. Uhamishaji na Kisawe ....................................................................................................56

4.3.2. Mbinu ya Usawe ....................................................................................................59

4.3.3. Mbinu ya Tafsiri Sisisi na Utohozi ....................................................................................................62

4.3.4. Tafsiri Sisisi na Ufupishaji ....................................................................................................63

4.3.5. Tafsiri Sisisi ....................................................................................................65

4.3.6. Tafsiri Kimaelezo ....................................................................................................67

4.3.7. Tafsiri Sisisi Fungamanifu ....................................................................................................69

4.4. Sababu za Matumizi ya Mbinu Husika katika Mchakato wa Kuunda Istilahi za LL ya *KT* .........72

4.4.1. Sababu za Matumizi ya Mbinu ya Kukopa ....................................................................................................72

4.4.2. Sababu za Matumizi ya Mbinu ya Tafsiri ya Maana au Mbinu ya Tafsiri Kimaelezo ...........75

4.4.3. Sababu za Matumizi ya Mbinu Tafsiri kwaVisawe ....................76

4.4.4. Sababu za Matumizi ya Mbinu ya Tafsiri Sisisi ....................76

4.5. Uhusiano baina ya Matokeo na Kiunzi cha Nadharia ....................78

4.6. Hitimisho....................80

SURA YA TANO **.................... 81**

MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ....................81

5.1. Utangulizi....................81

5.2. Muhtasari ....................81

5.2.1. Muhtasari kwa jumla ....................81

5. 2.2. Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ....................82

5.3. Mchango wa utafiti huu....................84

5.4. Hitimisho....................85

5.5. Mapendekezo ....................85

MAREJELEO **.................... 86**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| 0 (Anti-) | : Obscenity (Ustara) |
| A | : Appropriateness and Acceptability (Ufaafu na Ukubalifu) |
| BAKITA | : Baraza la Kiswahilila Taifa |
| C | : Consistency (Utaratibu ulio sawa) |
| DM | : Dictionnaire Médical |
| E | : Economy (Iktisadi) |
| Ed.D. | : Docteur en éducation |
| G | : Generativity (Uzalishaji) |
| I | : Internationality (Umataifa) |
| KAKAMA | : Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki |
| KKS | : Kamusi ya Kiswahili Sanifu |
| KT | : Kamusi ya Tiba |
| LC | : Lugha Chanzi |
| LL | : Lugha Lengwa |
| M.A. | : Master of Arts |
| NFZ | : Nadharia ya Fonolojia Zalishi |
| NIK | : Nadharia ya Istilahi za Kisayansi |
| NML | : Nadharia ya Mofolojia Leksika |
| S | : Systemicity (Utaratibu maalum) |
| T | : Transparency (Uangavu) |
| TATAKI | : Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| TUKI | : Taasisi ya Uchunguzi Kiswahili |
| TY | : Tafsiri ni Ya |
| UMA | : Uchanganuzi wa Maudhui |

UNESCO : United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

UVIKO : Ugonjwa wa Virusi vya Korona Vifupisho vninavyounda Akronimu

## MAJEDWALI

Jedwali Na. 4.1 Data za utafiti....42

Jedwali Na. 4.2. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Ukopaji wa Moja kwa Moja....51

Jedwali Na. 4.3 Istilahi Kutokana Utohozi....53

Jedwali Na. 4.4 Istilahi Kutokana na Mbinu ya Ukopaji kwa Uhawilishaji....55

Jedwali Na.4.5. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Uhamishaji na Kisawe....57

Jedwali Na.4.6. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Kisawe na Maelezo....60

Jedwali Na. 4.7. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Sisisi na Utohozi....62

Jedwali Na.4.8. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Sisisi na Ufupishaji....64

Jedwali Na.4.9. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Sisisi....66

Jedwali Na.4.10. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Kimaelezo....68

Jedwali Na.4.11. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Sisisi Fungamanifu....70

**AVANT-PROPOS**

La problématique de la terminologie liée à la traduction n'est pas étrangère aux yeux des traducteurs swahilis. Le programme de master en traduction et interprétation à l'Université du Burundi invite les futurs traducteurs- interprètes professionnels à se doter davantage de la terminologie bilingue sous forme de glossaires relevant de différents domaines tant techniques, littéraires que scientifiques. Cette tâche n'est pas facile à réaliser. En plus, elle nécessite la maitrise de techniques de création terminologique car le travail de recherche des termes équivalents d'une LD à LC constitue l'étape inévitable en traduction.

En outre, dans notre pays, le Burundi, il n'existe pas de programmes de traduction axés sur les langues techniques, alors que dans d'autres pays, les traductions liées au droit, à la santé et à l'éducation ont été développées comme des disciplines académiques, sans aucun doute, en analysant les stratégies pour faire face au manque de terminologie. Il est évident que, à travers ces disciplines, les étudiants maîtrisent les techniques de traduction des textes techniques comme ceux du domaine médical.

Ainsi, pour relever ces défis, nous avons opté pour l'analyse des techniques de création terminologique du domaine médical qui ont été utilisées par les auteurs du dictionnaire bilingue ; Dictionnaire médical (Anglais- Swahili) publié en 2003 par des experts en terminologie et en médecine en se focalisant sur la LC (le Kiswahili). Les techniques qui seront mis en lumière constitueront une référence fiable pour les traducteurs qui font face sans cesse à des nouveaux termes qui se manifestent suite à l'interconnectivité du monde qui est devenue un village planétaire.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1. Usuli wa Utafiti

Takribani lugha 7000 zinatumika duniani kote UNESCO (2024) ingawa si jambo rahisi kuamua hasa idadi ya lugha zinazozungumzwa kutokana na ugumu wa kuchora mipaka sahihi kati ya lugha kadhaa au lugha na lahaja. Hakuna jamii ya watu inayoweza kuwa katika hali ya upwekee milele na milele. Aidha, binadamu anapoishi katika mazingira yake hutafuta kila namna ya kuyakabili mazingira hayo kwa kuchunguza, kutafiti, kudadisi na kuvumbua vitu vipya ndani ya jamii, Jilala (2022). Kwa hiyo, uundaji wa istilahi ni jambo iisiloweza kuepukika katika lugha yoyote ile, Mwaro (2000).

Nao utandawazi ulisababisha hali ambayo watu wa ulimwengu hawana budi kuwa jamii moja. Ukuaji wa mataifa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiteknolojia kutokana na kuathiriana na ulimwengu mpana ulisababisha kuwa jambo linalotendeka katika nchi moja kuathiri mataifa mengine ya ulimwengu. Ulimwengu umekuwa mdogo kiasi kwamba bila hata uhitaji wa mtu, anajikuta kwenye haja ya kuwasiliana na wenye lugha tofauti naye. Kwa hiyo, bila kiungo kinachoziunganisha jamii za ulimwengu, ni vigumu kwa jamii kuweza kuwasiliana na kuelewana, Jilala (2022). Bila shaka, kuna haja ya kuhawilisha maarifa, taarifa na mawasiliano ya jamii, kukuza wa uchumi, elimu na maendeleo ya jamii kwa jumla, Jilala (2021).

Mawasiliano nayo ulimwenguni hayawezi kufanyika na jamii zikaelewana kwa sababu ya tofauti ya lugha zinazozungumzwa na jamii hizo, Newmark (1988). Hali hii inaonyesha kuwa jamii zinahisi hitaji la daraja linalounganisha lugha zinazotumiwa. Mbinu nzuri ya kulijenga daraja hilo la mawasiliano na kutumia tafsiri na ukalimani. Tafsiri inatumika kama daraja na kiungo kinachoziunganisha jamii za ulimwengu, kutokana na mwingiliano wa tamaduni na mahusiano ya kijamii duniani, Jilala (2014). Matatizo ya kiistilahi katika mchakato wa kutafsiri

na jinsi mfasiri anavyoweza kuyatatua si jambo geni, Bwenge (2000) wakati dhima ya istilahi kwa jumla ni kufanikisha mawasiliano baina ya watu wanaoshiriki mawasiliano kuhusu uwanja au taaluma fulani, Galinski (1985).

Bila tafsiri hakuna ambaye angeweza kufahamu ulimwengu wa mwingine au jamii nyingine wala kupata maarifa mapya, kuvumbua vitu vipya na hata kueneza utamaduni, ujuzi na maarifa mapya, Jilala (2022). Tafsiri ina jukumu kubwa kwa binadamu. Kama njia ya mawasiliano, tafsiri hutumika kutolea maelezo ya kibiashara, hutumika kwenye vyombo vya habari, nyaraka rasmi kama mikataba, ripoti za kimataifa, makala za kitaaluma na vitabu vya kiada na ziada, Mwajuma (2018).

Kwa wanadamu, tafsiri ni ni mbinu waliobuni ili iwezeshe kuwasaidia wanajamii kutoka jamiilugha fulani kuelewa lugha inayozungumzwa na jamii nyingine na hata kusaidia katika mawasiliano. Shughuli za tafsiri na ukalimani hufanyika kila siku katika maisha ya mwanadamu, Malangwa (2012). Kauli hiyo inathibitisha kuwa uhitaji wa tafsiri si wa wakati huu ambapo kumekwishafanywa tafiti mbalimbali kuhusu idadi ya lugha zinazopatikana duniani ila ni wa enzi za kale. Hata katika kipindi cha ujio wa wageni, hasa wakoloni, tafsiri ilifanyika ili kurahisisha mawasiliano baina ya wakoloni na jamii walizozitawala.

Mwansoko (1996) anaelezea tafsiri kama taaluma iliyotokana na haja ya kuieneza elimu ya Wamisri kule Ulaya. Hata hivyo, elimu hii ilipigwa vita kule Ulaya kwa kudhaniwa kuwa ni mafundisho ya kipagani. Baadaye, elimu hii ilionekana kuwasaidia Waarabu kujiendeleza kisayansi. Wataalamu wa Ulaya walichukua vitabu vya sayansi vya Kiarabu na kuvitafsiri ili kupata maarifa hayo. Huu ulikuwa wakati wa mwamko mpya wa taaluma hii ya tafsiri kule Ulaya, Jepkoech (2020). Katika kipindi hicho, kazi mbalimbali zilitafsiriwa ili kuitambulisha lugha ngeni kwa wenyeji na lugha asilia kwa wageni, Mwansoko (1996).

Barani Afrika, matunda ya juhudi za utafsiri si ya jana wala juzi. Mshindo (2010) anaeleza kuwa sayansi na taaluma nyingi zilizoanza Misri katika miaka ya 3000 na zaidi kabla ya kuzaliwa Kiristo zilitufikia sisi na mataifa ya Ulaya kwa njia ya tafsiri. Ingawa tafsiri ni taaluma kongwe duniani, bado inaelezewa kuwa ni taaluma changa katika nchi za Afrika Mashariki hususan Tanzania, Jilala (2024). Mwansoko (1996) anaeleza kuwa taaluma ya tafsiri ilianza kufundishwa nchini Tanzania katika miaka ya 1970 tu.

Suala la istilahi kwa kuhusiana na tafsiri si geni machoni mwa wafasiri wa Kiswahili. Kama anavyokiri Bwenge (2000) suala hili limekuwa likijadilia sana katika semina, warsha, makongamano ya kimataifa na ya kitaifa kutoka miaka ya nyuma hadi leo. Kwa mfano, suala la matatizo ya Istilahi za Kisayansi na kiufundi katika kutafsiri matini za nyanja malumu limekuwa likijadiliwa katila Shirika la Kimataifa la Wafasiri (FIT) kuanzia miaka ya 1950 kama anavyotukumbusha Stoberski (1981).

Maoni ya wanaismu hawa wawili yanasisitiza umuhimu wa kumilisi mbinu za uundaji wa istilahi kwa mfasiri. Mfasiri ni mtumiaji wa istilahi kama atumiaye msamiati ya kawaida. Matumizi ya istilahi ambayo yanasaidia kutimiza moja kati ya dhima za istilahi yaani kuhawilisha maarifa ya kupitia mchakato wa kutafsiri matini kutoka uwanja wa sayansi na teknolojia au wa kiufundi kwa ujumla. Dhima hiyo inathibitisha ukweli kuwa mfasiri ni mmojawapo wa watumiaji wakubwa wa istilahi.

Hata hivyo, taaluma ya tafsiri inayo lengo la kuhamisha maarifa na ujumbe kutoka lugha moja kwenda ligha nyingine kwa muda mrefu, Munday (2001) inaendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo hutokana na ugumu wa kazi ya tafsiri yenyewe, Gambier (2011). Pia, tafsiri si kitendo rahisi cha kupitisha ujumbe kutoka lugha moja kwenda nyingine ila ni kitendo changamano kinachohusu uakifishaji, njia za kueleza wakati, tarehe na mahali, Moora (2013).

Ugumu wa kazi ya tafsiri unatokana na ukosefu wa benki za istilahi na visawe wakati kazi kubwa ya mfasiri ni kutafuta visawe, Jilala (2021). Istilahi na visawe havipatikani pengine isipo katika Kamusi za Istilahi zilizotungwa na wanataaluma kutoka nyuga husika kama vile uga wa tiba, uga wa biashara na uchumi, uga wa sayansi na teknolojia, uga wa sheria, uga wa kidiplomatia, uga TEHAMA, n.k. Ugumu wa kazi ya tafsiri unawiana na uugumu wa uundaji wa istilahi za tiba ambayo si kazi rahisi. Kama inavyoelezwa na Moora (2013) ugumu wake unatokana na lugha ya kitabibu kutumiwa na kundi maalum la watu, yaani wataalam wa tiba. Hali hiyo inasababisha ukuzaji wa istilahi hizo katika lugha nyingine kuwa mgumu zaidi kwa kuwa si lugha ambayo hutumiwa na watu wa kawaida katika maisha yao ya kila siku.

Hata hivyo, kutokana na utandawazi, maarifa mapya huzuka na kuongeza ugumu wa kazi ya tafsiri kutokana na istilahi zinazohitaji kutafutiwa visawe ili daraja la mawasiliano lidumishwe kwa tafsiri. Isitoshe, ugumu huo unatokana na uga ambako kazi ya tafsiri inahusika. Katika nchi yetu ya Burundi hakuna programu za tafsiri zinazojikita katika nyuga za kiufundi wakati katika nchi nyingine, tafsiri zinazohusiana na sheria, afya na elimu zimeendelezwa kama taaluma za kiusomi, Wadensjo (1998) bila shaka na kuchambua mikakati ya kukabiliana na ukosefu wa istilahi. Ni dhahiri kuwa, kupitia taaluma hizo ndiko wanafunzi wanakomudu mbinu za kutafsiri matini za kiufundi kama vile matini za uga wa Tiba.

Isitoshe, kama anavyosema Nina (2008) taaluma ya tiba inahitaji utaalamu wa hali ya juu kwa kuwa taaluma ya kimatibabu huwa na upekee wake. Kwa sababu hiyo, mfasiri anahitaji kuwa zaidi ya mfasiri kwani tafsiri za kimatibabu ni suala linalohitaji uangalifu mkubwa kwa kuwa huathiri afya ya mwanadamu, Moora (2013). Jambo hilo si rahisi kulitekeleza wakati visawe vya istilahi vyote haviwezi kupatikana katika kamusi thaniya.

Utafiti huu ninaonuia kufanya unalenga kubaini istilahi za uwanja wa tiba kutoka Kamusi *ya Tiba* (*KT*, kuanzia sasa), Toleo la 2003, kutahmini mbinu za uundaji wa istilahi zilizotumiwa katika mchakato wa uundaji wa istilahi wa uwanja wa magonjwa na kutoa sababu zilizochochea matumizi ya mbinu hizo.

Kwa kutathmini mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa na wanazuoni waliobobea katika taaluma ya afya na istilahi katika mchakato wa kuundia istilahi za Lugha Lengwa (LL, kuanzia sasa) ya *KT*, mtafiti ana matumaini ya kuwasaidia wafasiri kupata uwezo wa kujiundia istilahi wakati kuna mfumuko wa istilahi kutokana na utandawazi.

## 1.2. Tatizo la utafiti

Pamoja na mfasiri kuwa mmojawapo wa watumiaji wakubwa wa istilahi, si wakati wote anapotafsiri matini za kisayansi au za kiufundi anapata istilahi anazohitaji na zilizo sahihi papohapo, Bwenge (2000). Kazi kubwa katika tafsiri ni kutafuta visawe katika lugha lengwa (LL, kuanzia sasa). Visawe vinapokosekana ndipo mbinu nyingine za kuhawilisha ujumbe kwenda LL hutumiwa, Jilala (2021). Kutokuwepo kwa istilahi mbalimbali katika LC na LL ni tatizo kubwa katika kazi ya tafsiri. Aidha, ni miongoni mwa matatizo yanayowakumba wafasiri kipindi hiki cha utandawazi na kasi kubwa ya maendeleo ya kisayansi na teknolojia ambayo haiwiani na kasi ya maendeleo ya kiistilahi. Uundaji wa istilahi hufanyika kiholela wakati mfasiri anaombwa kueleza dhana mpya za kiufundi katika LC kwenda lugha za kitaifa ambazo istilahi hizo ni geni na zinahitaji kuingizwa ili zirahisishe mawasiliano. Mara kwa mara tafsiri za kimatibabu zinapotosha maana kwa kuwa wengi wa wahudumu wa afya wanatumia dhana za kijumla kueleza masuala mahususi ya kimatibabu, Mabasa ( 2005) na kusababisha utata wa tafsiri. Kwa mantiki hiyo, mfasiri hana budi kupitisha ujumbe usiokuwa na utata wa maagizo na maelezo ya istilahi za tiba. Vilevile, ni vigumu kumudu mbinu za uundaji wa istilahi ikiwa mfasiri hana ujuzi wa kutosha katika uundaji wa istilahi za taaluma kama vile taaluma ya

tiba. Hivyo basi, licha ya baadhi ya tafiti kushughulikia eneo hilo, hakuna tafiti zilizojikita katika kutathmini mbinu za uundaji wa istilahi za LL ya *KT*.

Kutoshughulikia utafiti huu kutawasababisha wahudumu wa uga wa tiba kutonufaika katika kupata huduma ya tafsiri sadifu. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu unalenga kutathmini mbinu za za uundaji istilahi katika mchakato wa uundaji wa istilahi za LL ya *KT* na kutoa sababu ya matumizi ya mbinu hizo.

## 1.3. Malengo ya utafiti

Malengo yanayoongoza utafiti huu ni haya yafuatayo :

### 1.3.1. Lengo kuu la utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini mbinu za uundaji istilahi zilizotumika katika uundaji wa istilahi za LL ya *KT*.

### 1.3.2. Malengo mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni :

(i) Kubainisha istilahi zinazohusu magonjwa katika KT.

(ii) Kufafanua mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa kuundia istilahi zinazohusu magonjwa katika LL ya KT.

(iii) Kueleza sababu ya matumizi ya mbinu za kuundia istilahi zinazohusu magongwa ya LL ya *KT*.

## 1.4. Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na maswali yafuatayo:

(i) Ni zipi istilahi zinazohusu magonjwa katika LL ya KT?

(ii) Ni mbinu gani za uundaji istilahi zilizotumiwa kuundia istilahi zinazohusu magonjwa katika LL ya *KT* ?

(iii) Ni sababu zipi za matumizi ya mbinu hizo kuundia istilahi zinazohusu magongwa ya LL ya *KT*?

## 1.5. Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha watu wengi. Kwanza, utafiti huu utaziweka bayana istilahi zinazohusu magonjwa zipatikanazo katika *KT*. Utafiti huu tawasaidia waundaji wa istilahi na wafasiri kufahamu mbinu za uundaji istilahi zilizotumia na mabingwa wa tiba na wa uundaji istilahi na sababu zilizochochea matumizi ya mbinu hizo. Pili, utafiti huu utatoa mwanga kwa wafasiri ambao hawana budi ya kuudhibiti mfumko wa istilahi au msamiati unaolemea lugha ya Kiswahili. Utawawezesha kupata na kumudu mbinu za kuundia istilahi na kukidhi mahitaji ya kudumisha daraja la mawasiliano.

Tatu, utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa kwa wahudumu wa kitabibu ambao wanahitaji huduma ya tafsiri. Nne, ni mchango wa kiusomi ambao utasaidia kuchochea mjadala na mchango zaidi katika mjadala wa uundaji wa istilahi ambao unaonekana kutoandikiwa na kutafitiwa sana. Kwa hiyo, andiko hili litakuwa ni marejeleo muhimu kwa watakaochunguza zaidi mbinu za uundaji istilahi hasa ukizingatia kwamba hili ndilo andiko la kwanza linalojadili kwa mapana na lililoandikwa kwa lugha ya Kiswahili nchini Burundi. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kurejelewa katika tafiti zitakazofuata, na hivyo kuziba mapengo ambayo yapo kwa wafasiri na wanaistilahi watakaosoma matokeo yake.

## 1.6. Mipaka ya Utafiti

Kamusi za istilahi ni nyingi na isingewezekana kuzitumia zote katika utafiti huu. Kwa hiyo, utafiti huu uliteua *KT*. Kamusi hiyo iliteuliwa kwa sababu mbili. Kwanza, watunzi wake ;

Profesa Mwansoko, ni mtaalamu wa uundaji wa istilahi. Naye Dkt. Mwita, ni bingwa katika taaluma ya udaktari. Pili, TUKI ni asasi iliyopewa dhamana ya kufanya utafiti katika nyanja zote za lugha ya Kiswahili, ikiwa ni pamoja na uandikaji wa kamusi mbalimbali, iliipitia kazi hii kuona kama kanuni za uandishi wa kamusi zilizingatiwa. Kwa hiyo, kazi ya watalamu hao ilipitiwa na watalamu wa utabibu kwa ombili TUKI. Tatu, *KT* ni kubwa kuliko kamusi zingine kwa kuwa Licha ya waandishi kuunda istilahi, baadhi yake walizipata kutoka kwenye marejeo mbalimbali, zikiwemo kamusi. Vyanzo vingine vya istilahi zilizoingizwa katika *KT* ni mikutano na warsha mbalimbali ambazo Wizara ya Afya huwashirikisha watalaam kutoka BAKITA na TUKI. Aidha, maongezi ya kawaida na watu mbalimbali yamewasaidia waandishi kurutubisha istilahi zilizomo. Isitoshe, sayansi ya tiba ina mchango mkubwa kwani ni kiini cha kuhudumia binadamu kiafya. Hali hii ilimpa matumaini ya kupata data ya kutosha inayohusu uga ulioteuliwa kufanyiwa uchunguzi. Taaluma ya tiba ni pana na maarifa yaliyotolewa katika *KT* kupitia istilahi ni mengi. Kwa hiyo, haiwezekani kujihusisha na uchunguzi wa istilahi zote zilizomo katika *KT*. Mtafiti alishughulikia istilahi za uwanja wa magonjwa. Uwanja huu uliteuliwa miongoni mwa nyanja nyingi kwa sababu mbalimbali. Kwanza, uga wa magonjwa ni muhimu kwa binadamu. Mgonjwa anapoomba huduma ya afya anaagizwa na tabibu kupimisha ugonjwa katika maabara. Kutokana na matokeo anaambiwa ni ugonojwa upi unaomkumba na namna ya kupata dawa alizopewa, namna ya kumponya kama vile kupitia upasuaji au kuelekezwa kwa daktari bingwa wa ugonjwa fulani wakati anapogundua kuwa yeye hana ujuzi wa kutosha wa kumhudumia kiafya ili aweze kukomesha ugonjwa unaomlemea mgonjwa. Pili, Lugha ya kitabibu ina asili ya lugha nyingi, hususan, Kilatini, Kigiriki, Kijerumani, Kiingereza n. k. Hali hiyo inasababisha ugumu wa kuelewa na kueleza magonjwa, vyanzo vyake na mbinu na mikakati ya kuyakinga au kuyakomesha. Mwisho, uwanja wa magonjwa ni nguzo ya sekta afya. Mangonjwa yangelikosekana nyanja zinazoambatana na

uwanja huo kama vile matabibu, sayansi za tiba, vifaa na mazingira ya tiba, madawa zisingelikuwepo.

## 1.7. Vikwazo vya Utafiti

Vikwazo katika utafiti kwa namna yoyote haviwezi kuepukika. Kwa mujibu wa Durrel (1982) vikwazo katika utafiti ni vitu au mambo ambayo hukwaza mchakato wa uendeshaji wa utafiti. Hivyo katika utafiti huu vikwazo ambavyo vilijitokeza ni ukosefu wa vitabu muhimu kurejelewa matkabani ya Chuo kikuu cha Burundi. Vitabu vingi na makala vinavyopatikana mtandaoni vinahitaji kununuliwa kwa kutumia pesa za kigeni. Kwa kuwa mtafiti hakupata pesa za utafiti hakuweza kununua vitabu mbalimbali ambavyo vingelimsaidia kuendeleza utafiti wake. Mtafiti alitumia maandiko aliyoyakuwa mtandaoni na mengine yaliyotumiwa na watafiti wengine wa nje ya nchi ya Burundi kupitia barua pepe. Vikwazo vingine ni ukosefu wa mfumo rasmi ya tasnifu za uzamili katika lugha ya Kiswahili ulioidhinishwa na Chuo Kikuu cha Burundi. Ilmbidi mtafiti atumie mfumo wa kifaransa kwenye ukurasa wa kifuniko na kuiwasilisha mada tu katika Kiswahili.

## 1.8. Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu una jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi wa utafiti huu, una usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahususi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Sura ya pili inahusu mapitio ya mandiko ambayo ndani yake kulijadiliwa kazi tangulizi na nadharia za utafiti. Sura ya tatu inazungumzia mbinu za kukusanyia data, mbinu za kuchanganua data na udhibiti wa data. Sura ya nne inahusu uchanganuzi wa data kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu. Sura ya tano inatoa muhtasari na kujadili matokeo ya utafiti huu na kisha kutoa mapendekezo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

Sura hii inahusika na kuwasilisha tafiti mbalimbali zilizofanywa kabla ya utafiti huu ambazo zilichapishwa katika vitabu, makala na tasnifu ili kupata maarifa ambayo yanahusiana na mada hii kwa ajili ya kubainisha pengo ambalo utafiti huu ulishughulikia. Kwa hiyo, kutazungumziwa, dhana ya istilahi na mbinu za uundaji istilahi, dhana ya Kamusi na kamusi ya istilahi. Pia, kutajadiliwa mapitio ya kazi tangulizi na pengo la utafiti na kufafanua viunzi va nadharia zilizoongoza utafiti huu.

## 2.1. Ufafanuzi wa Dhana Muhimu

Katika sehemu hii kunaelezwa dhana muhimu ambazo zinahusiana na utafiti huu, na ambazo zinasikika katika mada ya utafiti huu.

### 2.1.1. Dhana ya Istilahi

Wataalamu wametoa fasili mbalimbali kuhusu dhana ya istilahi. Akida (1975) anafasili istilahi kama maneno yanayotumika katika sanaa ya sayansi. Kwa mujibu wa TUKI (1990) istilahi yaweza kuwa alama, herufi, neno au kifungu cha neno. Naye Mwangomango (1977) anafasili istilahi kuwa ni maneno ya kitaaluma ambayo yanatumiwa katika kila taaluma na sharti kila taaluma itenge maneno kwa ajili ya maelezo maalumu .TUKI (2019) na Massamba ( 2009) wanaafikiana na watangulizi wao Akida na Mwangomango na kufasili istilahi kama neno maalumu linalowakilisha dhana katika uwanja maalum wa maarifa/taaluma kama vile siasa, uchumi, sayansi na teknolojia, na mengine .Aidha, istilahi ni mfumo wa msamiati maalumu unaotumika katika taaluma mahsusi.

Mtazamo wake unawiana na mtazamo wa Bwenge (1996) kwa kuwa dhana ya istilahi inafungamana na dhana ya nyanja maalumu katika jumla ya maarifa ya binadamu. Kila uwanja au taaluma una msamiati wake maalum unowakilisha dhana muhimu unohusika. Pia, istilahi kwa maana ya taaluma inayoshughulikia. Kwa mujibu wa Mwaro (2000) istilahi ishara ya kiisimu inayorejelea dhana moja au zaidi. Istilahi yaweza kuwa neno, au kifungu cha maneno, herufi, akronimu nk. Istilahi, tofauti na neno ambalo hutegemea muktadha, hutegemea mfumo wa dhana ambamo dhana hupatikana.

Uundaji ni uzalishaji wa istilahi/neno mpya kuwakilisha dhana fulani pale ambapo halipo, Mwaro (2000). Kwa mujibu Mwaro ( 2000) na Kevogo (2020) dhana ya istilahi ina mitazamo miwili. Kwanza, dhana ya istilahi ni jumla ya maneno. Pili,dhana ya istilahi ni taaluma inayojishughulisha na nadharia, misingi, mbinu na miongozo ya uundaji wa istilahi. Kulingana na TUKI (2013) na BAKITA (1974) istilahi ni maneno yanayotumika katika taaluma fulani ili kukidhi matakwa ya taaluma hiyo. Naye Nimessi (2022) anadai kuwa istilahi inaweza kufafanuliwa kwa namna nyingi tofauti. Kwanza, istilahi inaweza kufafanuliwa kama taaluma ya uundaji wa maneno. Pili, istilahi inaweza kujadiliwa kama jumla ya maneno yanayotumika katika uga maalumu. Mwisho, istilahi inaweza kuangaziwa kama kanzidata ya maneno yanayotumika katika fani maalumu.

Maoni ya watafiti hao waliozungumzia hapo juu yanathibitisha kuwa dhana ya istilahi ni pana kwa kuwa ina mitazamo tofauti. Dhana ya istilahi inaweza kufasiliwa kama neno au kifungu cha maneno linalotumiwa katika uwanja wa kiufundi au taaluma ambayo lengo lake ni kuendeleza nadharia, mbinu ,misingi na miongozo ya uundaji wa istilahi, bila ya kusahau kanzidata ya maneno yanayotumika katika fani fulani kama vile tiba, komputa, kemia, biolojia, diplomatia,n.k hususan kipindi hiki cha utandawazi.Katika mchakato wa kushughulikia istilahi kama taaluma ndipo panazungumziwa mchango wa taaluma ya istilahi, uhusiano wake na taaluma zingine za isimu na mipaka yake.

### 2.1.2. Mbinu za Uundaji Istilahi

Suala la mbinu za uundaji wa istilahi za Kiswahili ni muhimu. Kutokana na umuhimu wake inaonekana kwamba limewavutia wasomi na wataalamu mbalimbali tangu karne ya 20.Watalamu hao ni kama Polome (1967), Ohly (1977), Temu (1972, 1984), Nabhmy (1982), Gibbe (1983), Kapinga (1983), Mbaabu (1985), Mdee (1986), Mwansoko (1989, 1990, 1993) na Tumbo na Mwansoko (1992), kuwataja hao tu miongoni mwa wengine.

Ni muhimu isisitizwe hapa kwamba wataalamu wa awali walioshughulikia mbinu za uundaji wa istilahi (k.v. Ohly, 1981; Tumbo, 1981; Mwasoko, 1990; na Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992) walizibainisha mbinu hizo katika makundi mawili. Nazo ni njia zitokanazo na 'Kiswahili chenyewe' kama vile minyambuliko, miambatamo, miungmo, uongezaji au upaji maama mpya kwa mpya kwa mmeno yaliyopo, ufupisho au akroninimu; na njia ya kukopa istilahi kutoka lahaja na lugha nyinginezo.

#### 2.1.2.1. Unyambuaji na Uambishaji

Miongoni mwa njia ambazo zinatumika zaidi katika uundaji wa maneno mapya kuna unyambuaji na uambishaji.Unyambuaji umeelezwa na Mwansoko (1990) na Bwenge (1996) kama uundaji wa istilahi kwa kuambatisha viambishi kwenye mzizi au shina la neno. Kwa kutumia mbinu hiyo neno hubadili kategoria yake.

Uambishaji nao unafasiliwa TUKI (1990) kama utaratibu wa kuweka viambishi kwenye mzizi wa neno ilikulipa mama mahsusi. Mwaro (2000) akifasili uambishaji anaeleza kuwa ni aina ya mbinu ya uundaji wa istilahi ambapo viambishi awali huongezwa kwenye mzizi wa jina ili kuunda istilahi ya kategoria ile lie. Aidha, anasisitiza matuniizi ya viambishi awali vya ngeli kwa sababu, kinyume na unyambuaji, katika uambishaji viambishi awali tu ndivyo hutumika.

Fasili za watalamu hao zinathibitisha utofauti uliopo kati ya mbinu ya unyambuaji na uambishaji.Kwa kunyambua neno au istilahi linabadili kategoria yake wakati mbinu ya uambishaji haisababishi neno au istilahi kubadili kategoria yake.

### 2.1.2.2. Uambatanishaji na Uunganishaji

Uambatanishaji wa istilahi ni utaratibu ambao unahusu kuteuliwa na kuchukuliwa kwa maneno mawili (au zaidi) yenye maana na yaliyo huru na kuyaunganisha ili kuunda jina moja lenye dhana moja mpya. Kwa mujibu wa Havyarimana (2024) mbinu ya uambatanishaji husaidia kuingiza maneno mengine katika lugha kwa kuunganisha maneno na kuyafanya kuwa neno moja lenye maana.Kwa mujibu wa Jilala (2021) mbinu ya uambatanishaji na uunganishaji anaizungumzia kwa kutumia dhana ya ufungamanifu. Japo ni mbinu ya tafsiri, mbinu ya ufungamanifu inatumiwa na wataalam katika kuunda istilahi za sayansi na teknolojia huku ikiambatana na mbinu ya muambatano ya uundaji wa istilahi.

Mtazamo wa wataalam hao unaungana mkono kwani mchakato wa kutumia mbinu hio unahitaji kuwepo kwa angalau maneno mawili ambayo hutiwa pamoja kwa kuunganishwa au kufunganishwa ili yaweze kuunda neno moja lenye dhana moja jipya

### 2.1.2.3. Ufupishaji

Ufupishaji au vifupisho ni matumzi ya sehemu za maneno katika kuunda istilahi. Kwa mujibu wa Bwenge (1996) ufupishaji maneno yanayotuimiwa kwa pamoja kwa kuchukua herufi za mwanzo tu za mnaneno hayo. Kwa mujibu wa Mwaro (2000) kuna aina tatu za ufupishaji ambazo ni akronimu, uhulutishaji na ukatizaji.

**2.1.2.3.1. Akronimu**

Akronimu inachukuliwa kuwa ni aina ya ufupishaji ambapo jina, istilahi au neno linatengenezwa na ufupisho wa maneno yanayotumiwa kwa pamoja kwa kuchukua silabi ya kwanza, silabi mbili za mwanzo, silabi tenzi za kati au hata neno zima. Mifano: UKIMWI: Ukosefu wa Kinga Mwilini.

**2.1.2.3.2. Uhulutishaji**

Uhulutishaji ni mfanyiko wa kuendeleza istilahi ambapo mofimu huru mbili au zaidi huchanganywa au huungwa ili kuunda neno.

**2.1.2.3.3. Ukatizaji**

TUKI (1990) inafafanua neno ukatizaji kama hatua ya kufupisha neno kwa kuondoa sehemu za mwanzoni na mwishoni. Wataalam wengine walioshughulikia mbinu ya ukatizaji ya uundaji istilahi za Kiswahili k.v. Temu (1984), Njeru (1990) na Irira (1990) wanakubaliana kuwa ukatizaji ni aina ya ufupishaji ambapo neno hujengwa kimkato kwa kuondoa sehemu ya mwanzoni au mwishoni mwa neno hilo, pasi na kubadilisha maana yake.

**2.1.3. Uradidi**

Dhana ya uradidi kama mbinu ya uundaji wa istilahi katika Kiswahili ilijadilia na wataalam mbalimbali. Mbaabu (1992) anadokeza kwamba uradidi au "uradufu" ni jambo linalojitokeza kwa wingi katika lugha za Kibantu. Kwa mujibu wa Rubanza (996) uradidi ni mojawapo ya mifanyiko inayotumiwa katika uundaji wa maneno ya Kiswahili ambapo neno, jina, mofimu, mizani au silabi hurudiwarudiwa katika nomino. Lengo kubwa la uradidi ni kusisitiza jambo au hali fulani. Naye Mwaro (2000) anafasili uradidi kama mfanyiko unaoonyesha kutendeka kwa mifanyiko au kitu au jambo mara kwa mara, yaani ile hali ya mazoea hudhihirika wazi.

Mtazamo kupitia wataalam mbalimbali unadhihirisha kuwa mbinu ya uradidi inatekelezwa kwa kurudia ama mzizi wa neno au kurudia mizani ya kwanza. Hali ya mazoeza yaani ya kutendeka mara kadhaa kwa tendo ni chanzo cha matumizi ya mbinu ya uradidi.

### 2.1.4. Upanuzi wa Maana za Maneno

Upanuzi wa maana za maneno ni mfanyiko mmojawapo muhimu wa kuendeleza leksikoni ya Kiswahili, ambapo neno lililopo kwenye lugha hupewa maana zaidi ya maana yake ya awali. Mwanalugha yachina (1981) akizungumzia sifa za matumizi ya mbinu ya upanuzi wa maana za maneno anasititiza kuwa matumizi yake yamesaidia kukuza istilahi za Kiswahili na anatoa mfano wa maneno kaina vile ndege, tawi, piga kura na intego ambayo maaana yake asilia imebadilika kutokana na kuongezwa kwa maana na matumzi maalum ya kisasa. Mwansoko (1992) anasisitiza kwamba kuongeza maana au kuyapa maneno maana finyu kuliko ile ya awali haufanywi 'vivi hivi tu,' bali kwa kufuata mantiki ya uhusiano kati ya maana ya kawaida, au ya msingi na lie ya kiistilahi.

## 2.2. Dhana ya Tafsiri na Mbinu za Tafsiri

### 2.2.1. Dhana ya Tafsiri

Dhana ya tafsiri imekuwa ikijadiliwa na wataalamu wengi kwa kuwa si mpya kiusomi ; miongoni mwa hao ni kama Catford (1965) ; Taber (1969) ; Mwansoko (1996); Newmark (2003) na Munday (2012).

Kwa mjibu wa Caford (1965) kutafsiri ni kuchukua mawazo yaliyomo katika maandishi kutoka lugha moja (lugha chanzi/ LC) na kuweka badala yake mawazo yanayolingana na hayo kutoka lugha nyingine (lugha lengwa/ LL). Tunatambua kupitia kauli yake kuwa tafsiri inahusu maandishi tu.

Naye Nida na wenzake ( 1969) kutafsiri hujihusisha na kuhamisha ujumbe katika lugha lengwa ambao ni linganifu kutokana na ule wa lugha chanzi kwa kuzingatia maana na mtindo.

Pia, wanaeleza kuwa tafsiri hujumuisha kuzalisha upya ujumbe wa lugha chanzi kwa kutumia visawe vya asili vya lugha lengwa vinavyokaribiana zaidi na lugha chanzi kimaana na kimtindo. Wao wanatilia mkazo uzalishaji upya wa ujumbe kwa kutumia visawe asili vinavyokaribiana na matini chanzi kimaana na kimtindo. Kwa mantiki hii, tunaweza kusema kuwa tafsiri ni ujumbe uliopo katika maandishi ambayo asili yake si lugha ya matini inayosomwa.

Kulingana na Nord (1977) tafsiri imebadilika sana na imekuwa muhimu kuzingatia yaliyomo katika matini chanzi kuhakikisha kuwa yamehawilishwa katika matini lengwa na wala si kutafsiri maneno tu bila kuzingatia muktadha wa matini ilikoandikwa, muktadha wa matini tafsiri itakapotumiwa zaidi. Bila kuzingatia matakwa hayo ujumbe unaweza kupotoka na mawasiano yakakwama.

Kwa mujibu wa Newmark na wenzake (1981) tafsiri mwafaka huwa tukio linalojumuisha vipengele vya tafsiri maana na vile vya tafsiri mawasiliano. Wanaongezea ya kuwa vipengele vya maana au semantiki katika tafsiri huhusiana na kueleweka kwa ujumbe katika muktadha wa matini pokezi na kwa upande mwingine ujumbe huo kuwa na athari kimawasiliano kwa hadhira. Pia, Newmark anaunga mkono dai kuwa mfasiri hana budi ya kuendeleza milele na milele uaminifu wake kwa mambo haya matatu yafuatayo : (i) mwandishi wa matini asilia, (ii) kaida za lugha pokezi na, (iii) mpokeaji ujumbe wa tafsiri (hadhira).

Hapo ni wazi kwamba wataalamu hao hawaegemei upande wowote yaani upande wa tafsiri maana au wa tafsiri mawasiliano. Mfasiri katika harakati zake za kutafsiri ananufaika akiwa anatumia mbinu mbalimbali kuliko kutumia mbinu moja.

Larson na wenzake (1984) wanachukua mwegemeo wa kiisimu na kuona kuwa tafsiri huhusu uhamishaji wa maana ya vipengele vya lugha asili hadi lugha pokezi. Katika mchakato huo,

maana ndiyo yenye kuhamishwa, nayo haipaswi kubadilishwa kamwe. Maoni yao yanadhihirisha umuhimu wa kipengele cha maana katika tafsiri, sawa na ambavyo nadharia ya maana hufanya.

Kwa mujibu wa Newmark (2003) kufasiri ni kuweka maana ya matini moja katika lugha nyingine kwa namna ambayo mwandishi amekusudia matini hiyo iwe. Inadhihirika kuwa yeye anasisitiza kuhawilisha maana iliyomo katika LC kwenda LL badala ya kuegamia kwenye upande wa kuhawilisha maneno. Maana hiyo inazingatia pia utamaduni wa lugha husika.

Naye Mwansoko (2006) anafasili neno tafsiri kama zoezi la kuhawilisha ujumbe kutoka matini chanzi kwenda matini lengwa. Kauli yake inaafikiana na kauli za Newmark (1981/2003). Tafsiri bora ni ile inayozingatia maana ya matini chanzi badala ya kuzingatia uhawishaji wa maneno. Kumanisha kuwa uhawilishaji wa maneno kutoka LC kwenda LL kuwiane na uhawilishajiwa maana iliyokusudiwa.

Mwansoko (2013) hapingi msimamo wake wa hapo mwaka 2006 anapothibitisha kuwa tafisiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine, falisi ya dhana tafsiri aliyotolea kule awali. Mtazamo wake unalenga kuonya wafasiri kuzingatia kila mara maana ya matini chanzi ili idhihirike katika matini lengwa.

Kwa mujibu wa Jilala (2023) tafsiri hufanywa kwa kuhamisha ujumbe uliopo katika maandishi na ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo au ujumbe unaotafsiriwa na kuwa na visawe vinavyokaribiana katika lugha lengwa. Hapo kunaweleka kuwa si kazi rahisi kupata visawe kamili unapofanya kazi ya tafsiri. Mfasiri anatumia visawe ambavyo ana matumaini kuwa vinaweza kukaribiana kwa maana na vile vilivyotumiwa katika lugha chanzi.

Kwa ufupi, wataalamu hawa wanatilia mkazo uzalishaji mpya wa ujumbe kwa kutumia visawe asili vinavyokaribiana na matini chanzi kimaana na kimtindo. Pia, suala la tafsiri lazima lichangamane na uwepo wa lugha mbili yaani chanzi na lengwa. Kuwepo mchakato wa

ubadilishaji wa lugha ya awali na kuweka katika lugha mpya bila kupoteza maana na tena kuwe na suala la kutokubadilika kwa mtindo na muundo wa kazi ya lugha chanzi.

### 2.2.2. Dhana ya Mbinu za Tafsiri

Kwa mujibu wa TATAKI (2010) mbinu ni njia ya kuetekeleza jambo. Njia zinazotumika katika kutafsiri ni mbinu mbalimbali ambazo zinazoweza kuwaongoza wafasiri wa ML kutoka katika MC.

Kwa mujibu wa Mwansoko na wenzake (2015) kuna aina kuu nne za mbinu za tafsiri ambazo ni tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Tafsiri ya neno kwa neno ni ile ambayo kila neno pamoja na mofimu zake hufasiriwa kwa maana ya kikamusi kwa kufuatishwa chini ya matini chanzi (MC) yake. Tafsiri sisisi ni ile ambayo maneno, yakiwemo yale ya kitamaduni, hutafsiriwa kwa kuzingatia maana zake za msingi, ila kwa kuzingatia sarufi ya LL. Tafsiri ya kisemantiki ni ile inayozingatia vipashio vyote vya MC na kuvifasiri kwa vipashio vyake katika LL. Tafsiri ya kimawasiliano ni ile inayozingatia maana, mtindo, muundo, mazingira na utamaduni wa LL katika kuhawilisha taarifa za MC kwenda katika matini lengwa (ML). Wanazuoni hao wanaposema aina kuu za tafsiri wanamaanisha kuwa kuna aina zingine ndongondogo. Pia, ni nadra kupata aina moja ikitumika upwekee; aina hizo zinatumika kwa kushirikiana.

Akishadidia hoja kwamba kuna tofauti baina ya mikakati ya tafsiri na mbinu za tafsiri, Molina na Albir (2002) waanasema kuwa mbinu ya tafsiri inahusu namna mchakato wa tafsiri unavyoendeshwa kulingana na lengo la mfasiri yaani kitendo cha jumla kinachoathiri matini nzima. Kupitia maelezo haya, inaelezeka kuwa mbinu za tafsiri hutumiwa katika kushughulikia matini yote. Kwa mantiki hiyo, mfasiri anaweza kuamua kuchukua mwelekeo wa kimawasiliano badala ya tafsiri sisisi katika kutafsiri matini fulani, Ngesu (2019). Kuhusu mikakati, Molina na Albir (2002) wanaeleza kwamba mikakati ni taratibu (kwa kujua au

kutojua, ya kusemwa au ya ishara) inayotumiwa na mfasiri kutatua matatizo yanayotokea anaposhughulika na mchakato wa tafsiri akiwa na lengo mahususi. Mikakati huitumiwa kutafsiri vipashio vidogo ndani ya matini inayofanyiwa tafsiri. Kwa mujibu wa Pjuastuti (2014) mikakati ya tafsiri ni njia au taratibu anazotumia mfasiri katika kutafsiri maneno, vishazi na sentensi kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Vinay na Derbelnet (2004) wanaeleza kwamba msingi wa uteuzi wa mikakati ya tafsiri ambayo mfasiri anaweza kuteua ni mikakati miwili yaani tafsiri ya moja kwa moja na tafsiri isiyo wazi. Kuhusu tafsiri ya moja kwa moja ni uteuzi wa kategoria za kisarufi au visawe vya dhana vinavyolingana baina ya lugha chanzi na lugha lengwa. Ilhali ,tafsiri isiyo waziinahusu uteuzi wa mikakati inayoweza kukabiliana na changamoto za tafsiri ya vipengele visivyokuwa na visawe vya moja kwa moja. Vinay na Darbelnet (2004) wanatoa mifano ya tafsiri ya moja kwa moja kama vile: ukopaji, tafsiri ya dhana na tafsiri sisisi. Kuhusu mikakati ya jumla/isiyo ya wazi, wanatoa mifano minne: uhamishaji, usawe, ubadilishaji na urekebishaji.

Kuna mijadala mbalimbali kuhusu mitazamo tofauti ya matumizi ya mikakati ya tafsiri. Wanazuoni Newmark (2003), Malangwa (2014) na Munday (2016) wanakubaliana kwamba kuna tofauti baina ya mbinu na mikakati. Vilevile, kuna wanazuoni wanaotumia istilahi ‘mikakati’, ‘mbinu’ na ‘taratibu’ kwa maana ya mbinu/mikakati (Lorschester, 1991; Chesterman, 1997; Jilala, 2014). Kwa mujibu wa Newmark (2003) mbinu za tafsiri huteuliwa kulingana na aina ya matini, walengwa na lengo la tafsiri. Hii ina maana kwamba matini inaweza kuchukua mwelekeo wa tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki au tafsiri ya kimawasiliano. Kutokana na mitazamo hiyo ya mwanaisimu tuliozungumzia na tutatumia mbinu za tafsiri badala ya mikakati.

### 2.2.3. Dhana ya Kamusi

Lugha hukua, hubadilika na maneno mengi huibuka kuwasilisha dhana mpya kila uchao. Hali hii husababisha hitaji la kukusanya, kufasili na kuusanidi msamiati huo ili kuutunza.
Kwa mujibu wa Mdee (1996) kamusi ni "Kitabu cha orodha ya maneno pamoja na maana zake". Karibu ya miaka thelathini iliyopita, mtalamu huyo alifasili kamusi kama kitabu cha marejeo chenye msamiati uliokusanywa kutoka kwa wazungumzaji fulani, na kupangwa kwa utaratibu maalum, kisha kufafanuliwa kwa namna ambayo msomaji anaweza kuelewa Mdee (1977). Maoni ya Mdee yanaanisha kwamba maneno baada ya kuorodheshwa yapewe maana ili mtumiaji wa kamusi apate uelewa na mwanga wa kutosha wa msamiati uliokuwa na utata kuelewa.
Kamusi ni mojawapo ya vyombo muhimu vitumikavyo kuhifadhi, kusambaza na kuimarisha lugha ya Kiswahili, Adika ( 2020). Fisili hii inamaanisha kuwa lugha hutajirika kupitia kamusi. Watu wanotumia kamusi wanapata maarifa mbalimbali hata ya mambo yalitokea zamani ni hivi karibuni na kusambazwa mwa watu kupitia kamusi.

Aina za kamusi zinaainishwa kwa kuzingatia kigezo cha lugha zinazotumiwa na muundo wake. Kwa mujibu wa Mdee (1997) aina za kamusi hutegemea idadi ya lugha ambazo zimetumiwa katika kamusi moja, walengwa wa kamusi, na mambo yanayoshughulikiwa katika kamusi. Kwa kuzingatia kigezo cha lugha, Mdee (1997) anabainisha aina tatu za kamusi ni muktadha wa matumizi zake. Kwanza, kamusi wahidia yaani iliyoandikwa kwa kutumia lugha moja tu na inalengwa kwa wazungumzaji wazawa wa lugha hiyo. Pili, kamusi thaniya, yaani kamusi iliyoandikwa kwa lugha mbili. Katika kamusi ya aina hii vidahizo huandikwa kwa lugha moja (LC) na maelezo ya maana ambayo kwa kawaida huwa neno moja yaani visawe, huandikwa kwa lugha nyingine (LL). Tatu, Kamusi mahuluti, yaani kamusi iliyoandikwa kwa lugha nyingi, vidahizo vya kamusi mahuluti hupatiwa visawe kutoka katika lugha mbalimbali. Kamusi thaniya na Kamusi mahuluti hutumiwa katika mchakato wa tafsiri na pia hujulikana

kama kamusi ya wingilugha. Maoni yake yanamaanisha kuwa ili kamusi itungwe kunateuliwa walengwa na kiwango cha ujuzi wanao, idadi ya ludha wanapendekeza kutumia.kwa hiyo kuna kamusi za lugha ya kawaida na za lugha ya kiufundi zilizoandikwa katika kwa lugha moja au nyingi.

Miongoni mwa sifa za kamusi kuna muundo wake. Kwa mujibu wa Benjoint (1996) kamusi imegawanyika katika sehemu kuu tatu:sehemu ya mwanzo, ya kati na mwisho. Kwanza, mwanzo wa kamusi pia huitwa utangulizi: unaonyesha malengo ya mwandishi, maana na aina ya kamusi na alichokusudia mwandishi wasomaji wake katika kamusi husika.Vile vile, tunaweza kupata mwongozo wa mtumiaji. Pili, matini kamusi ambacho ndicho kiini cha kamusi ambacho kina sehemu mbili ambazo ni vidahizo na vitomeo. Tatu, mwisho wa kamusi pia huitwa sherehe ya kamusi: ni taarifa mabazo huandikwa mwishoni mwa kamusi baada ya vidahizeo na fahiwa zake.
Hii ina maana kwamba, mtumiaji wa kamusi yoyote ingekuwa bora kuichunguza kabla ya kuitumia.Utangulizi unaongoza namna ya kuitumia na hadhira, kupata vitomeo na vidahizo atakavyopata na maarifa kama nyongeza yaliyowekwa mwishoni mwa kamusi.

**2.2.4. Dhana ya Kamusi ya Istilahi**

Kevogo na wenzake (2020) wakizungumzia dhana ya kamusi ya kiistilahi wanasema kuwa ni kamusi maalumu inayowasilisha, kwa lugha moja au zaidi, istilahi halisi za kisayansi, mbinu au sanaa na ufafanuzi. Kamusi ya kiistilahi imebanwa kwa msamiati inaoufasili. Ni wazi kuwa kamusi ya istilahi huenda ikawa aina ya kamusi thaniya mara nyingi. Pia, hizo ni kamusi zenye msamiati wa eneo mahsusi kama vile michezo, falsafa, sheria, tiba, uchumi, n.k. Kamusi za istilahi zina vidahizo vyake na maumbo ya istilahi.

**2.3. Kamusi ya Tiba (2003)**

Baada ya kuzungumzia maana ya kamusi, aina na muundo, ni bora zaidi kuzungmzia sifa za kamusi ya Tiba ambao iliteuliwa kufanyiwa tathmini ya mbinu za uundaji wa istilahi za uwanja wa magonjwa kupitia LL .

Kamusi ya Tiba ilitungwa wa mabingwa wawili ,Prof. H.J.M. Mwansoko (Dip. Journalism, Dip. Translation, M.A., Ph. D.) na Dkt. A. M. A. Mwita (M.D, M. Sc.) matunda ya juhudi za pamoja za wanaistilahi wawili na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Mwaka 1998, Dkt. Mwita aliwasiliana na kuwasilisha mswada kwa Profesa Mwansoko wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Profesa Mwansoko alibaini kuwa mswada unafaa kuendelezwa zaidi hususan katika uundwaji wa istilahi sadifu zaidi. Aidha ni yeye aliyeandaa misingi na kanuni za uundaji wa istilahi za Kiswahili zilizotumiwa katika kamusi hii. Pia ndiye aliyeshughulikia lugha kienzo ya kamusi. Kazi hiyo nayo ilifanyika kwa vipindi kutokana na majukumu mengi ya kikazi ya waandishi wote wawili. Vyanzo vingine ni mikutano na warsha mbalimbali ambazo Wizara ya Afya huwashirikisha watalaam kutoka BAKITA na TUKI. Aidha, maongezi ya kawaida na watu mbalimbali yamewasaidia waandishi kurutubisha istilahi zilizomo. Hatimaye mswada uliwasilishwa TUKI mwezi Juni, 2003 kwa uchapishaji, KT( 2003).

Kamusi ya Tiba ni kamusi ya taaluma kwa kuwa imeandikwa na wasomi waliobobea taaluma mbali mbali ili zitumike katika ulingo fulani wa kitaaluma.Iliandikwa kwa ajili ya kukidhi matakwa ya kitaaluma ambapo istilahi mbalimbali huwa imeorodheshwa na kupewa ufafanuzi wake au maana zake kulingana na ulingo wa taaluma husika.

Katika kamusi hii maneno ( istilahi) yalipangwa kwa alfabeti A hadi Z. Maneno yote yanayoanza na herufi fulani yote yaliwekwa chini ya herufi hiyo.

Hata kama maneno ( istilahi) zaidi ya moja yote yanayoanza na herufi moja nayo yalipangwa kwa utaratibu wa kialfabeti kwa kuzingatia heru inayoanza na inayofuata.Kategoria ya

kisarufi ya maneno( istilahi) iliwasilishwa kabla ya istilahi upande wa kiingereza vile vile na wa kiswahili.kwa mfano adj –kivumishi,adv – kielezi, n- Nomino, K- Kitenzi. Kamusi hii ina kichwa; Kamusi ya Tiba, ina dibaji,utangulizi, muundo ila haina nyongeza.

Kutokana na sifa zake, *KT* inaorodheshwa katika kamusi thaniya au kamusi za uwili lugha. Ikubushwe kuwa watunzi wa *KT* walianza kukusanya istilahi za LC yaani Kiingereza na kuziweka katika LL yaani Kiingeza kwa kutumia mbinu mbalimbali za uundaji wa istilahi za kamusi ya kiistilahi. Tutapata muda mwafaka ya kuzichambua mbinu hizu katika sura ya nne unaojikita kuwasilisha da kuchanganua data za utafiti huu.

Baada ya kuchunguza dhana muhimu zinazojitokeza katika mada yetu ya utafiti, sasa tunafikiri kuwa tumefikia hatua nzuri ya kuchunguza kazi tangulizi ambazo zimeshafanyika, zinazoshabihiana na utafiti huu kwa lengo la kubainisha pengo la utafiti.

## 2.4. Mapitio ya kazi Tangulizi.

Kuna tafiti mbalimabali ambazo zimefanywa kuhusu mikakati na mbinu ambazo zimekuwa zikitumika katika utungaji wa kamusi za kiistilahi za Kiswahili katika nyanja mbalimbali na kwa kutumia mikabala na nadharia tofauti tofauti.

Mdee (1980) alishughulikia mbinu za uundaji wa istilahi kama vile ukopaji wa istilahi za kigeni na uswahilishaji wake, ukopaji kutoka lugha za Kiafrika, akronimu na unyambuaji. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kwamba watumiaji wa Kiswahili walionelea mbinu ya uendelezaji wa Kiswahili mumo kwa mumo, yaani uundaji unaotokana na lugha enyeji kuwa bora zaidi.Matokeo ya utafiti yake yanatoa mchango kwa kutoa mwanga kwa utafiti huu kwani ulitafiti mbinu za uundaji istilahi kwa jumla. Tofauti iliopo kati ya utafiti wake na utafiti huu ni uwanje ulioteuliwa kutafitiwa. Wakati yeye hakuteuwa uwanja maalumum utafiti huu unajikita katika uwanja wa wa tiba moja mwa njanya wiliowasilishwa katika *KT*.

Mwansoko (1990) alishughulikia mifanyiko inayotuniiwa katika uundaji wa istilahi. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha matumizi ya mbinu kuu mbili zifuatazo : ( 1) Lugha yenyewe kwa minyambuliko, miambatano, miungano, kuongeza maana, au kuyapa maneno; maana maalum, na vifupisho. (2) Mikopo kutoka lahaja na lugha nyingine, pamoja na tafsiri sisisi. Isitoshe, alichukua fursa hiyo kujadili misingi ya uteuzi wa lugha changizi auchasili ya istilahi. Mtaalamu huyu anapendekeza matumizi ya Kiingereza kama lugha chasili ya istilahi za Kiswahili na alitoa sababu zifuatazo: Kwanza kabisa, wengi wa watumiaji lengwa wa istilahi za Kiswahili walipata na/au wanaendelea kupata elimu-yao kwa Kiingereza. Hivyo wanazipendelea istilahi zenye asili ya Kiingereza kwa sababu si ngeni kwao. Vitabu vingi zaidi vinavyotuinika shuleni, vyuoni na Chuo Kikuu vimeandikwa kwa Kiingereza, ikiwa ni pamooja na kuwepo kamusi ya Kiingereza-Kiswahili ya kurejelewa. Tasnifu za waatalamu hawa zina mwingiliano mkubwa na kazi yetu hii. Hivyo ilitubidi kutalii mbinu walizozituniia kwenye utafiti wao, na uchanganuzi wa data itakayopatikana.

Mwangi (1996) alichapisha tasnifu ‘‘Matatizo ya Leksikografia tafsiri: Tathmini ya Kamusi ya F. Johnson (1939) ’’ iliyojengwa katika msingi unaoafiki kuwa kamusi za lugha mbili ni kazi halisi za tafsiri. Lengo lake lilikuwa kuonyesha kuwa hata kamusi za lugha mbili zina matatizo mengi ya tafsiri katika ngazi mbalimbali za lugha. Utafiti wake uliegemea sana upande wa leksikografia-tafsiri na kuonyesha nafasi ya maana katika tafsiri ya moja kwa moja, tafsiri-huru na tafsiri mawasiliano. Utafiti huu umeonyesha nafasi ya maana katika tafsiri ya moja kwa moja, tafsiri-huru na tafsirimawasiliano. Utafiti wetu unalenga kutathmini mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa kuundia istilahi za LL ya KT tofauti naye aliyechunguza matatizo mengi ya tafsiri katika ngazi mbalimbali za lugha. Lakini, hii ina maana kuwa utafiti wetu ulilenga kuchunguza kamusi ya kifundi tofauti na utafiti wa Mwangi ambao ulijiegemeza katika kamusi ya kawaida.

Mwaro -Were (2020) aliwasilisha utafiti wa tafsnifu wa uzamivu wenye mada ‘‘Usayansi wa Istilahi za Isimu ya Kiswahili’’. Lengo la utafiti wake lilikuwa la kutathmini usayansi katika istilahi na mbinu za kuundia istilahi za isimu ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kwamba mbinu inayozalisha istilahi za isimu zenye 'usayansi' ni ile ya uasilishaji wa istilahi kutoka Kiswahili chenyewe, ikifuatwa na uunganishaji na uambatanishaji, unyambuaji na ubunaji. Mbinu za upanuzi wa maana za maneno, ukopaji/utohoaji, uradidi, uhulutishaji na ufupishaji yaani akronimu na ukatizaji. Pia, ilikuwa jaribio la kuchunguza 'usayansi' wa istilahi za isimu ya Kiswahili na mbinu zinazotumiwa kwa minajili ya kuibua sababu za kusadifu ama kutosadifu kwa istilahi kwa walengwa wa lugha hii ya Kiswahili wa Afrika Mashariki. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kuwa sababu ya kuendeleza istilahi za isimu ya Kiswahili imetokana na lugha hii kutaka kujieleza yenyewe katika uwanja wa isimu. Kazi yake japo haijikiti katika kutathmini mbinu za tafsiri katika uundaji istilahi za kamusi una uhusiano na kazi hii. Sote tunashughulikia uundaji wa istilahi. Kwa hiyo, bila shaka pamoja na kutoa mwanga, itasaidia kutoa ufafanuzi wa data yetu.

Mosota (2016) katika utafiti wake kupitia tasnifu ya uzamili wenye mada,Utohozi wa Msamiati kutoka Kiswahili hadi Ekegusii».Lengo la utafiti huu lilikuwa la kuweka wazi usayansi uliopo katika istilahi zilizotoholewa kutoka Kiswahili hadi Ekegusii. Katika mchakatako wa kuendeleza utafiti huu umetumia nadharia ya ukopaji uhamisho na N.I.K. katika ufafanuzi wa kazi hii. Nadharia ya ukopaji uhamisho iliyoasisiwa na Odlin (1989) ilimpa mwelekeo. Vilevile uasilia wa istilahi tohozi umechunguzwa iwapo maneno tohozi yote yalikuwa na majina asilia. Taratibu za utohozi zimechunguzwa na matokeo yalionyesha kuwa utohozi huongozwa na kudhibitiwa na sheria na kanuni za fonolojia ya Ekegusii. Matokeo ya utafiti huu yana umuhimu kwa utafiti wetu. Mtafiti huyu yeye amejikita katika kuchunguza taratibu za utohozi kwa madhumuni y aya kuunda istilahi kutoka kiswahili kwenda Ekegusi.

Sisi tunalenga kutathmini mbinu za tafsiri katika uundaji istilahi za Kamusi ya Tiba . Sisi tunajikita katika Kiingereza na Kiswahili wakati yeye ni Kiswahili Ekegusi.

Adolph (2019) alichapisha tasnifu ya uzami yenye mada‘‘Utohozi wa istilahu za kiingereza katika Kiswahili: uchunguzi kifani wa taaluma za tiba na compyuta’’. Utafiti huo umechunguza utohozi wa istilahi za fani ya tiba na kompyuta za kiingereza katika lugha ya Kiswahili kwa kuangazia michakato na athari zake. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni nadharia ya Fonolojia Zalishi (NFZ) iliyoasisiwa na Naomi Chomsky na Moris Halle (1968) pamoja na nadharia ya mofolojia Leksika (NML).Ambayo mwasisi wake ni Kiparsky (1982). Aidha, data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia mbinu za hojaji na uchambuzi wa matini. Data iliyokusanywa ilichambuliwa kwa kutumia mkataba wa maelezo na wa kitakwimu. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa lugha ya Kiswahili imetoa istilahi za fani ya tiba na kompyuta kutoka katika kiingereza. Pia, utafiti umebaini kuwa wakati wa utohozi wa istilahi katika Kiswahili, michakato mbalimbali ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia hufanyika. Michakato hufanyika kadiri kanuni na taratibu za lugha ya Kiswahili ili istilahi ziweze kukubalika. Michakato ya kifonolojia iliyobainishwa katika utafiti huu ni pamoja na mchakato wa udondoshaji, uchopekaji, usahilishaji wa irabu uangalifu kuwa irabu sahili na mchakato wa ufupishaji wa irabu ndefu. Utafiti huu umebaini kuwa utohozi wa istilahi za fani ya tiba na kompyuta za kiingereza za kiingereza katika Kiswahili una athari chanya na hasi katika lugha ya Kiswahili. Athari chanya zilizobainika ni pamoja na zile za kifonolojia, kisemantiki na kileksia. Hivyo mtafiti anapendekeza kuwa pawepo na uhamasishaji wa matumizi ya istilah za Kiswahili zilizopo ili kuepuka mfumko wa istilahi nyingi zinazorejelea dhana moja.Utafiti wake una malengo tofauti na malengo yetu. Pia, sampuli lengwa ni tofauti na yetu. Yeye ana lengo la kuchunguza utohozi katika taaluma ya tiba na kompyuta kwa ujumla .Taaluma hizo ni pana, zina vijisekta mbalimabali .Aidha, utafiti wetu unalenga kuchunguza mbinu za tafsiri

katika uundaji wa istilahi za uga maalumu ; uga wa Tiba wala si kuchunguza mbinu ya utohozi pekee yake.

Pia, Adolph (2021) alichapisha makala ‘‘Mabadiliko ya Kifonolojia ya Istilahi za Kiingereza katika Kiswahili: Uchunguzi Kifani kutoka Covid 19’’. Nadharia ya NFZ (Nadharia ya Fonolojia Zalishi) iliyoasisiwa na Noam Chomsky na mwenzake (1968) ndiyo iliyoongoza utafaiti wake Katika kuchunguza mabadiliko ya kifonolojia ya utohozi wa istilahi hizo.Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa mabadiliko mengi ya kifonolojia yanahusiana na utohozi wa istilahi za COVID 19 kutoka lugha ya Kiingereza kuja Kiswahili. Isitoshe, aliwasilisha sababu mbali mbali za utohozi wa istilahi za LC katika LP. Miongoni mwa sababu hizo ni maendeleo ya sayansi na teknolojia, shughuli za kiuchumi, ukoloni, muwasala kati ya wazungumzaji wa lugha moja na nyingine pamoja na mlipuko wa magonjwa. Utafiti wake ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu moja ya malengo mahususi ya utafiti huu ni kutoa sababu ya matumizi ya mbinu za tafsiri katika uundaji wa istilahi za LL ya *KT*. Kwa hiyo ,matokeo yanatupa mwanga zaidi.

Adolph na wenzake (2024) walichunguza mkakati wa tafsiri mkopo wa istilahi za Kiingereza katika Kiswahili na athari zake kwa kuangazia uga wa biolojia, fizikia na kemia kupitia vidahizo teule vya Kamusi ya Biolojia, Fizikia na kemia TUKI (2012). Azma kuu ya uchunguzi huu ni kutathmini mchango wa tafsiri mkopo wa msamiati wa Kiingereza katika suala zima la kukuza lugha ya Kiswahili. Malengo ya makala hii yametimizwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Istilahi za Kisayansi iliyoasisiwa na Kiingi (1998) na kuendelezwa na Kiingi na Mwaro-Were (2000, 2001) . Matokeo yameonyesha kuwa Kiswahili kimejipatia istilahi lukuki katika tasnia ya biolojia, fizikia pamoja na kemia kupitia mkakati wa tafsiri mkopo. Utafii wao una malengo yanayotofautiana na malengo ya utafiti wetu hata kama sote tunashughulikia data kutoka kamusi za kifundi.Wao wana lengo la kuchunguza mkakati wa tafsiri mkopo na athari zake wakati utafiti huu unapoo madhumuni ya kuchunguza mbinu za uundaji istilahi bila

kuchagua tunayopendelea zilizotumiwa kuunda istilahi za uwanja wa magonjwa katika LL ya K T.

Isitoshe, Adika (2021) katika makala ''Ukopaji kama Mkakati wa Kuendeleza Istilahi za TEHAMA katika Kiswahili: Uchunguzi wa Vidahizo Teule vya Kamusi Sanifu ya Kompyuta, Kiputiputi (2011)'' aliendelea na utafiti kuhusu istilahi. Malengo ya utafiti huu ni kuchambua aina za ukopaji na jinsi unavyojitokeza, kuchanganua vipengele vya kimuundo vya istilahi mkopo na kueleza upungufu unaodhihirika katika taratibu za kuundia istilahi mkopo. Uchanganuzi wa istilahi hizo ulitekelezwa kwa mujibu wa vigezo vya istilahi faafu vya PEGITOSCA katika Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) iliyowasilishwa na Kiingi (1998). Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba kati ya aina tatu za ukopaji: utohozi, uasilishaji na tafsiri mkopo, ni tafsiri mkopo ndiyo iliyochangia idadi kubwa zaidi ya mikopo. Utafiti wake kwa mara nyingine unatofautiana na utafiti wetu kwa kwa malengo na japo unawiana na nadharia moja ,miongoni mwa mbili tunazotumika katika utafiti huu.Nadharia ya UMA hakuitimika bila ya kusahau data, na malengo ya utafiti. Ila, matokeo yao yalitusaidia kufanya majumuisho ya mbinu za uundaji wa istilahi za LL ya KT kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

Jilala (2021) alifanya utafiti kupitia makala yenye mada ''Mbinu na Nafasi ya Tafsiri katika Uundaji wa Istilahi za Sayansi na Teknolojia: Mifano Kutoka Progaram za Klinux na Microsoft''. Lengo la utafiti lilikuwa tathmini ya mbinu na nafasi ya tafsiri katika uundaji wa istilahi za sayansi na teknolojia.Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ulinganifu wa aina ya matini iliyoasisiwa na Reiss (1971/2000) ambayo ilitumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Matokeo ya utafiti yahitimisha kuwa uundaji wa istilahi za sayansi na teknolojia unategemea nadharia na mbinu za tafsiri ili kupata maana na matumizi ya istilahi za LC katika LL. Mbinu zilizoonekana zinajitokea zaidi ni mbinu ya tafsiri sisisi, uhawilishaji, utohozi na uasilishaji. Utafiti huu ulibainisha kuwa tafsiri ina nafasi kubwa katika uundaji wa istilahi za

sayansi na teknolojia. Utafiti wake unatofautiana na utafiti wetu kwa kuchunguza mbinu na nafasi za uundaji wa istilahi za Programu za kompyuta wakati utafiti wetu unapochunguza mbinu za uundaji wa istilahi za LL ya *KT*. Kutokana na mbinu za tafsiri alizogundua, utafiti huu una thamani kubwa kwetu kwani utasaidia kutoa mwanga ili kufikia malengo ya utafiti wetu.

Kwa ufupi, maandiko hayo yalijadili mbinu ambazo zimekuwa zikitumika katika utungaji wa kamusi za kiistilahi za Kiswahili, matatizo ya leksikografia tafsiri na usayansi wa istilahi zilizokwisha wasilishwa.Wanazuo hao walitathmini mbinu moja moja kama vile utohozi na namna ya kufanya utohozi. Pia, walitathmini nafasi ya tafsiri katika uundaji wa istilahi.

Kwa ujumla, japo tafiti zilizotangulia utafiti huu zinatoa mwanga kwa utafiti huu kwa namna mbalimbali utafiti wetu unadokeza upwekee wake. Kwanza, imedhihirika kuwa watafiti waliegemea ama lengo ya kutathmini mbinu ya utohozi au ya tafsiri mkopo na athari zake. Ama kumeshughulikiwa nafasi ya tafsiri katika uundaji wa istilahi lakini hatuna aliyepiga hatua yangu ya kufanya uchunguzi wa kina wa kutathmini mbinu za uundaji istilahali kwa ujumla zilizotumiwa kuunda istilahi za kamusi za fani hasa LL ya *KT* wakizingatia uwanja kama vile wa magonjwa kutoa na sababu za matumizi ya mbinu hizo. Utafiti wetu ukiwa na lengo hilo kama tulivyosema hapo awali manufaa yatakuwa makubwa kwa mfasiri wa kesho, kwa wa watafiti na kwa watoa huduma ya tiba.

**2.5. Pengo la Utafiti**

Maandishi yaliyojadiliwa hapo juu yamedhihirisha shughuli za watafiti mbalimbali kuhusu matatizo ya tafsiri na athari zake katika leksikografia. Pia, nafsi na mbinu za uundaji wa istlihahi za kamusi ya kompyuta bila ya kusahau kujadiliwa kwa mara nyingi athari ya tafsiri tohozi na mkopo kama mbinu ya kuunda istilahi za kiswahili kutoka kiingereza. Kwa mujibu wa maandiko hayo, uundaji wa istilahi za kiswahili huegemea sana mbinu za tafsiri na mbinu ya

utohozi pamoja na mbinu ya mkopo inatoa mchango mkubwa katika mustakabali wa uundaji wa istilahi za Kiswahili.

Aidha miongoni mwa tafiti mbalimbali zilizojaribu kuchunguza mbinu za uundaji wa istilahi kwa kutumia data kutoka kamusi walichunguza tafsiri mkopo wakati kuna mbinu nyingi za uundaji istilahi kwa ujumla na uundaji istilahi za kamusi ambazo huenda zinaweza kupatikana katika LL ya KT.

Hivyo, utafiti huu umeonekana muhimu katika ukuzaji wa mustakabali za uundaji wa istilahi za taaluma mbalimbali ili kuziba pengo la mfumko wa istilahi. Utafiti huu utajikika katika kutathmini mbinu za uundaji istilahi zote zilizotumiwa katika mchakato wa uundaji wa istilahi za uwanja wa magonjwa kupitia LL ya *KT* yaani kiswahili kutoka LC yaani kiingereza ambazo zinapatikana katika *KT*, kutoa maelezo ya sababu ya matumizi ya mbinu zilizogunduliwa.

## 2.6. Mkabala wa Kinadharia

Kwa mujibu wa Massamba (2004) nadharia ni kanuni na misingi ambayo hujengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kiolezo cha kueleza jambo.

Tavallaei na Abu-Talib (2010) ambao wanaielezea dhana ya nadharia kwa namna tatu. Mosi, nadharia huweza kumaanisha seti ya kanuni na maelezo kuhusu jambo fulani. Pili, huweza kuchukuliwa kama lensi au dira ya kuendeshea tafiti, tahakiki, na/au mijadala. Tatu, ni nyenzo ya kufikia mahitimisho ya kimjadala kuhusu dhana mbalimbali za sayansi za jamii. Kwa mujibu wa Chesterman (2004) nadharia inaeleweka kuwa ni mkusanyiko au mfungamano wowote wa dhana, mawazo, kauli, taratibu na kanuni mbalimbali zilizopangwa kwa utaratibu mahususi ili zitumike kama kiolezo cha kuelezea jambo fulani, kuongezea welewa wa mtu kuhusu jambo hilo au kama mwongozo mzuri wa mtafiti wa kudadisia na kutatulia matatizo yake ya kiutafiti.

Kila fani ina dira inayoiongoza katika uchunguzi, uchambuzi na ufafanuzi, Jilala (2024) . Kwa hiyo, na utafiti huu lazima uwe na nadharia inayouongoza pamoja na mikabala yake. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili yaani ya Uchanganuzi wa Maudhui (UMA, kuanzia sasa) iliyoasisiwa na Krippendorff (2004) na nadharia ya Istilahi za Kisayansi (kuanzia sasa NIK) iliyoasisiwa na Kiingi (1989) na kuendelezwa na Were-Mwaro, (2000). Kulingana na White ( 2006) ambaye ni mmoja wa wataalamu wa UMA, mkabala huu hutumika kama mwongozo na metodolojia ya utafiti wa data za kitaamuli.

### 2.6.1. Mihimili ya UMA

Kwa mujibu wa Krippendorff (2004) UMA hujumuisha usomaji makini na wa kina wa maandishi, picha au jambo lolote la kiishara ambapo maudhui huibuliwa na mtafiti kwenye mchakato wa kuchambua matini inayohusu muktadha maalumu.

Kwanza, nadharia hii huchukuliwa kama mwongozo kwa sababu humwongoza mtafiti kulitazama jambo analotafiti na kufikia hitimisho kwa kuongozwa na sifa zake.

Ujumbe unaotokana na matini husika kama data ya utafiti, huibuliwa na mchambuzi kwa kuifahamu matini yake, kubuni uchanganuzi, kupanga misimbo ya kufafanua vipengele vya matini hiyo, hatimaye kufasiri matokeo kulingana na uelewa wake kwa kuzingatia muktadha wa matini chunguzwa.

GAO-PEMD (1996) wanasisitiza kwamba mkabala huu ni mbinu ya utafiti inayotumika kwa utaratibu maalumu, kuchanganua taarifa ya matini kwa njia sanifu ambayo humruhusumchambuzi kutoa hitimisho juu ya taarifa hiyo. Mchanganuzi hubainisha dhima/mawazo, masuala au mada ambazo anazihitaji kwa ajili ya utafiti wake.

### 2.6.2. Hatua za Nadharia ya Uchanganuzi wa Maudhui

Kama ilivyopendekezwa na Krippendorff (2004) na kusisitizwa na White na Marsh (2006) hatua za uchanganuzi wa maudhui huwa ni tano. Hatua ya kwanza ni kupata mkusanyiko wa matini yaani data ya uchanganuzi. Hatua ya pili ni kubainisha tatizo la utafiti linaloongoza uchambuzi wa matini na data inayopatikana kutoka kwenye matini inayochambuliwa. Hatua ya tatu ni uteuzi wa sampuli yaani usampulishaji. Hatua ya nne ni usimbaji au kutafsiri data ya matini kulingana na tafsiri inayojibu maswali yanayoongoza utafiti. Hatua ya tano ambayo pia ni ya mwisho, ni kutoa mahitimisho ambayo yanakusudia kujibu swali la utafiti.

Kutokana na hatua hizi, ni dhahiri kuwa nadharia ya UMA inaweza kutoa picha ya istilahi za *KT* kwa kuzibainisha kupitia data, kusaidia kutathmini mbinu za uundaji wa istilahi za LL ya *KT* na kueleza sababu ya matumizi ya mbinu husika. Isitoshe, naharia ya UMA inazewa kusaidia walimu na watafiti kuchunguza mbinu za uundaji wa istilahi na kuhakikisha kuwa mbinu wanazotumia zinawainuia wanafunzi na wateja wao wanapopata huduma kutoka kwao.

## 2.7. Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK)

Nadharia ya Istilahi za Kisayansi imetumika ili kutupatia data na kuchambua data za utafiti huu. Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) ilitumika ili kufidia mapungufu ya nadharia ya NJI. Nadharia ya NIK iliasisiwa na Kiingi mwaka 1989. NIK ni nadharia changa ya kiistilahi na ya kisasa. Nadharia hii ina sifa saba maalum zinazohusu lugha na uendelezaji au usasaishaji wa istilahi za lugha. Sifa hizo ni pamoja na; kwanza, dhana za kimsingi. Kazi yoyote ya ukuzaji na uendelezaji walugha ianze na dhana za kimsingi, yaani dhana, kitamkwa na istilahi. Dhana ni za kimataifa, kitamkwa na istilahi si vya kimataifa. NIK inasisitiza katika kipengele hiki kwamba dhana mpya zinapoingia katika jamii - tumizi- lugha au sehemu ya jamii, zinafaa kukopwa lakini sio pamoja na istilahi zake.

Dhana inaweza kukopwa lakini iandikwe istilahi faafu. Kile kinachojenga nadharia halisi ni madai yanayokubalika; sheria ya kuongoza uundaji istilahi huongoza katika kutambua usawa wa sentensi kisarufi na kuwepo au kutokuwepo kwa istilahi fulani katika lugha za kurejelea dhana mpya; ni mfumo wa vipindi vya arki vya kidhana. Hii ni sifa moja wapo ya NIK inayojumlisha elementi au arki za kidhana zinazopatikana katika ubongo wa binadamu ; ni sheria ya uundaji istilahi CTR (Conceptual Transformatio Rule) au sheria ya ugeuzi maumbo kidhana. Sheria ya CTR inasisitiza kwamba istilahi mpya hujengeka au huzalishwa pasi na kuzingatia lugha tunayoitumia katika mazungumzo ; sifa inayohusu kanuni CB (Conceptual Bridging Rule) sheria ya kidhana ya kuziba mapengo ya istilahi. Kutokana na sifa hii muhimu ya NIK, suala linalosisitizwa ni vitambulishi vya dhana ; sifa ya mwisho na ambayo ndio muhimu ni vigezo vya istilahi faafu vya PEGITOSCA: Ambavyo ni udhahiri, uangavu, utaratibu uliosawa, uzalishaji kwa mnyambuliko na ufupi wa istilahi.

**2.8. Hitimisho**

Katika sura hii kumejadiliwa kazi zilizotangulia ambazo zinahusiana na mada hii. Maudhui ya sura hii yamebainisha mitazamo ya wataalamu mbalimbali ambao kazi zao zinahusiana na mada ya utafiti huu. Baada ya utangulizi, kumetokea sehemu ya dhana muhimu na mapitio ya kazi tangulizi ambayo nayo imefuatwa na ile ya pengo la utafiti. Mwishoni, mtafiti amejadili mkabala wa kinadharia ambao uliongoza utafiti huu. Sura ifuatayo itajikita katika uchambuzi wa mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1. Utangulizi

Sura hii ndiyo inayowasilisha mbinu zilizotumika katika kukamilisha utafiti huu. Kwa mujibu wa TUKI (2015) mbinu ni namna ya kufanya jambo. Kothari (1990) naye anaeleza kwamba utafiti wa kitaaluma ni wajibu ambao unafanywa kwa kuzingatia mbinu, njia na taratibu zote za utafiti ili uweze kupata matokeo yasiyo na shaka kulingana na kile kilichokusudiwa kutafitiwa. Utafiti huu ni wa kitaaluma, mtafiti lazima afanye lolote awezalo ili kutimiza malengo ya utafiti huu kwa kueleza eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji na uchambuzi wa data.

## 3.2. Usanifu wa Utafiti

Kothari (2008) ameeleza kuwa usanifu wa utafiti ndio unaoonyesha kuwa utafiti husika ulikuwa ni wa namna gani na data zilikusanywa vipi. Ramadani (2018 ) anafalisi usanifu wa utafiti kwa kusisitiza dhima yake, Usanifu wa utafiti ambao kwa wakati mwengine hujulikana kama umbo la utafiti, hutoa picha kamili inayoonyesha namna na jinsi utafiti ulivyofanyika tangu unaanza mpaka unamalizika.

Kwa kutumia Nadhari ya Uchambuzi wa Maudhui, Usanifu wa utafiti huu katika sehemu kubwa ni wa maelezo. Usanifu wa maelezo kama ulivyofafanuliwa na Cohen (2007) ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Mtafiti huzipanga kutokana na maudhui au makundi yanayofanana. Katika utafiti huu, mtafiti amechunguza kamusi ya istilahi kwa kuzichunguza kifani baadhi ya istilahi za LL ya *KT* zinazojikita katika uwanja wa magonjwa zitakazoshughulikiwa kwa kina ili kukamilisha lengo kuu la utafiti. Mtafiti amekuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki, kuvunbua, kufanya majaribio,

kutafisri tarifa alizozozipata kupitia mundo huu wa utafiti. Sehemu ndogo ya utafiti imetumia majedwali kama kielezo.Isitoshe, Nadharia ya kisasa na yenye 'usayansi' ambayo imeongoza kazi hii ni nadhari ya istilahi ya kisayansi (NIK). Maana ya 'usayansi katika mbinu ni uwezo wa mbinu za uundaji istilahi za lugha husika kufanyiwa uchunguzi ili kutambua 'ufaafu' wa kila mojawapo, kwa kuzingatia misingi na kanuni za uendelezaji wa leksia ya lugha husika Mwaro (2000).Msingi wa utaratibu maalum umetumia katika sura hii.Utaratibu huu unaeleza kuwa istilahi iundwe kuambatana na utaratibu fulani wa kuunda.

### 3.3. Mkabala wa Utafiti

Kwa mujibu wa Walliman (2006) mkabala wa utafiti ni utaratibu ambao mtafiti anateua ili kukusanya na kuchambua taarifa kwa mujibu wa kupata majibu ya maswali aliyojiuliza au kupima mabunio aliyojiwekea kwenye utafiti wake. Maoni yake yanawiana na maoni ya TUKI (2012) inapofasili dhana ya mkabala kama utaratibu unaofuatwa kukubali jambo. Mkabala uliotumika katika utafiti na uandishi wa kazi hii ni mkabala wa kitaamuli ambao haukuhusisha data ya kitakwimu kwa kiasi kikubwa. Pia, mkabala huo ulitumiwa katika kuchanganua na kujadili data kimaudhui.

### 3.4. Eneo la Utafiti

Kwa mujibu wa Kothari (2004) eneo la utafiti ni eneo ambalo mtafiti huliteuwa kwa ajili ya kulifanyia utafiti wake ili kumuwezesha kutimiza malengo yake. Utafiti huu umefanyika katika Chuo Kikuu cha Burundi kipatikanacho jijini Bujumbura. Utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani kwa kiasi kikubwa ambapo ulifanyika katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Burundi. Sababu ya kuchagua eneo hilo ni kwamba utafiti huu ulilenga kupata na kusoma maandiko mbalimbali yaliyohusiana na utafiti. Hivyo katika maktaba huo ndiko kulikopatikana machapisho mbalimbali ambayo yalimpatia mtafiti data za msingi na data za upili za utafiti huu. Maktabani humo, mtafiti alisoma kazi tangulizi mbalimbali kama vile majarida, makala,

tasnifu na vitabu vinavyohusiana na mada ya utafiti huu. Siku hizi kuna kazi mbalimbali za kitaaluma zinapatikana mtandani. Kwa kutembelea wavuti tofauti, mtafiti aliweza kupata na kupakua *KT* ambayo ndiyo msingi wa kazi hii. Isitoshe, katika tamasha za madhimisho ya siku ya Kiswahili; Saba Saba iliyofanyikwa kwa mara ya kwanza katika Chuo kikuu cha Burundi Bewa la Mutanga, mfatiti alinunua vitabu vinayoundwa na kamusi mbalimbali.Vitabu hivyo vilimsadia mtafiti kupata uelewa wa mada aliyokuwa ameteua kufanyia utafiti.

### 3.5. Sampuli na Usampulishaji

#### 3.5.1. Sampuli Lengwa

Kwa mujibu wa Kothari (2004) sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo humpatia mtafiti data na kutoa mahitimisho yake. Nalo kundi lengwa a ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti; yaani watu, taasisi, vitu au matukio kwa ujumla ,Walliman (2011). Hivyo, sampuli inatoka katika kundi lengwa ; ni sehemu ya kundi lengwa. Kwa hiyo, katika utafiti huu kundi lengwa ni *Kamusi ya Tiba* (2003).

#### 3.5.2. Usampulishaji

Dhana ya usampulishaji inafasiliwa na Sigh (2007) kama mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Kwa mujibu wa Newman (2006) usampulishaji ndio kitendo chenyewe cha kufanya uteuzi wa sampuli ya utafiti husika. Mtazamo huo unatoa mwanga kuwa mtafiti anapofanya utafiti wowote wa kisayansi lazima aweze kuteua mbinu mwafaka ya kuichagua sampuli ya watafitiwa. Ziko njia mbili za usampulishaji ambazo ni usampulishaji nasibu ambapo uwezekano wa kumchagua mwanakundi lengwa yeyote huwa mkubwa, na usampulishaji usio nasibu ambapo kuchagua sampuli kunatokana zaidi na maamuzi ya mtafiti Butoyi ( 2022).

Katika utafiti huu, michakato ya usampulishaji yote miwili ilitumiwa. Kwanza, usampulishaji usio nasibu ulitumika katika kuichagua kamusi uliyowasilisha hapo juu. Pili, usampulishaji nasibu ulitumika kwa kuzichagua istilahi za uga wa magonjwa katika *KT* miongoni mwa nyuga zingine zilizowasilishwa, yaani kutoka katika kundi lengwa.

### 3.6. Mbinu za utafiti

Utafiti huu umehusu tathmini ya mbinu za uundaji wa istilahi za LL ya *KT*. Mbinu za utafiti ni zile njia zilizotuongoza tangu mwanzo wa utafiti hadi mwishoni wake. Kama anavyosema Kothari (2004) mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa na mtafiti katika kuufanyia kazi utafiti wake. katika sehemu hii kutazungumziwa mbinu zilizotumiwa kukusanyia data na kuchangulia data.

#### 3.6.1. Mbinu za Kukusanyia Data

Akizungumzia kuhusu ukusanyaji wa data, Ame (2017) anasema kuwa mbinu za kukusanyia data ni mbinu ambazo mtafiti huzitumia ili kupata data za utafiti. Naye Kothari (2013) kukusanya data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika.

Katika utafiti huu, katika mchakato wa kukusanya data mbinu ambayo ilitumiwa kwa minajili ya kupata taarifa, kuibua ukweli na kujibu maswali ya utafiti ni mbinu ya mapitio ya nyaraka.

#### 3.6.2. Mapitio ya Nyaraka

Kwanza, mtafiti alisoma kwa makini *KT* tangu mwanzoni hadi mwishoni. Mkakati huu ulimwezesha mtafiti kubainisha istilahi za kamusi hiyo na kuteua istilahi zinazohusiana na magonjwa. Mchakato huo ulikuwa na lengo la kumsaidia mtafiti kujibu maswali ya kwanza na pili la utafiti huu.

Kisha,mapitio ya nyaraka yalifanyika kwa usomaji wa machapisho maktabani na mtandaoni kupitia wavuti tofauti. Hii mbinu ilimweza mtafiti kutalii maktabani na kusoma vitabu, magazeti, tasnifu kadhaa za umahiri na uzamivu zinazozungumzia mada zinazoshabihiana na mada ya utafiti huu. Lengo kubwa la kutalii maktabani ni kuchunguza kile ambacho wataalamu wengine wanasema juu ya mada ya utafiti huu. Hali hii ilimsaidia mtafiti kupata data za upili.. Katika mchakato huu, mtafiti aligundua na kuwasilisha kazi tangulizi za utafiti huu. Isitoshe mbinu hii ilikuwa na manufaa katika utafiti huu kwa kuchangia ufahamu wa nadharia zilizotumiwa katika tafiti za awali.

### 3.6.3. Uchanganuzi wa Data

Ili kufanikisha malengo ya utafiti wetu tumelazimika kufanya uchambuzi wa data tulizokusanya. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kuifasiri data iliyokusanywa kwa kueleza maana ya data hiyo ili kujibu maswali ya utafiti, Hatch (2002). Uchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013) ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika.

Kutokana na data zilizohusika katika utafiti huu ambazo uchanganuzi wake ulilenga kuchunguza mbinu zilizotumiwa katika uundaji wa istilahi za LL ya *KT* baada ya kuzibainisha, kuchunguza sababu za utokeaji wake, kulihusishwa mchanganyiko wa mikabala ya kimaelezo na kitakwimu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Holloway (1997) na Dawson (2007) katika mkabala wa kitaamuli kuna mbinu mbili za uchambuzi wa data: uchambuzi wa data kimaudhui au kimada na uchambuzi linganishi wa data . Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaudhui au kimaelezo kwa kauli nyingine.

Kwa kutumia majedwali, istilahi za tiba zinazohusiana na uga wa magonjwa zilizopendekezwa na mtafiti ziliwasilishwa, na mbinu zilizotumiwa katika uundaji wa istilahi zilitathminiwa kimaelezo. Mkabala wa kimaelezo pia ulitumiwa katika mchakato wa kutoa sababu za matumizi ya mbinu mbalimbali zilizochunguzwa. Kwa kufanya hivi, ilimsaidia mtafiti kuchambua na kujadili data za utafiti kulingana na malengo mahususi na hivyo kujibu maswali ya utafiti.

### 3.7. Maadili ya utafiti

Ni jambo la muhimu kwa utafiti wowote mtafiti akizingatia kanuni za kimaadili zinazotolewa na taasisi husika au mdhamini wa utafiti, pamoja na kanuni za kimataifa, Ruane (2005). Kwa mujibu wa TUKI (2013 )maadili ni mwenendo mwema. Kwa upande wake, Mukuthuria (2010) anasema kuwa maadili ni uwajibikaji na uelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote mtafiti anatungamana nao katika utafiti; uelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa ajili ya binaadamu.

Kwa hiyo, katika kutekeleza utafiti huu, baadhi ya maadili yalizingatiwa. Kwanza, mtafiti aliwasilisha mada kwa Mkurugenzi anayehusika na mkondo wa tafsiri na ukalimani, kisha akaijadili pamoja na wasimamizi wa kazi hii. Pili, alihudhuria semina na mahojiano ya ana kwa ana na ya kwa simu na kuyazingatia mapendekezo yote aliyopewa na wasimamizi wake na ambayo yalilenga kuboresha utafiti huu.

Mwisho, wakati wa uandishi wa ripoti ya utafiti, mtafiti amejiepusha na ubwakuzi kwa kutonakili kazi za watu wengine pasipo kuzingatia taratibu kubalifu za urejeleaji.

### 3.8. Hitimisho

Sura hii imejadili vipengele mbalimbali kuhusiana na mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Kwa ujumla, imezungumzia eneo la utafiti na watafitiwa, sampuli lengwa ya vitafitiwa na

watoataarifa na mchakato wa usampulishaji. Kumezungumziwa pia mbinu za kukusanyia data, mkabala wa kuzichanganua data na maadili ya utafiti huu. Sura ifuatayo itajikita katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data zilizopatikana kutokana na mbinu za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1. Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji, uchambuzi na ufafanuzi wa data kutoka katika *KT* ambayo ndiyo inalengwa na utafiti huu. Katika ukusanyaji na uchambuzi wa data, mtafiti alitumia nadharia ya UMA iliyoasisiwa na Krippendorff (2004) na NIK ilionzishwa na Kiingi ( 1996) na kuendeleza na Mwaro( 2000). Sura hii inatoa taarifa faafu juu ya ukusanyaji wa data na uainishaji wa mbinu za uundaji wa istilahi zilizotumiwa katika mchakato wa uundaji wa istilahi za LL ya *KT*. Aidha, sura hii imegawanywa katika sehemu kuu nne zinazozingatia data zilizopatikana kutokana na malengo mahususi ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza inawasilisha, kubainisha, kuchambua na kujadili data zilizopatikana kutokana na lengo la kwanza ambalo ni kubainisha istilahi zinazohusu magonjwa zilizomo katika *KT* na la pili ambalo ni Kufafanua mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa kuundia istilahi zinazohusu magonjwa zilizomo katika *KT* kupitia utafiti huu. Sehemu ya pili inajihusisha na lengo la tatu la utafiti huu ambalo ni kueleza sababu ya matumizi ya mbinu za kuundia istilahi zinazohusu magongwa zilizomo katika *KT* na sehemu ya tatu inatoa mjadala wa lengo la tatu. Sehemu ya nne nayo inajikita katika kujadili uhusiano baina ya matokeo na kiunzi cha nadharia. Mwisho wa sura unahusisha hitimisho la mjadala utakaokuwa umefanyika katika sura hii.

## 4.2. Uwasilishaji wa Data

Data zinazowasilishwa hapa zimetoka katika *KT*. Data zilizokusanywa zilipatikana kwa njia ya mapitio ya nyaraka. Kwa kupitia nyaraka, mtafiti aliweza kupata data kuhusu istilahi za magonjwa. Mojawapo ya malengo mahususi ya utafiti huu lilikuwa ni kubainisha istilahi za LL ya *KT*. Mtafiti alisoma kwa mara ya kwanza *KT* yote ili kutambua kwa ujumla fikra zilizokuwemo. Kwa kutumia mpangilio wa alfabeti mtafiti aliteua na kusanya istilahi za uwanja wa magonjwa. Pia, mtafiti hakuziorodhesha zote kwa kuwa kazi yake haikuhusu kamwe kunakili *KT* . Istilahi zifuatazo zilizowasilishwa katika jedwali lifuatalo ndizo zinazounda data ya utafiti huu.

**Jedwali Na. 4.1 Data za utafiti**

| Na | **Istilahi ya Kiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|---|
| 1 | A.P.H (ante partum haemorrhage) | Kutokwa damu kabla ya kuzaa (K.D.K.K) apiechi | hali ya hatari ya kutoka damu ukeni wakati wa ujauzito, aghalabu kutokana na kuachia kwa plasenta. |
| 2 | abiotrophy | abiotrofi | kuzeeka mapema kutokana na kufa kwa seli na tishu mwilini kwa sababu ambazo hazijulikani. |
| 3 | ablepharia | ablefaria | hitilafu ya kuzaliwa nayo ya ukosefu, wa vikawa vya macho. |
| 4 | abolumania | abolumania | ugonjwa wa akili ambapo mgonjwa hukosa ari na hubabaika katika kutoa maamuzi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | abscess | jipu | mkusanyiko wa usaha katika tishu kutokana na uambukizo wa vimelea. |
| 6 | acephalocardia | kefalikadia | hitilafu ya kuzaliwa ya kukosekana kwa kichwa na moyo. |
| 7 | acephalocardia | akefalikadia | hitilafu ya kuzaliwa ya kukosekana kwa kichwa na moyo. |
| 8 | achromasia | akromasia | \| ukosefu wa rangi ya mwili. 2 kushindwa kwa seli kushika rangi wakati wa kutia rangi kwenye tishu. |
| 9 | adenoma | adenoma | tyuma ya epithelia yenye asili za tezi |
| 10 | AIDS (Acquired immunodeficiency syndrome) | UKIMWI (Upungufu wa Kinga Mwilini) ya kupata (SIUKIKU-si ya kurithi) | ugonjwa unaosababishwa na virusi vya ukimwi ambao huenezwa kwa ngono, ulawiti, damu (kutiwa damu, sindano chafu, vifaa visivyotakaswa) na uambukizo wa mtoto kutoka kwamama wakati wa ujauzito. Dalili za ukimwi ni pamoja na uambukizo usio mna dalili (hugundulika tu kwa kupima damu, mkojo n.k.) au dalili za magonjwa mbalimbali yanayotokana na kuharibiwa kwa mfumo wa kinga ya mwili; k.m. tiibi, magonjwa ya ngozi, homa za mara kwa mara, uchovu wa mwili na ukondefu. |
| 11 | alveolar abscess | jipu la mzizi wa jino | mkusanyiko wa usaha chini ya mzizi wa jino. |
| 12 | Alzheimer’s desease | ugonjwa wa Alzheimer | ugonjwa wenye dalili za upungufu wa akili kwa watu wa umri wa kati |
| 13 | anticoagulant. | kizuia kuganda | kemikali ambayo huzuia kuganda kwa damu |
| 14 | antifebrile | kituliza homa | dawa ambayo hushusha homa |
| 15 | antritis. | antritisi | inflamesheni ya antramu |
| 16 | aphtous ulcers. | | vidonda vya kinywani ambavyo hurudiarudia |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18 | autoeroticism | mapenzi nafsia | kujiridhisha kingono kwa mtu kujifanyia vitendo fulani yeye mwenyewe |
| 17 | Baker'Cyst, kifuko c | kifuko cha Baker | uvimbe unaojichomoza kutoka gotini na ambao ni henia ya membreni sinoviali ya goti. |
| 20 | beriberi | beriberi | ugonjwa unaotokana na upungufu wa Vitamini $B_1$ katika chakula; |
| 21 | bibliomania | bibliomania | hamu isiyo ya kawaida ya kumiliki vitabu |
| 22 | bilharziasis | kichocho | ugonjwa wa mfumo wa mkojo au wa utumbo unaosababishwa na minyoo ya kichoko. |
| 23 | blastoma | blastoma | tyuma itokanayo na seli za kiinitete |
| 24 | cacotrophy | utapiamlo | maradhi ya mwili yanayotokana na lishe duni au lishe ya kupita kiasi. |
| 25 | cacotrophy | utapiamlo | maradhi ya mwili yanayotokana na lishe duni au lishe ya kupita kiasi. |
| 26 | cancerophobia | kansafobia | woga wa kinurotiki wa kupatwa na |
| 27 | cancerophobia | kansafobia | woga wa kinurotiki wa kupatwa na |
| 28 | catarrh | katara | inflamesheni ya membreni ute |
| 29 | cholecystitis | kolesistitisi | inflamesheni ya kibofu cha nyongo |
| 30 | coryza | mafua | inflamesheni ya mianya ya huambatana na kwa kutokwa kamasi |
| 31 | cystoparalysis | kupooza kwa kibofu cha mkojo | hali ya kukosekana kwa mawasiliano ya neva katika kibofu cha mkojo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 32 | dedentition | kung'oka meno | kutoka kwa meno hasa kutokana na ugonjwa. |
| 33 | dedentition | kung'oka meno | kutoka kwa meno hasa kutokana na ugonjwa. |
| 34 | dedentition | kung'oka meno | kutoka kwa meno hasa kutokana na ugonjwa. |
| 35 | dermatoconiosis | koniosisi ngozi | wa ugonjwa wowote wa ngozi utokanao na vumbi |
| 36 | distention | mtuno, uvimbe | |
| 37 | encephalopathy | enkefalopathi | ugonjwa wowote ule wa ubongo. |
| 38 | enterorrhagia | enterorajia | kuvuja kwa damu katika utumbo |
| 39 | fever | homa | kuzidi kupita kiwango cha joto la mwili. |
| 40 | fournier's disease | gangirini ya fonia | kuoza kwa ngozi ya pumbu ambako chanzo chake hakijulikani. |
| 45 | fulgurant | | maumivu makali sana na ya ghafla, huja kama vile umeme wa radi |
| 46 | gastric ulcer (s) | ki/vidonda cha/vya tumbouondoaji wa mshikano | kidonda au vidonda kadhaa vya membreni ute ya tumbo. |
| 47 | gastroparalysis acoumeter | kupooza kwa tumbokipima sauti | hali ya tumbo kushindwa kufanya kazi.kifaa cha kupimia usikivu. |
| 48 | globus hystericus | histeria ya donge | dalili mojawapo ya _ nurosisi ambapo mwathirika huhisi kana kwamba anakabwa na donge kooni. |
| 49 | glossopathy | glosopathi | ugonjwa wowote ule wa ulimi. |
| 50 | gynatresia. | ginatresia, kuziba kwa uke | hali ya kutokuwepo kwa mwanya, ukeni |
| 51 | haemarthrosis | hemathrosisi | kuvujia kwa damu ndani ya kifundo. |
| 52 | heliophilia | heliofilia | woga wa kupita kiasi wa mwanga wa jua |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 53 | hernia | henia | kujichomoza kwa sehemu ya, au kwa kiungo chote cha ndani ya kaviti ya mwili |
| 54 | hyadatid disease | ugonjwa wa hiadatidi | hali ya kuwa na uambukizo wa wa viluwiluwi vya tegu Taenia echinococcus. |
| 55 | impotence | hanithi | |
| 56 | jaundice, physiological | umanjano wa kifiziolojia | umanjano wa mtoto mzaliwa unaotokana na uchanga wa ini wa kutoweza kukonjugeti kemikali ya bilirubini kwa kasi ya kutosha |
| 57 | Lagnesis | ukware | uchu wa kupindukia wa ngono |
| 58 | leucoderma | lukodema | ugonjwa wa ngozi wa mabaka meupe (kwa kukosa rangi) ambayo huzungukwa na ngozi ya rangi iliyokolea zaidi. |
| 59 | leukoplakia | lukoplakia | ugonjwa kroniki wa mabaka meupe katika ulimi au katika membreni ute za kinywani au za jenitalia; mara nyingine hupelekea kansa. |
| 60 | leukoplakia | lukoplakia | ugonjwa kroniki wa mabaka meupe katika ulimi au katika membreni ute za kinywani au za jenitalia; mara nyingine hupelekea kansa. |
| 61 | malaria | malaria | ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vimelea vya kundi la protozoa vya plasmodia ambao huenezwa kwa kuumwa na mbu jike aina ya anofelesi. Dalili za malaria ya kawaida ni homa, maumivu ya viungo, kuumwa kichwa, kichefuchefu n.k. Dalili za malaria kali ni mojawapo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | au zaidi ya moja kati ya hizi zifuatazo: degedege, kuchanganyikiwa na akili, kupoteza fahamu, upungufu mkubwa wa damu, kushindwa kwa figo kufanya kazi, kukojoa mkojo wenye rangi hudhurungi, mwili kuwa manjano. |
| 62 | meningitis | meninjitisi, homa ya uti wa mgongo | inflamesheni ya meninjesi; husababishwa na makundi mbalimbli ya vimelea k.m. virusi, bakteria, kuvu na protozoa. |
| 63 | meningitis | meninjitisi, homa ya uti wa mgongo | inflamesheni ya meninjesi; husababishwa na makundi mbalimbli ya vimelea k.m. virusi, bakteria, kuvu na protozoa. |
| 64 | noma | noma | kidonda cha shavu na kinywa au cha vulva na uke |
| 65 | nosohaemia | nosohemia | ugonjwa wowote wa damu. |
| 66 | nosohaemia | nosohemia | ugonjwa wowote wa damu. |
| 67 | obesity | unene | kuongezeka kwa mafuta mwilini kupita kiasi. |
| 68 | obstipation, contipation | konstipesheni, kufunga choo | hali ya kushindwa kupata haja kubwa kulingana na kawaida ya mhusika au hali ya kujisaidia kinyesi kigumu |
| 69 | occupational diseases | magonjwa ya mazingira, magonjwa ya kikazi | magonjwa yanayotokana na aina ya kazi aifanyayo mtu. |
| 70 | pachychilia | pakikilia | unene usiokuwa wa kawaida wa midomo. |
| 71 | palmar abscess | jipu la kiganja | jipu katika peritoniumu ya pelvisi. |
| 72 | palmar abscess aerobiology | jipu la kiganjabiolojia hewa | tanzu ya biolojia inayohusu viumbe vilivyomo hewani. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 73 | pertussis | kifaduro | ugonjwa wa kikohozi cha muda mrefu unaosababishwa na bakteria wa spishi ya Bodetela |
| 74 | pharyngopathy | faringopathi | ugonjwa wowote ule wa koromeo |
| 75 | post-haemorrhage | utokaji damu kwa mara nyingine tena | |
| 76 | reticulosarcoma | retikulosakoma | aina ya sakoma yenye seli za retikula za tezi za limfu au za uboho. |
| 77 | sea sickness | kigegezi cha baharini | hali ya kichefuchefu, kutapika, kizunguzungu na uchovu wa mwili ambao huwapata baadhi ya watu wanaposafiri na chombo cha majini kama meli. |
| 78 | sexual diseases | magonjwa ya kujamiiana, magonjwa ya ngono kujamiiana | magonjwa yanayoenezwa aghalabu kwa njia ya |
| 79 | sprue | spruu | ugonjwa wa kuhara wa muda mrefu unaoambatana na kutoa choo cha mafuta, vidonda vya kinywani, kukonda na anemia. |
| 80 | struma | struma | 1 uvimbe wa tezi ya shingo ya thiroidi |
| 81 | sursanure | | kidonda ambacho kimepona kwa juu lakini kwa ndani bado. |
| 82 | tetanus | tetanasi, pepopunda | ugonjwa unaotokana na sumu kali (toksini) ya bakteria klostridiumu tetani; |
| 83 | tetralogy of Fallot | unne wa Fallot | hitilafu ya kuzaliwa ya moyo yenye dosari nne ambazo ni: pulmonari. (ii) kuenea kwa mshipa mkuu wa moyo (mkole/aota) hadi upande wa kulia wa moyo-kiasi kwamba: mshipa hupokea damu kutoka: ventrikali za kushoto na kulia za moyo (badala ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ventrikali ya kushoto tu). (iii) kuwepo tundu katika kiambaza cha ventrikali. (iv) hipatrofi ya ventrikali ya kulia ya moyo. |
| 84 | thrombokinesis | thrombokinesisi | ugandaji wa damu. |
| 85 | thrombokinesis | thrombokinesisi | ugandaji wa damu. |
| 86 | ulaemorrhagia | ulemorajia. | utokwaji na damu kutoka katika kovu |
| 87 | venereal diseases<br>radiobiolgy | magonjwa ya ngono, magonjwa ya kujamiiana<br><br>biolojia miale | magonjwa ambayo huambukiza kwa njia ya ngono<br>tanzu ya elimu inayohusu athari ya miale ya nishati kubwa katika viumbe hai. |
| 88 | vertigo | kizunguzungu, kizungupia | hisia ya kukosa mizania ya mwili; hutokea kwa sababu za kisaikolojia au kutokana na magonjwa ya masikio, macho, ubongo, tumbo au damu. |
| 99 | whiteleg | | mguu uliovimba kutokana na thrombosisi ya vena ya femora. |
| 90 | whooping cough | ugonjwa wa kifaduro | aina ya kikohozi cha muda mrefu hususan kwa watoto ambacho husababishwa na bakteria aina ya Bodetela. |
| 91 | xerasis | zerasisi | ugonjwa wa kukauka na kushindwa kukua kwa nywele |
| 92 | zoanthropy | zoanthropi | aina ya ugonjwa wa akili ambapo mwathirika hudhania kwamba amegeuka kuwa mnyama. |
| 93 | zoonoses | zuonosia | magonjwa yenye asili ya wanyama ambayo pia huweza kuenezwa kwa binandamu. |

**Chanzo**: ***KT***, ***Septemba, 2024***

## 4.3. Istilahi za Uwanja wa Magonjwa katika LL ya *KT* na Mbinu za Uundaji Istilahi Zilizotumiwa

Katika sehemu hii, mtafiti alishughulikia lengo la pili la utafiti huu. Lengo la pili ni kufafanua mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa katika mchakato wa uundaji wa istilahi za uwanja ulioteuliwa kutoka *KT*.

Uchambuzi wa Data ulidhihirisha istilahi za aina ya magonjwa kutoka LL ya *KT*. Pia, kulidhihirika mbinu mbalimbali za uundaji istilahi zilizotumiwa kuundia istilahi za uwanja wa magonjwa katika LL ya *KT*. Ili kutoa uelewa wa moja kwa moja, kwa kila mbinu ya uundaji wa istilahi iliyotathminiwa, mtafiti alitumia jedwali ambalo linaonyesha mifano kwa kila aina ya mbinu naohusika na utafiti huu. Chini ya jedwali kumewekwa ufafanuzi zaidi kwa madhumuni ya kujadili matokeo na kukamilisha uelewa. Kwa kuchambua data zilizowasilishwa mbinu zilizogunduliwa ni hizi zihfuatazo:

### 4.3.1. Ukopaji

Kwa mujibu wa Vinay na Darbelnet (2004) ukopaji ni mkakati wa tafsiri wa kuhamisha neno au dhana ya lugha chanzi kwenda LL. Kuna aina tatuza ukopaji, yaani ukopaji wa moja kwa moja kutoka LC kwenda LL bila kufanya marekebisho yoyote. Pia, mbinu hiyo inajulikana kama uwasilishaji Were-Mwaro (2000). Aina ya pili ya ukopaji inahusu kufanyia neno la LC marekebisho yaani utohozi ili liendane na kaida za LL. Tatu, ni uhawilishaji ambao ni mchakato wa kuhamisha neno la LC kwenda katika LL likiwa limefanyiwa marekebisho kidogo. Uhawilishaji unajumuisha kuandika herufi za alfabeti ya lugha moja kwa herufi za alfabeti ya lugha nyingine (Jilala, 2021; Child, 1992; Armstrong, 2005).

Istilahi za LL ya *KT* ziliundwa kwa matumizi ya aina hizo mbili za ukopaji kama ilivyodhihirika katika sehemu ifuatayo.

#### 4.3.1.1. Ukopaji wa Moja kwa Moja.

Mbinu hii ya ukopaji wa moja kwa moja inajulikana pia kwa jina la uhamishaji kamili au uwasilishaji. Mbinu hii inahusu ukopaji wa neno au istilahi kutoka LC kwenda LL bila kulifanyia marekebisho yoyote. Kwa hiyo, hapa chini jedwali Na. 4.1 linawasilisha mifano inayodhihirisha matumizi ya mbinu hiyo. Mifano hiyo ilitokana na data zilizokusanywa kutoka *KT* kwa kujishinikiza kwenye LL.

**Jedwali Na. 4.2. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Ukopaji wa Moja kwa Moja**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| abolumania | abolumania | ugonjwa wa akili ambapo mgonjwa hukosa ari na hubabaika katika kutoa maamuzi. |
| adenoma | adenoma | tyuma ya epithelia yenye asili za tezi |
| beriberi | beriberi | ugonjwa unaotokana na upungufu wa Vitamini $B_1$ katika chakula; |
| bibliomania | bibliomania | hamu isiyo ya kawaida ya kumiliki vitabu |
| blastoma | blastoma | tyuma itokanayo na seli za kiinitete |
| influenza | influenza | mafua makali ya virusi vya influenza; dalili zake ni mafua, homa, uchovu kikohozi n.k. |
| malaria | malaria | ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vimelea vya kundi la protozoa vya plasmodia ambao huenezwa kwa kuumwa na mbu jike aina ya anofelesi. Dalili za malaria ya kawaida ni homa, maumivu ya viungo, kuumwa kichwa, kichefuchefu n.k. Dalili za malaria kali ni mojawapo au zaidi ya moja kati ya hizi zifuatazo: degedege, kuchanganyikiwa na akili, kupoteza fahamu, upungufu mkubwa wa damu, kushindwa kwa figo kufanya kazi, kukojoa mkojo wenye rangi hudhurungi, mwili kuwa manjano. |
| noma | noma | kidonda cha shavu na kinywa au cha vulva na uke |
| struma | struma | 1 uvimbe wa tezi ya shingo ya thiroidi |

**Chanzo**: ***KT***, ***Septemba, 2024***

Katika jedwali hapo juu kulibainika matumizi ya mbinu ya ukopaji wa moja kwa moja au uhamishaji katika uundaji wa istilahi za LL ya *KT* zinazohusu uwanja wa magonjwa. istilahi katika LL zilipatikana bila vidahizo kufanyiwa marekebisho yoyote. Katika matumizi ya mbinu hiyo,kama inavyodhihirika katika jedwali Na. 4.1, watunzi, baada ya kukopa istilahi kama ilivyokuwa katika LC na kuiwasilisha vilevile katika LL, waliambatanisha na maana ya istilahi katika LL, yaani Kiswahili.

Kuna kazi tangulizi zilizozungumzia ukopaji kamili ambazo zinawiana na kazi hii. Hoffer (2005) anaeleza kuwa mzungumzaji wa lugha anaweza kuchukua kama lilivyo kutoka lugha chanzi na kulitumia katika lugha pokezi.

**4.3.1.2. Utohozi**

Katika sehemu hii kunazungumziwa namna waundaji wa istilahi za LL ya *KT* walivyotumia mbinu hii katika kuunda istilahi za uwanja wa magonjwa . Utafiti huu ulibaini kuwa waundaji wa istilahi walitumia mbinu ya utohozi.Utohozi ni mtindo wa kuchukua msamiati wa lugha asilia na kuutafsiri au kuunukuu kwa kufuata kaida za kifonolojia na kimofolojia za lugha pokezi. kwa mujibu wa Venuti ( 2000) mbinu ya ukopaji ndiyo mbinu rahisi zaidi ya tafsiri. Naye Stephano (2018) anasema kuwa kutoholewa kwa elementi ni kuziboresha ili ziendane na miundo na maumbo ya LC. Data za utafiti huu zilidhirisha kuwa baadhi ya istilahi za LL ya *KT* zilizotolewa zimetokana na matumizi ya mbinu hii katika kuunda mchakato wa kuunda istilahi hizo. Jedwali lifuatalo linatoa mifano inayoendana na hali hiyo.

**Jedwali Na. 4.3 Istilahi Kutokana Utohozi**

| **Istilahi yaKiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| abiotrophy | abiotrofi | kuzeeka mapema kutokana na kufa kwa seli na tishu mwilini kwa sababu ambazo hazijulikani. |
| ablepharia | ablefaria | hitilafu ya kuzaliwa nayo ya ukosefu, wa vikawa vya macho. |
| acephalocardia | kefalikadia | hitilafu ya kuzaliwa ya kukosekana kwa kichwa na moyo. |
| achromasia | akromasia | \| ukosefu wa rangi ya mwili. 2 kushindwa kwa seli kushika rangi wakati wa kutia rangi kwenye tishu. |
| catarrh | katara | inflamesheni ya membreni ute |
| cholecystitis | kolesistitisi | inflamesheni ya kibofu cha nyongo |
| encephalopathy | enkefalopathi | ugonjwa wowote ule wa ubongo. |
| glossopathy | glosopathi | ugonjwa wowote ule wa ulimi. |
| haemarthrosis | hemathrosisi | kuvujia kwa damu ndani ya kifundo. |
| hernia | henia | kujichomoza kwa sehemu ya, au kwa kiungo chote cha ndani ya kaviti ya mwili |
| leucoderma | lukodema | ugonjwa wa ngozi wa mabaka meupe (kwa kukosa rangi) ambayo huzungukwa na ngozi ya rangi iliyokolea zaidi. |
| leukoplakia | lukoplakia | ugonjwa kroniki wa mabaka meupe katika ulimi au katika membreni ute za kinywani au za jenitalia; mara nyingine hupelekea kansa. |
| meningitis | meninjitisi, homa ya uti wa mgongo | inflamesheni ya meninjesi; husababishwa na makundi mbalimbli ya vimelea k.m. virusi, bakteria, kuvu na protozoa. |

| | | |
|---|---|---|
| nosohaemia | nosohemia | ugonjwa wowote wa damu. |
| obesity | unene | kuongezeka kwa mafuta mwilini kupita kiasi. |
| obstipation, contipation | konstipesheni, kufunga choo | hali ya kushindwa kupata haja kubwa kulingana na kawaida ya mhusika au hali ya kujisaidia kinyesi kigumu |
| pachychilia | pakikilia | unene usiokuwa wa kawaida wa midomo. |
| pharyngopathy | faringopathi | ugonjwa wowote ule wa koromeo |
| reticulosarcoma | retikulosakoma | aina ya sakoma yenye seli za retikula za tezi za limfu au za uboho. |
| sprue | spruu | ugonjwa wa kuhara wa muda mrefu unaoambatana na kutoa choo cha mafuta, vidonda vya kinywani, kukonda na anemia. |
| tetanus | tetanasi, pepopunda | ugonjwa unaotokana na sumu kali (toksini) ya bakteria klostridiumu tetani; |
| thrombokinesis | thrombokinesisi | ugandaji wa damu. |
| ulaemorrhagia | ulemorajia. | utokwaji na damu kutoka katika kovu |
| xerasis | zerasisi | ugonjwa wa kukauka na kushindwa kukua kwa nywele |
| zoanthropy | zoanthropi | aina ya ugonjwa wa akili ambapo mwathirika hudhania kwamba amegeuka kuwa mnyama. |
| zoonoses | zuonosia | magonjwa yenye asili ya wanyama ambayo pia huweza kuenezwa kwa binandamu. |

**Chanzo**: ***KT*, *Septemba, 2024***

Mifano katika jedwali Na. 4.3 inaonyesha kuwa watunzi wa *KT* walitumia kwanza mbinu ya utohozi katika mchakato wa kuunda istilahi za LL ya kamusi hiyo. Katika kuzifafanua istilahi husika, kulitumiwa mbinu ya tafsiri kimaelezo kwa kuwasilisha maana yake. Aidha, mifano inaonyesha kuwa tafsiri ya vidahizo vilivyojitokeza kama neno mojamoja katika LC ilifanyika kwa neno mojamoja pia katika LL. Kwa mfano kidahizo "carminative" kimetafsiriwa kwa "kaminativu", "dermatoglyphics" kama "dematoglifikia".

#### 4.3.1.3. Ukopaji kwa Uhawilishaji.

Kama ilivyoelezwa awali, uhawilishaji ni mchakato wa kuhamisha neno kutoka LC kwenda LL likiwa limefanyiwa uboreshwaji mdogo,Jilala (2021). Katika muktadha huu, neno likikopwa linafuata ruwaza na muundo wa LC katika LL. Mbinu hiyo ilitumika kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

**Jedwali Na. 4.4 Istilahi Kutokana na Mbinu ya Ukopaji kwa Uhawilishaji**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| antritis. | antritisi | inflamesheni ya antramu |
| gynatresia. | ginatresia, kuziba kwa uke | hali ya kutokuwepo kwa mwanya, ukeni |
| leukoplakia | lukoplakia | ugonjwa kroniki wa mabaka meupe katika ulimi au katika membreni ute za kinywani au za jenitalia; mara nyingine hupelekea kansa. |
| meningitis | meninjitisi, homa ya uti wa mgongo | inflamesheni ya meninjesi; husababishwa na makundi mbalimbli ya vimelea k.m. virusi, bakteria, kuvu na protozoa. |
| nosohaemia | nosohemia | ugonjwa wowote wa damu. |
| thrombokinesis | thrombokinesisi | ugandaji wa damu. |

**Chanzo**: ***KT*, *Septemba, 2024***

Jedwali Na. 4.4 hapo juu linaonesha kuwa uundaji wa istilahi za LL ya *KT* umetumia mbinu ya uhawilishaji kwa kuhamisha neno kama lilivyo kutoka katika LC kwenda katika LL . Pia baada ya kufuata ruwaza na muundo wa LC katika LL kumewasilisha maana yake katika LL yaani Kiswahili. Mbinu hii inatofautiana kidogo na mbinu ya utohozi. Wakati utohozi inamaanisha mtindo wa kuchukua msamiati wa lugha asilia na kuutafsiri au kuunukuu kwa kufuata kaida za kifonolojia na kimofolojia za lugha pokezi k.m ‘‘encephalopathy’’ na utohozi wake ‘‘enkefalopathi y’’. Hapa, konsonanti /c/ iligeuzwa katika /k/, /ph/ katika /f/ na / y/ katika vokali /i/, yaani fonolojia 2 na vokali 1. Ila, uhawilishaji unajumuisha kuandika herufi za alfabeti ya lugha moja kwa herufi za alfabeti ya lugha nyingine ; km istilahi «placebo» ambayo ilitafsiriwa kama /plasebo/ kwa kubadilisha fonimu /c/ katika /s/ tu/.

#### 4.3.1.4. Uhamishaji na Kisawe

Mbinu hii ya uundaji wa istilahi kwa uhamishaji na kisawe iliwasilishwa na Odoyo (2012) aliposhughulikia ‘‘Nafasi ya Tafsiri katika Taaluma ya Onomastiki’’kwa kuzingatia mbinu tafsiri ya toponomastiki. Alipendekeza kuwa nomino pekee zihamishwe bila kufaniwa marekebisho yoyote. Ila ni vyema kuambatanisha na kisawe kwa kubainisha ugunduzi wa mtafiti maalum.

Utafiti huu ulibaini kuwa, katika uundaji wa istilahi za uwanja wa magonjwa kupitia LL ya *KT* waundaji wa istilahi hizo walitumia mbinu ya tafsiri kwa uhamishaji na Kisawe. Hii ni mbinu ya ukopaji ambapo sehemu moja ya istilahi ni asilia iliyokopwa na nyingine imetafsiriwa. Katika kuchambua data zilizotumiwa katika utafiti huu, matumizi ya mbinu hii yalitambulika kama inavyodhihirishwa na mifano katika jedwali Na. 4.4 hapo kwenye ukurasa ufuatao.

**Jedwali Na.4.5. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Uhamishaji na Kisawe**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| Alzheimer's desease | ugonjwa wa Alzheimer | ugonjwa wenye dalili za upungufu wa akili kwa watu wa umri wa kati |
| Jackson's epilepsy | kifafa cha Jackson | aina hii ya kifafa husababishwa na lesheni katika koteksi-mota ya ubongo. |
| Baker'Cyst, kifuko c | kifuko cha Baker | uvimbe unaojichomoza kutoka gotini na ambao ni henia ya membreni sinoviali ya goti. |
| tetralogy of Fallot | unne wa Fallot | hitilafu ya kuzaliwa ya moyo yenye dosari nne ambazo ni: pulmonari. (ii) kuenea kwa mshipa mkuu wa moyo (mkole/aota) hadi upande wa kulia wa moyo-kiasi kwamba: mshipa hupokea damu kutoka: ventrikali za kushoto na kulia za moyo (badala ya ventrikali ya kushoto tu). (iii) kuwepo tundu katika kiambaza cha ventrikali. (iv) hipatrofi ya ventrikali ya kulia ya moyo. |

**Chanzo**: ***KT*, *Septemba, 2024***

Mifano iliyomo kwenye jedwali Na. 4.5 inaonyesha kuwa istilahi za majina ya watu hazikutoholewa ; zilihamishwa kama bila mabadiliko yoyote kutoka katika LC kwenda LL. Kujiepusha tutafsiri majina ya watu kunaonekana kama mbinu ya kuundia istilahi za LL ya *KT*. Majina hayo ya watu yalitumiwa katika LL bila kubadilishiwa muundo. Majina hayo ni ya mabingwa wa tiba waliofanya utafiti na kuiendeleza sayansi ya tiba katika muktadha fulani. Isitoshe, mbinu hiyo iliweza kutumika katika mchakato wa uundaji wa baadhi ya visawe kwa istilahi zinazohusu magonjwa tu. Km, tafsiri ya istilahi‘‘Alzheimer's desease'' ilitafsiriwa kama‘‘ugonjwa wa Alzheimer''. Nomino pekee ‘‘ Alzheimer'' ilihamishwa kama ilivyokuwa katika LC kwenda LL, istilahi ‘‘ desease'' ilitafsiriwa kwa kutafutiwa kisawe katika LL kama‘‘ ugonjwa''.Mbinu ilitumiwa vile vile katika mchakato wa kutafsiri istilahi‘‘Baker'cyst'' ambapo nomino peekee ‘‘ Baker'' ilihamishwa kisha kuunganishwa na kisawe cha istilahi‘‘cyst'' kama ‘‘ kifuko''. Isitoshe, data ilidhihirisha kwamba mbinu hii iliambatanishwa

na mbinu ya Tafsiri Elezi ; km katika ‘‘Alzheimer’s desease’’ ambayo ilitafsiriwa kama‘‘ugonjwa wa Alzheimer : ugonjwa wenye dalili za upungufu wa akili kwa watu wa umri wa kati’’.

Uchanganuzi wa data unaonesha kwamba aina zote za ukopaji zilitumiwa na wanaistilahi waliounda istilahi za LL ya *KT*. Mara kwa mara, mbinu ya kutoa maelezo ya dhana husika kwa Kiswahili fasaha ilitumika pamoja na mbinu ya uhamishaji na utohozi.

Kuna kazi tangulizi zilizoshughulikia tathmini na uchunguzi wa mbinu za uundaji wa istilahi za nyuga mbalimbali zinazoshabihiana na hii. Kazi hizo zinahakikisha matumizi ya mbinu ya kukopa neno au istilahi kama iilivyo ama kwa kuitohoa au kuihawilisha bila ya kusahau kuiambatanisha na kisawe kimoja kutoka lugha asili. Hervey na mwenzake (1992) wanaeleza kuwa kuna mbinu mbili za uundaji istilahi kwa kukopa. Mbinu hizo hutumia mkakati wa kutafsiri nomino za pekee, ambapo jina linaweza kuhamishwa moja kwa moja kutoka LC kwenda LL bila kufanyiwa mabadiliko yoyote au linaweza kutoholewa ili lifanane kimatamshi na kimaandishi na maneno asili ya LL. Hoffer (2005) anaeleza kuwa mzungumzaji wa lugha anaweza kukopa neno na kulibadilisha na kuwa na matamshi ya lugha pokezi. Pili, anaweza kuchukua kama lilivyo kutoka lugha chanzi na kulitumia katika lugha pokezi. Tatu, anaweza kubadilisha sehemu ya neno tu, yaani sehemu moja kuwa ya mkopo na nyingine kuwa ya asili. King’ei (2010) anadai kuwa lugha ya Kiingereza imekopa msamiati mwingi kutoka lugha za Kilatini, Kigiriki, Kifaransa, Kijerumani na Kiarabu. Guerra (2012) akinukuliwa na Singoei na wenza ( 2020) wanaongezea kwa kusema kuwa ukopaji ni njia kuu ya kuitajirisha lugha pokezi kimsamiati. Mbinu hii kwa kawaida hutumika wakati istilahi husika imekosa kabisa kisawe chake katika tamaduni lengwa au iwapo mfasiri anajaribu kupata athari ya mtindo wa MC. Adolph (2019) aligundua kuwa wakati wa utohozi wa istilahi katika Kiswahili, michakato mbalimbali ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia hufanyika. Michakato hiyo hufanyika kadiri kanuni na taratibu za lugha ya Kiswahili zilivyo ili istilahi ziweze kukubalika katika hiyo

lugha. Isitoshe, Adolph (2024) alihakikisha kuwa tafsiri mkopo ya msamiati wa Kiingereza ina mchango mkubwa katika suala zima la kukuza lugha ya Kiswahili. Adika (2021) aligundua kwamba kati ya aina tatu za ukopaji, yaani utohozi, uwasilishaji na tafsiri mkopo; tafsiri mkopo ndiyo iliyochangia idadi kubwa ya istilahi mkopo.

Ufanano mkubwa wa tafiti za wanazuoni hao na huu ni kuwa zote zinalenga kutambua namna mbinu ya ukopaji inavyotumiwa katika mchakato wa uundaji wa istilahi. Hata hivyo, tafiti zao zinaegemea kwenye tathmini na uchambuzi wa kina wa matumizi ya mbinu moja ambapo utafiti huu unalenga kutathmini mbinu tofauti za uundaji wa istilahi za LL kamusi ikichukua mfano wa uwanja wa magonjwa upatikanao katika *KT*.

**4.3.2. Mbinu ya Usawe**

Kwa mujibu wa TUKI (2013) kisawe ni moja kati ya maneno mawili au zaidi yanayokaribiana kimaana, sawa na sinonimu. Naye Venuti ( 2012) anasema kuwa historia ya tafsiri inajengeka katika msingi wa usawe na uamilifu. Anakazia kwa kusema kuwa fasili ya usawe huelezwa kwa kutumia dhana kama vile usahihi, utoshelevu, ulinganifu na uaminifu. Hivyo, lengo kuu la matumizi ya mbinu ya usawe ni kuweza kudumisha athari ile ile ya ujumbe wa LC kwa hadhira lengwa. Mifano iliyomo katika jedwali Na 4.5 inadhihirisha kuwa mbinu ya usawe iliyotumiwa si moja. Hivyo, kuna mbinu za usawe kamilifu, usawe nusu, usawe kwa upana na usawe finyu.

Utafiti huu ulibaini kuwa, katika uundaji wa istilahi za LL ya *KT* katika mchakato wa kuunda istilahi za uwanja wa magonjwa, kulitumiwa mbinu ya tafsiri ya visawe kamilifu.Mbinu hio hutumika kwa kutafsiri neno husika kutoka LC kwa kutumia visawe linganifu katika LL,Newmark (1988). Data za utafiti huu zilidhirisha kuwa baadhi ya istilahi za LL ya *KT* yaani katika Kiswahili zimetokana na matumizi ya mbinu hii ya kisawe kamilifu kama inavyodhihirika katika mifano iliyomo kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali Na.4.6. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Kisawe na Maelezo**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| abscess | jipu | mkusanyiko wa usaha katika tishu kutokana na uambukizo wa vimelea. |
| bilharziasis | kichocho | ugonjwa wa mfumo wa mkojo au wa utumbo unaosababishwa na minyoo ya kichoko. |
| coryza | mafua | inflamesheni ya mianya ya huambatana na kwa kutokwa kamasi |
| distention | mtuno, uvimbe | |
| fever | homa | kuzidi kupita kiwango cha joto la mwili. |
| impotence | hanithi | |
| Lagnesis | ukware | uchu wa kupindukia wa ngono |
| vertigo | kizunguzungu, kizungupia | hisia ya kukosa mizania ya mwili; hutokea kwa sababu za kisaikolojia au kutokana na magonjwa ya masikio, macho, ubongo, tumbo au damu. |
| whooping cough | ugonjwa wa kifaduro | aina ya kikohozi cha muda mrefu hususan kwa watoto ambacho husababishwa na bakteria aina ya Bodetela. |

**Chanzo**: ***KT***, ***Septemba, 2024***

Jedwali Na. 4.6 hapo juu linaonyesha istilahi za LL ya *KT* ambazo zimetokana na visawe vinavyowiana na maneno ya LC, yaani Kiingereza. Kwa mujibu wa Panou (2013) kisawe kamilifu hutokea wakati dhana husika zinapolingana kimaana hivi kwamba zinarejelea kitu kimoja kilichoko katika LC na LL. Mifano ya matumizi ya kisawe kamilifu ni kama vile “bilharziasis” na kisawe chake “kichocho”; “vertigo” na kisawe chake “kizunguzungu”/ “kizungupia” ; “impotence” na kisawe chake “hanithi”,n.k . Kuhusu usawe nusu, Panou ( 2013) anaeleza kwamba dhana hutofautiana katika LC na LL. Aidha, dhana inaweza kuwepo katika LC na kutokuwepo katika LL.

Katika mifano iliyowasilishwa, usawe ulijitokeza , na mara baada ya kisawe kuwasilishwa, maelezo ya istilahi husika yaliwasilishwa ili yasaidie katika kupata uelewa kamili katika LL. Kwa mfano, kidahizo "obesity"kilitafusiliwa kwa "unene", na kisawe hiki kikaongezewa maelezo *"kuongezeka kwa mafuta mwilini kupita kiasi"*. Maelezo haya yanasaidia katika kutambulisha kwa watumizi wa kamusi kuwa ni unene wa kiasi gani unazungumziwa katika muktadha huu. Kama anavyosema Panou (2013) utafiti huu ulihakikisha kuwa matumizi ya usawe unaokaribiana unatumiwa kuonyesha kwamba neno au dhana katika LC inaelezwa kwa dhana au neno jingine kutoka LL ambalo ni sawa na hilo lakini lisilolingana nalo. Mkakati huu huhakikisha kuwa istilahi au kijelezi kinatafsiriwa kwa kuzingatia uakisi wa umbo au uamilifu wake. Hivyo, huweza kuchukuliwa kama namna ya kufafanua dhana kwa kutolea maelezo au mifano ili ipate kueleweka zaidi, Singoei ( 2020). Pia, mbinu hii iliambatanishwa mara kwa mara na mbinu ya tafsiri kimaelezo.

Kazi tangulizi zilizoshughulikia zinazoshabihiana na hii zinahakikisha matumizi ya mbinu ya tafsiri kwa kutumia kisawe. Newmark (1988) alithibitisha kuwa hii hutumika kwa kutafsiri neno la LC kwa kutumia visawe linganifu kutoka katika LL. Naye Jilala ( 2021) aliona kuwa katika uundaji wa istilahi za sayansi na teknolojia, waundaji wa istilahi hutumia mbinu ya tafsiri kwa visawe kamilifu.kwa kutimiza kubwa katika tafsiri ambayo ni kutafuta visawe katika LL. Visawe vinapokosekana ndipo mbinu nyingine za kuhawilisha ujumbe katika LL hutumiwa. Katika hatua ya uchambuzi, mfasiri huyatafutia maneno ya LC visawe kutoka katika LL.

Upande mmoja, ufanano mkubwa uliopo baina ya tafiti za wanazuoni hao na huu ni kuwa zote zinaafikiana kuwa kazi kubwa ya tafsiri ni kutafuta visawe japo katika utafiti huu, matumizi ya visawe vya LL hayakujitokeza kwa kiasi kikubwa. Upande mwingine utofauti kati ya tafiti tangulizi na utafiti huu ni kuwa katika mchakato wa uundiji wa istilahi za LL ya *KT* kwa kutumia mbinu ya kisawe, waundaji waliambatanisha visawe na uwasilishaji wa maana yake katika LL kwa lengo la kurahisisha uelewa zaidi kwa hadhira.

### 4.3.3. Mbinu ya Tafsiri Sisisi na Utohozi

Utafiti huu ulibaini kuwa, katika uundaji wa istilahi za LL ya *KT* kulitumiwa mbinu ya tafsiri sisisi kwa kutafutia visawe kamilifu pale ambapo utohozi wenyewe hukuweza kukamilisha mahitaji. Mbinu hii hutumika kwa kutafsiri neno la LC kwa kutumia visawe linganifu kutoka katika LL Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili. Mifano iliyowasilishwa kwenye jedwali hapo chini inadhihirisha matumizi ya mbinu hiyo.

**Jedwali Na. 4.7. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Sisisi na Utohozi**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| dermatoconiosis | koniosisi ngozi | wa ugonjwa wowote wa ngozi utokanao na vumbi |
| fournier's disease | gangirini ya fonia | kuoza kwa ngozi ya pumbu ambako chanzo chake hakijulikani. |
| jaundice, physiological | umanjano wa kifiziolojia | umanjano wa mtoto mzaliwa unaotokana na uchanga wa ini wa kutoweza kukonjugeti kemikali ya bilirubini kwa kasi ya kutosha |
| hyadatid disease | ugonjwa wa hiadatidi | hali ya kuwa na uambukizo wa wa viluwiluwi vya tegu Taenia echinococcus. |
| globus hystericus | histeria ya donge | dalili mojawapo ya _ nurosisi ambapo mwathirika huhisi kana kwamba anakabwa na donge kooni. |

**Chanzo**: ***KT*, *Septemba, 2024***

Mifano iliyowasilishwa katika Jedwali Na.4.7 inathibitisha matumizi wa mbinu ya tafsiri sisisi na utohozi kwa wakati mmoja katika uundaji wa istilahi za LL ya *KT* kupitia uwanja wa magonjwa. Kwa kiasi kikubwa, mbinu hii inahusu istilahi ambazo zinaundwa kwa mwambatano wa maneno mawili au zaidi, yaani istilahi ambatano au virai (vya a- unganishi). Kwa mfano, istilahi “hyadatid disease” ilitafsiriwa kwa “ugonjwa wa hiadatidi”.

Pia, waundaji wa istilahi za LL ya *KT* waliambatanisha na uwasilishaji wa maana ya istilahi iliyopatikana kwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi na utohozi. .

Kazi tangulizi zilizoshughulikia tathmini na ufafanuzi wa mbinu za tafsiri zinathibitisha matumizi ya mbinu ya tafsiri sisisi na utohozi. Aghajani na mwenzake (2018) waligundua kuwa mbinu hii inafaa katika mchakato wa tafsiri baina ya lugha mbili zinazofanana, yaani lugha nasaba na zinazoshabihiana kiutamaduni. Naye Jilala (2021) aligundua kuwa katika mbinu za tafsiri zinazotumika katika uundaji wa istilahi za sayansi na teknolojia kuna mbinu ya tafsiri sisisi na utohozi.

Ila matokeo ya tafiti zao yana ufanano na utafauti na matokeo ya utafiti huu .Kwanza wanaisimu wote wanakubaliana kwamba katika matumizi ya mbinu hii, mfasiri hana nafasi kubwa ya kufuata kanuni za kiisimu za LL. Pili, kazi zao hazikuonyesha kuwa mbinu hii inaweza kuambatana na mbinu ya tafsiri kimaelezo kama ilivyodhihirika katika utafiti huu. Tafsiri kimaelezo ilipoambatanishwa na mbinu ya tafsiri sisisi na tohozi inanufaisha watumiaji wa KT kwa kupata ulewa zaidi wa istilahi zilizotafsiriwa.

**4.3.4. Tafsiri Sisisi na Ufupishaji**

Kupitia matokeo ya utafiti huu imebaini kuwa, mbinu ya tafsiri sisi imetumika kuunda istilahi za LL ya *KT* kisha kulipa kifupisho chake katika mchakato wa kuunda istilahi za uwanja wa magonjwa. Kupitia mifano itakayowasilisha chini ya aya hii, utafiti huu utadhihirisha jinsi waliounda istilahi za LL ya *KT* walivyoitumia mbinu ya tafsiri sisisi na kuiambatanisha ufupishaji wa maneno.

**Jedwali Na.4.8. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Sisisi na Ufupishaji**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| A.P.H (ante partum haemorrhage) | Kutokwa damu kabla ya kuzaa (K.D.K.K) apiechi | hali ya hatari ya kutoka damu ukeni wakati wa ujauzito, aghalabu kutokana na kuachia kwa plasenta. |
| AIDS (Acquired immunodeficiency syndrome) | UKIMWI (Upungufu wa Kinga Mwilini) ya kupata (SIUKIKU-si ya kurithi) | ugonjwa unaosababishwa na virusi vya ukimwi ambao huenezwa kwa ngono, ulawiti, damu (kutiwa damu, sindano chafu, vifaa visivyotakaswa) na uambukizo wa mtoto kutoka kwamama wakati wa ujauzito. Dalili za ukimwi ni pamoja na uambukizo usio mna dalili (hugundulika tu kwa kupima damu, mkojo n.k.) au dalili za magonjwa mbalimbali yanayotokana na kuharibiwa kwa mfumo wa kinga ya mwili; k.m. tiibi, magonjwa ya ngozi, homa za mara kwa mara, uchovu wa mwili na ukondefu. |

**Chanzo**: ***KT***, ***Septemba, 2024***

Jedwali Na. 4.8 hapo juu inawasilisha data zinazodhihirisha matumizi ya tafsiri sisisi na ufupishaji. Data hizi zilionesha kuwa uundaji wa istilahi ulifanyika kwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi na ufupishaji kwa wakati mmoja katika mchakato wa kuunda istilahi za magonjwa. Aidha , mbinu hiyo imeambatanishwa na mbinu ya tafsiri kimaelezo.

Kazi tangulizi zilizoshughulikia kutathmini na kufafanua mbinu za tafsiri zinazotumiwa katika uundaji wa istilahi kuna moja inayo ufananisho na matokeo ya utafiti haya. Jilala (2021) ndiye aliweza kuvumbua mbinu hii.Ila, utaofauti uliyopo kati ya ugunduzi wake na ugunduzi wa utafiti huu ni kwamba hapa mbinu hii imeambatanishwa na mbinu ya tafsiri kimaelezo mahali pote ilipotumiwa na waundaji wa istilahi za LL ya KT. Rubanza (1996) anaeleza kuwa baadhi ya majina ya maeneno katika lugha nyingine za dunia hutokana na ufupishaji wa maneno yanavyotumiwa kwa pamoja kwa kutumia herufi au silabi za mwanzo

tu za maneno hayo. Njia hii ameiita Akronimu. Miongoni mwa mifano mwanachuo huyo aliyotoa kuna UKIMWI: ‘‘Ukosefu wa Kinga Mwilini’’.

Mfano huo ni sawa na mfano umetolewa katika jedwili lililopo hapo juu. Isitoshe, mbinu ya ufupishaji si mbinu ya tafsiri ila inaorodheshwa miongoni mwa mbinu za uundaji istilahi zilizopendekezwa na na taaluma ya istilahi. Naye Matinde (2012) anaeleza kuwa ufupishaji ni mbinu ambayo hutokana na kitenzi ‘fupisha’ chenye maana ya kufanya kitu kiwe kifupi au kupunguza urefu wa kitu. Mtazamo wa Matinde ( 2012) anapodai tafsiri kuwa ni mbinu ya kuunda maneno ambapo maneno au vifungu katika LC yanafasiriwa katika LL kwa kuzingatia muundo wa lugha pokezi unawiana na mtazamo wa Jilala (2021). Kwa kupendekeza matumizi ya mbinu ya tafsiri sisisi kisha mbinu ya ufupisho na kuziambatanisha ya tafsiri kimaelezo,mbinu ya ufupishaji haipotoshi mbinu za tafsiri zilizotumia pamoja.

### 4.3.5. Tafsiri Sisisi

Utafiti huu ulibaini kuwa katika uundaji wa istilahi za uwanja wa magonjwa za LL ya *KT* waundaji wa istilahi hutumia mbinu ya tafsiri sisisi. Tafsiri sisisi imetumika kwa kuhamisha maana ya LC kwenda LL kwa kutafsiri neno kwa neno lakini kwa kuzingatia muundo wa LL. Waundaji wa istilahi za LL ya KT walitumia tafsiri sisisi yaani tafsiri ya moja kwa moja ya neno la LC kwenda LL pamoja na mbinu ya kueleza istilahi yaani kuifafanua. Matumizi ya mbinu hii yanadhihirika katika mifano iliyowasilishwa hapo chini.

**Jedwali Na.4.9. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Sisisi**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Tafsiri ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| alveolar abscess | jipu la mzizi wa jino | mkusanyiko wa usaha chini ya mzizi wa jino. |
| anticoagulant. | kizuia kuganda | kemikali ambayo huzuia kuganda kwa damu |
| antifebrile | kituliza homa | dawa ambayo hushusha homa |
| dedentition | kung'oka meno | kutoka kwa meno hasa kutokana na ugonjwa. |
| gastric ulcer (s) adhesiotomy | ki/vidonda cha/vya tumbouondoaji wa mshikano | kidonda au vidonda kadhaa vya membreni ute ya tumbo. operesheni ya kuondoa sehemu ambazo pamoja |
| gastroparalysis acoumeter | kupooza kwa tumbokipima sauti | hali ya tumbo kushindwa kufanya kazi.kifaa cha kupimia usikivu. |
| occupational diseases | magonjwa ya mazingira, magonjwa ya kikazi | magonjwa yanayotokana na aina ya kazi aifanyayo mtu. |
| palmar abscess | jipu la kiganja | jipu katika peritoniumu ya pelvisi. |
| palmar abscess aerobiology | jipu la kiganjabiolojia hewa | tanzu ya biolojia inayohusu viumbe vilivyomo hewani. |
| post-haemorrhage | utokaji damu kwa mara nyingine tena | |
| sea sickness | kigegezi cha baharini | hali ya kichefuchefu, kutapika, kizunguzungu na uchovu wa mwili ambao huwapata baadhi ya watu wanaposafiri na chombo cha majini kama meli. |
| sexual diseases | magonjwa ya kujamiiana, magonjwa ya ngono kujamiiana | magonjwa yanayoenezwa aghalabu kwa njia ya |
| venereal diseases radiobiolgy | magonjwa ya ngono, magonjwa ya kujamiiana<br><br>biolojia miale | magonjwa ambayo huambukiza kwa njia ya ngono tanzu ya elimu inayohusu athari ya miale ya nishati kubwa katika viumbe hai. |

***Chanzo: Kamusi ya Septemba, 2024***

Jedwali Na.4.9 linawasilisha data zinazodhihirisha matumizi ya tafsiri sisisi katika mchakato wa uundaji wa istilahi za uwanja wa magonjwa za LL ya *KT*. Mara nyingi, mbinu hii iliambatana na mbinu ya tafsiri kimaelezo. Ila kuna wakati ambapo waundaji wa istilahi walitumia mbinu ya tafsiri sisisi tu. Km, wakati wa kutafsiri itsilahi‘‘palmar abscess’’ kama‘‘ jipu la kiganja‘‘ kumetumia mbinu ya Tafsiri Sisisi. Ilhali walipotafsiri jipu istilahi‘‘acoumeter’’ kama‘‘kipima sauti: kifaa cha kupimia usikivu’’, inadhihirika kwamba mbinu ya tafsiri sisisi imeambatanishwa na mbinu ya tafsiri kimaelezo au tafsiri maana kwa kauli nyingine.

Kazi tangulizi za kazi hii zinaibua matumizi ya mbinu ya tafsiri sisisi. Malangwa (1992) alifasili dhana ‘‘sisisi’’kama namna ya ukopaji ambapo neno au kirai kutoka lugha moja huhamishwa hadi lugha nyingine kwa kufuata kanuni za orodha ya maneno ya LL. Mwaro-Were ( 2000) aligundua kuwa katika harakati zao za kuendeleza leksikoni ya Kiswahili, watunzi wa istilahi wamekuwa wakitumia pia utaratibu wa ‘‘kaleki’’ au tafsiri sisisi. Ingawa watafiti hao walipendekeza uhamishaji wa neno au mofimu kwa mofimu ni dhahiri kwamba watunzi wa istilahi za LL ya *KT* waliitumia mbinu husika kwa kuheshimu mpangilio wa maneno wa LL. Mpangilio wa istilahi zinazotokana na tafsiri sisisi ulibadilishwa ili ulingane na kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lugha pokezi yaani Kiswahili. Isitoshe, watunzi wa KT walipendekeza kuunganisha mbinu ya tafsiri tisisi na mbinu ya tafsiri kimaelezo ambayo tunaangazia hapo chini matumizi yake katika mchakato wa kutunga *KT* kupitia uundaji wa istilahi za LL ya kamusi hiyo.

### 4.3.6. Tafsiri Kimaelezo

Utafiti huu ulibaini kuwa, katika uundaji wa istilahi za uwanja wa magonjwa katika LL ya KT, waundaji wa istilahi walitumia mbinu ya tafsiri kimaelezo. Data za utafiti wetu zilidhirisha kuwa baadhi ya istilahi za LL ya *KT* yaani Kiswahili zimetokana na matumizi ya mbinu hii katika mchakato wa kuunda istilahi hizo. Jedwali Na.4.8 linatuelezea matokeo haya.

**Jedwali Na.4.10. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Kimaelezo**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Tafsiri ya kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** |
|---|---|---|
| aphtous ulcers. | | vidonda vya kinywani ambavyo hurudiarudia |
| autoeroticism | mapenzi nafsia | kujiridhisha kingono kwa mtu kujifanyia vitendo fulani yeye mwenyewe |
| cystoparalysis | kupooza kwa kibofu cha mkojo | hali ya kukosekana kwa mawasiliano ya neva katika kibofu cha mkojo |
| dedentition | kung'oka meno | kutoka kwa meno hasa kutokana na ugonjwa. |
| fulgurant | | maumivu makali sana na ya ghafla, huja kama vile umeme wa radi |
| sursanure | | kidonda ambacho kimepona kwa juu lakini kwa ndani bado. |
| whiteleg | | mguu uliovimba kutokana na thrombosisi ya vena ya femora. |

***Chanzo: KT, Septemba, 2024***

Data zilizowasilishwa katika jedwali Na. 4.10 zinaonyesha mifano ya matumizi ya mbinu ya tafsiri kimaelezo katika uundaji wa istilahi za *KT*. Mbinu hiyo ilitumiwa peke yake kama katika kutafsiri kidahizo "cystoparalysis" ambacho kilielezewa kama "kupooza kwa kibofu cha mkojo". Isitoshe matumizi ya mbinu ya tafsiri kimaelezo ilitumiwa baada ya kuwasilisha kisawe kama katika "dedentition " na kisawe chake "kung'oka meno " kisha kufafanua kisawe hicho kama "kutoka kwa meno hasa kutokana na ugonjwa". Pia, watunzi wa *KT* walianza kuwasilisha kisawe na kukiambatanisha na mbinu nyingine kama vile matumizi ya kisawe, utohozi na tafsiri sisisi, kama katika "autoeroticism " na tafsiri yake "mapenzi nafsia" zilizoambatanishwa na mbinu ya tafsiri elezi "kujiridhisha kingono kwa mtu kujifanyia vitendo fulani yeye mwenyewe " ili kuwawezesha watumiaji wa *KT* kupata uelewa zaidi wa maana za istilahi katika LL.

Kazi tangulizi za kazi hii zinadhihirisha uhusiano kati matokeo ya utafiti huu nazo. Singoei (2020) aliona kuwa mchakato wa mbinu hio unachunguza kama istilahi inatafsiriwa kwa kutumia ufafanuzi wa umbo au uamilifu wake. Hivyo, huweza kuchukuliwa kama namna ya kufafanua dhana kwa kuweka maelezo au mifano ili ipate kueleweka zaidi kwa watumizi wa wake kupitia *KT*. Isitoshe, Rehema (2020) alieleza kuwa ufafanuzi ni utoaji wa maelezo ya ziada au maelezo mbadala ili kueleweshaau kusisitizia. Maoni ya wanazuoni hao yana ufanano mkubwa na matokeo ya utafiti huu.Watunzi wa *KT* kupitia uundaji wa istilahi za LL,walitumia mbinu ya tafsiri kimaelezo ili watumiaji wa *KT* wapate uelewa zaidi wa istilahi zilitowasilishwa katika LL. Isitoshe,watunzi wa *KT* kwa kuunda istilahi za LL yake kuna wakati walianza kuwasilisha visawe kisha kuviambatanisha na mbinu ya tafsiri kimaelezo. Wakati mwingine waliwasilisha maelezo moja kwa moja. Japo wanazuoni hao wanakubaliana kuhusu mchakato wa matumizi ya mbinu hii, hawakueleza kwamba huenda ikaambatanishwa na mbinu zingine kama ilivyodhihirika katika mifano iliyowasilishwa kupitia jedwali la hapo juu.

**4.3.7. Tafsiri Sisisi Fungamanifu**

Katika tafsiri sisisi maneno hutafsiriwa yakiwa pwekepweke kwa kuzingatia maana zake za kimsingi katika lugha chanzi bila kujali sana muktadha, Omari (2013). Aidha , kama anyoeleza Mwansoko (1996) tafsiri hii hufuata mfumo wa sarufi, hususan sintaksia ya LL. Kwa mujibu wa TUKI ( 2013) neno au kivumishi ‘‘fungamanifu’’ linatoka katika kitenzi ‘‘ fungamana’’ na maana yake ni ‘‘shirikiana katika mambo fulani’’. Maoni haya yanamanisha kuwa istilahi zilizotafsiriwa pwekepweke zilishirikiana kuundia istilahi moja. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha mifano ya matumizi ya mbinu ya tafsiri sisisi fungamanifu za istilahi ya LL kutoka *KT* kama inavyoptikana katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali Na.4.11. Istilahi Kutokana na Mbinu ya Tafsiri Sisisi Fungamanifu**

| **Istilahi ya Kiingereza** | **Istilahi ya Kiswahili** | **Maana yake kwa Mjibu wa *KT*** | **Ufungamanifu** |
|---|---|---|---|
| acephalocardia | akefalikadia | hitilafu ya kuzaliwa ya kukosekana kwa kichwa na moyo. | akefali+ kadia |
| cancerophobia | kansafobia | woga wa kinurotiki wa kupatwa na | kansa+ fobia |
| cacotrophy | utapiamlo | maradhi ya mwili yanayotokana na lishe duni au lishe ya kupita kiasi. | utapia+mlo |
| enterorrhagia | enterorajia | kuvuja kwa damu katika utumbo | entero+rajia |
| heliophilia | heliofilia | woga wa kupita kiasi wa mwanga wa jua. | helio+filia |

***Chanzo: KT, Septemba, 2024***

Jedwali hilo hapo juu linawasilisha data ambazo zinadhihirisha kuwa mbinu ya tafsiri sisisi fungamani imetumika uunaji wa istilahi za LL ya *KT*. Mbinu hii imeambatana na matumizi ya uambatishaji wenye kufungamanisha maneno na kufanya neno kuwa moja. Isitoshe, mbinu hii imeambatanishwa na mbinu ya tafsiri kimaelezo katika mifano yote iliyowasilishwa kutoka nyuga zote zilizoteuliwa. Ifahamishwe kwamba katika mchakato wa matumizi ya mbinu hii waundaji wa istilahi za LL ya KT walitumia pia mbinu ya tafsiri tohozi na mbinu tafsiri kwa Kisawe kiamilifu. Matumizi ya mbinu hizo yanadhihirika katika mfano kama " acephalocardia" imetafsiriwa kama " akefalikadia: hitilafu ya kuzaliwa ya kukosekana kwa kichwa na moyo". Hasa katika mfano " heliophilia " iliyotafsiriwa kama "heliofilia, woga wa kupita kiasi wa mwanga wa jua ". Ukichunguza tafsiri hizo utaona kuwa maneno mawili yameambatishwa ili kuunda neno moja kama kisawe cha neno la LL.

Kazi tangulizi za hii zinadhihirisha ufanano na matokeo ya utafiti huu kuhusu matumizi ya mbinu ya tafsiri sisisi Fungmanifu. Kwanza, Jilala ( 2021) amabaye pia ni mwanzilishi wa mbinu hii ya tafsiri sisisi fungamanifu aliiangazia. Katika mchakato wa tafsiri sisisi fungamanifu istilahi mbili zinaambatanishwa ili kuunda istilahi moja katika LL ya *KT*. Kazi nyingine iliyoshughulikia mbinu ya tafsiri sisisi fungamanifu ni kazi ya Mwaro –Were (2000). Mwanazuoni huyu alipendekeza kuwa stilahi mbili au tatu zinaweza kuunganishwa na kuunda istilahi moja, kama mfano huu unavyoonyesha, “binarism” na tafsiri yake “uwiliwili” kutoka “uwili uwili”.

Kazi tangulizi hizo mbili zinadhihirisha utofauti na kazi hii.Wanazuoni hao wawili hawakuambatanisha mbinu ya tafsiri sisisi fungamanifu na mbinu ya tafsiri kimaelezo kama walivyoziambatanisha watunzi wa *KT* katika mchakato wa kuinduia istilahi za LL .

Katika sehemu hii kulitathminiwa mbinu mbalimbali za uundaji istilahi zilizotumiwa na watunzi wa *KT* katika mchakato wa kuiundia istilahi zake za LL yaani Kiswahili hususan uwanja wa magonjwa. Uchambuzi wa data ulidhihirisha kwamba mbinu ya ukopaji kamili na usio kamili, tafsiri , tafsiri sisisi, tafsiri kwa usawe, tafsiri kimaelezo zilitumiwa,ufupishaji, ufungamanifu zilitumiwa Aidha, uchambuzi wa data ulidhihirisha kuwa mbinu za tafsiri zilizotumiwa zilitumiwa na watunzi wa *KT* kwa kushirikiana na mbinu za uundaji wa istilahi zilizopendekezwa na wanaistilahi. Kuliwekwa wazi kwamba ni nadra kupata mbinu moja imetumika pekee. Bila shaka, uteuzi wa mbinu za uundaji wa istilahi na mbinu za tafsiri ulifanywa kimakusudi. Kwa hiyo, katika kipengele kifuatacho tutajadili kwa kina sababu za matumizi ya mbinu zilizotumia na watunzi wa *KT* katika mchakato wa kuundia istilahi za LL ya *KT* yaani Kiswahili kutoka LC yaani Kiingereza kwa juzingatia uwanja wa magonjwa.

## 4.4. Sababu za Matumizi ya Mbinu Husika katika Mchakato wa Kuunda Istilahi za LL ya *KT*

Uchambuzi wa data zilizowasilishwa katika utafiti huu ulidhihirisha matumizi ya mbinu mbalimbali za uundaji wa istilahi pakiwemo mbinu tafsiri zilizotumiwa na watunzi wa istilahi za LL ya *KT* katika mchakato wa kuunda istilahi za uwanja wa magojwa. Kwa jumla kuliwekwa bayana mbinu mbinu ya ukopaji moja kwa moja, mbinu utohozi, mbinu ya ufupisho, mbinu ya tafsiri kwa usawe, mbinu ya tafsiri sisi, mbinu ya tafsiri maana au tafsiri elezi zilitumika. Mbinu hizo zilitumika ama kipekee ama kwa kuambatanishwa na mbinu zingine za tafsiri. Hivyo, kuna wakati ambapo mbinu ya tafsiri kwa kisawe kamilifu ilitumika ikiwa pamoja na mbinu ya tafsiri ya maana yaani tafsiri kimaelezo. Mbinu hiyo ya tafsiri ya maana nayo iliibuliwa ikiwa imetumiwa peke yake au ikishirikiana na mbinu zingine za tafsiri.

Matumizi ya mbinu hizo katika mchakato wa kuunda istilahi za LL ya *KT* bila shaka hawazikutumiwa bila kusudi lolote. Kwa hiyo, lengo la kipengele hiki ni kuwasilisha sababu za matumizi ya mbinu zilizotathminiwa kupitia uchambuzi wa data zilizokuwa zimekusanywa kutoka katika *KT*.

### 4.4.1. Sababu za Matumizi ya Mbinu ya Kukopa

Maneno katika lugha hayakopwi tu kiholela bali kuna sababu mbalimbali zinazochochea ukopaji huo, Malangwa (2021). Baadhi ya sababu hizo zinafafanuliwa katika aya zinazofuata. Kamusi ya TUKI (2019) inaonesha kuwa lugha ya Kiswahili imekopa msamiati kutoka lugha za kigeni zaidi ya 13. Wazungumzaji wa lugha wana kasumba ya kukopa msamiati kutoka lugha za kigeni kila wanapotagusana na jamii hizo hata kama msamiati unaoelezea dhana hiyo ulikwisha kukopwa kutoka lugha zingine. Akida na wenzake (1971) wanasisitiza kuwa msamiati wa Kiswahili upanuliwe kwa kukopa msamiati wa kigeni kwa madai kuwa hakuna lugha ulimwenguni isiyowahi kukopa msamiati wa kigeni wala inayojitosheleza kimsamiati.

Naye Likhako (1991) anaunga mkono Akida na kwa kuelezea kuwa sababu ya ukukopa inatokana na sifa ya lugha zote na kila lugha hukopa kwani lugha nyingi duniani zimekopa msamiati kutokana na lugha zingine. Kiango (1999) anaeleza kuwa ukopaji wa maneno si suala la lugha fulani maalumu tu, bali ni mbinu ya kukuza lugha inayotumiwa na lugha zote duniani, Kiswahili kikiwamo. Aidha, kama anavyoeleza Oyare Mboya( 2016) lugha mbili zinapoingiliana kimatumizi, huwa ni kawaida kuathiriana. Kuathiriana kule kunaweza kuleta mabadiliko katika lugha zilizohusika. Hata hivyo, athari nyingi hutokea katika upande wa msamiati ambapo wazungumzaji wa lugha hizo wanaweza kukopana msamiati.Sababu nyingine iliyochochea matumizi ya ukopaji kwa kutohoa yaani kufanyiwa marekebisho istilahi ili ilingane na tabia na muundo wa maneno ya lugha pokezi ili uafikiane na muundo wa lugha pokezi yaani Kiswahili, kifonolojia na kimofolojia.Ikumbushwe kuwa kuna sauti za kiingerezaambazo hazipo katika sauti thelatini za kiswahili. Kwa mujibu wa TUKI( 2012) sauti za kiswahili hizo zisizopatikana katika Kiswahili ni q na x. Kwa hiyo, baadhi ya istilahi zilizokopwa sharti zifanyiwe uswahilishaji ili ziwiane na muundo wa maneno unaokubalika katika lugha ya Kiswahili.Kwa mujibu wa Mwaro- Were( 2000) ukopaji unatokana pia na kutokuwepo kwa msamiati asili wa kurejelea dhana mpya inayoingia katika LL. Mbinu ya ukopaji inasaidia katika kuziba pengo la ukosefu wa visawe vya maneno au istilahi zisizopatikana katika kamusi mbalimbali. Kwa mujibu wa Malangwa na wenzake ( 2016) hali ya kutokuwa na usawe baina ya lugha chanzi na lugha lengwa husababishwa na teknolojia ya kisasa inayoingiza maneno na dhana ngeni kwa kasi kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Hali hii hutokea kwa sababu ya kuibuka kwa dhana mpya katika jamii za ulimwengu kutokana na ukuaji wa maendeleo kiteknolojia, kiuchumi, kisiasa na kijamii , iribemwangi na mwenzake ( 2011).

Halikadhalika, vipengele vya kitamaduni na majina ya pekee husababisha ukopaji wa moja kwa moja (kuhamisha neno la LC vile lilivyo kwena LL) .Pia, ukopaji kamili umefanya kwa

sababu istilahi hizo hazina utata wa kifonolojia na kimofolojia katika LL yaani lugha ya kiswahili. Katika mchakato wa kutumia mbinu ya utohozi, ilidhihirika kuwa nomino za pekee hazikutoholewa yaani zilihamishwa bila kufanyiwa marekebisho yoyote. Mosota ( 2016) akitoa sababu amesema kuwa majina mageni ambayo yameibuka kwa sababu ya teknolojia, inabidi maneno hayo yathamishwe katika bila kutoholewa ili kukidhi mahitaji mapya yanayozuka. Baadhi ya istilahi zilizohamisha bila kufaniwa ruwaza zinahusu majina ya wataalamu wa tiba ambo walitafiti magonjwa na kuvumbua madawa yakuyakomesha au kuapunguzia madhara. Wakati mwingine**.** Nao ukopaji kamili umefanya kwa sababu istilahi hizo hazina utata wa kifonolojia na kimofolojia katika LL yaani lugha ya kiswahili. Pili, inasaidia kuokoa muda wa kuwasilisha kazi ya uundaji wa istilahi .Vinay na Darbelnet( 2004) wametoa sababu za matumizi ya mbinu ya wa moja kwa moja kama huu wa kuhamisha majina vile yalivyokuwa katika LC hutumiwa kwa sababu zifuatazo: kutokuwepo na visawe baina ya LC na LL, kuwepo kwa dhana geni za kiteknolojia, mwandishi kuamua kusawiri ladha ya utamaduni wa lugha chanzi na kuleta athari ya kimtindo.

Kwa ujumla kutokana na kuathiriana kwa lugha,ukopaji lazima utokee. Hii ni kumaanisha kuwa lugha sharti iwe na mikakati teule ambayo itatumika ili kubuni msamiati mpya wa kurejelea dhana kama hizo. Njia mojawapo ya kuunda maneno mapya ni kukopa na kutohoa. Kwa mujibu wa za sababu zilizotolewa na watafiti mbali mbali waliowasilisha hapo juu, ukopaji wa maneno huandamana na ugeuzaji wa maneno ili yaweze kufuata kanuni za kifonolojia na kimofolojia za lugha pokezi. Ugeuzaji huu ndio huitwa utohozi.Ukopaji nao wa moja kwa moja hutokea wakati istilahi inoingizwa katika LL kutoka LC halina utata wa kimatamshi na kimaandishi, yaani inawiana na kanuni za kifonolojia na kimofolojia zake. Pia tuliona kuwa kuna istilahi zinazohusiana na majina ya pekee zinakopa bila kufanyia marekebisho yoyote.

Utafiti ulidhihirisha kuwa naneno hukopwa katika lugha kutokana na sababu mbalimbali. Mosi, ni mahitaji ya msamiati katika lugha kwa ajili ya kuelezea dhana au kitu ambacho hakikuwa kinajulikana katika jamii ya lugha hiyo. Pili, ukopaji unaweza kutokana na mwingiliano wa nguvu za kisiasa ambazo husababisha pia jamii kutumia maneno ya lugha tawala, na hivyo, kuongeza msamiati katika lugha lengwa Robins (1980) na Chuwa (1988). Kiingereza kilikuwa lugha tawala katiki nchi mbalimabali za Afrika Mashariki zilizokuwa china ya ukoloni wa Uingereza kwa miongo kadhaa. Hali hii isababisha ukopaji wa maneno ya kiswahili ili kukudhi haja ya mawasiliano.

### 4.4.2. Sababu za Matumizi ya Mbinu ya Tafsiri ya Maana au Mbinu ya Tafsiri Kimaelezo

Mbinu za uundaji wa istilahi zilizotumiwa ziliambatanishwa na mbinu ya tafsiri maana au mbinu ya tafsiri kimaelezo. Mbinu hizo hazikutumiwa bila sababu .Sababu ya kwanza iliyochochea matumizi ya mbinu hio inapatikana katika Dibaji ya *KT* ( 2003) yenyewe**.** Kwa mujibu wa Kiango ( tizama Dibaji ya KT kwa maelezo zaidi) ambaye alikuwa Kaimu Mkurugenzi kutumia mbinu hio sababu hizo anaziangazia katika mihimili mbalimbali **.** Mosi ni tangu wahenga na wahenga, Kiswahili hakikuwa kimepewa nafasi kubwa ya kukitumia katika taaluma ya uganga, uhaba wa msamiati na istilahi za fani hii umejitokeza wakati wa kutunga kamusi hii ya tiba. Pili**,** lugha isipopewa nafasi kubwa ya matumizi katika nyanja mbalimbali, msamiati wake unakuwa finyu. Tatu, Kamusi hii ya tiba ni ya Kiingereza Kiswahili. Kwa maana ya kwamba kamusi imeanza na orodha ya istilahi katika Kiingereza kisha kutafuta visawe vyake katika Kiswahili. Ziko baadhi ya istilahi za uganga za Kiingereza zimepata visawe vyake katika Kiswahili. Lakini kuna baadhi hazikuwa na visawe vyake. Kwa zile istilahi istilahi wakati ule wa kutunga *KT* hazikuwa na visawe, miongoni mwa mbinu zilizotumiwa kuna mbinu ya tatu ambayo ni kutoa maelezo tu ya dhana husika kwa Kiswahili fasaha.

Kwa ufupi,mbinu hiyo ilisaidia kujaribu kutoa uelewa zaidi wa istilahi kwa msomaji wa istilahi au wa kazi ya tafsiri kwani Kiswahili ,kama lugha zingine, ina uhuru na uwezo wa kueleza dhana zilizomo katika lugha zingine, kwa hiyo anatumia mbinu hizo mbili.

### 4.4.3. Sababu za Matumizi ya Mbinu Tafsiri kwaVisawe

Katika data zililowasilishwa kumedhihirika istilahi ambazo zilitafsiriwa kwa kutumia mbinu ya tafsiri kwa visawe.

sababu mbalimbali zinazochochea matumizi ya mbinu ya tafsiri kwa visawe. Kwanza, Jilala ( 2021) anaeleza kwamba kazi muhimu kwa wafasiri ni kusaka visawe katika kamusi za istilahi au kwenye wavuti mbalimbali. Naye Nkwera (1978) anaelezea kuwa mbinu hiyo inawasaidia kuwasilisha kazi yao kulingana na muda uliokubaliwa. Sababu nyingine ni kwamba *KT* imeanza na orodha ya istilahi katika Kiingereza kisha kutafuta visawe vyake katika Kiswahili, TUKI( 2003). Kila wakati wanapofanya kazi ya tafsiri wanahifadhi istilahi na visawe vyake katika benki ya istilahi wanazojiunda, wanapopata istilahi na kisawe kinacholingana kimuktadha wanazitumia mara moja.sababu nyingine ya utumiaji wa mbinu ya tafsiri kwa visawe ,Jilala( 2024). Kwa mujibu wake, lugha nyingi duniani zilitajirika kwa kuwa zilihusika na tafsiri tangu enzi za kale pakiwemo lugha ya Kiingereza na ya Kiswahili. Kwa hiyo, wafasiri wana uwezo wa kulinganisha istili kimaana na kuteua istilahi yenye maana sawa kutoka lugha ya Kiswahili au lugha nyingine za Kibantu. Isitoshe, istilahi hizo huwa zinatumiwa na taasisi za kimataifa na kuzipatia mashiko na ukubalifu wa kimataifa.

### 4.4.4. Sababu za Matumizi ya Mbinu ya Tafsiri Sisisi

Watalaamu mbalimbali walizungumzia sababu zilizochochea matumizi ya Mbinu ya Tafsiri Sisisi. Vinay na Derbelnet (2004) wanaeleza kwamba, tafsiri sisisi inahusisha tafsiri ya moja kwa moja ya neno la lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Katika matumizi ya mkakati huu, mfasiri hana nafasi kubwa ya kufuata kanuni za kiisimu za lugha lengwa. Mfasiri hutafsiri

maneno kwa kuzingatia maana zake za kimsingi katika lugha chanzi. Sababu hii inathibitisha kuwa matumizi ya mbinu hii yanarahisisha na kuharakisha kazi ya uundaji wa istilahi.

Kwa ufupi kulipatikana sababu mbalimbali za mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa na watunzi wa istilahi za LL ya KT. Mbinu ya tasfiri mkopo inasaidia katika kuziba pengo la ukosefu wa visawe vya maneno au istilahi zisizopatikana katika kamusi mbalimbali na benki za istilahi wanazojitungia wa kufanya kazi ya utafsiri. Katika mchakato wa uundaji istilahi utohozi inatumika kwa kuwa husaidia kurekebisha maneno waliyokopa ili yaafikiane na muundo wa LL kifonolojia na kimofolojia. Istilahi za Kiingereza zilizokopwa zinaandikwa upwa kwa kutumia muundo wa Kiswahili ili zisomeke kwa Kiswahili. Mbinu ya tafsiri kimaelezo inatumika kwani ni njia mwafaka dhana husika kwa Kiswahili fasaha na kuziba pengo la ukosefu wa visawe katika LL. Sababu kubwa ya matumizi ya mbinu ya tafsiri kwa usawe ni kwamba kazi muhimu kwao kama wafasiri ni kusaka visawe katika kamusi za istilahi au kwenye wavuti mbalimbali. Wakati kumekosekana visawe ndipo hatua ya kutumia mbinu zingine za tafsiri huchukulia. Naye mbinu ya tafsiri sisisi inatumiwa kuwani inasaidia katika kuzingatia muundo wa istilahi na dhima yake katika LL.

*KT* ni ya Kiingereza Kiswahili. Bila shaka, imeanza na orodha ya istilahi katika Kiingereza kisha kutafutiwa istilahi katika Kiswahili. Hivyo, ni wazi kuwa mbinu ya tafsiri kwa usawe ilitumiwa na watunzi wa *KT*. Kwa kufuata mkakati huo, ziko baadhi ya istilahi za magonjwa za Kiingereza zilizopata visawe vyake katika Kiswahili au katika lugha zingine za Kibantu kwa kukopa maneno ambayo anaweza kuelezea dhana zinazokusudiwa. Mara kwa mara, mbinu za tafsiri zilitumika pamoja. Ama mbinu ya tafsiri mkopo iliambatanishwa na mbinu ya tafsiri kwa usawe, ama kwa kuiambatanishwa na mbinu ya tafsiri kimaelezo. Isitoshe, mbinu ya tafsiri sisisi ilitumika ikiunganishwa na mbinu ya tafsiri kimaelezo. Hiyo mbinu ya tafsiri sisisi iliambatanishwa pia na mbinu ya kuunganisha istilahi mbili pamoja. Ifahamike kwamba Kamusi hii ni ya uwanja wa tiba na uuguzi. Kwa hiyo sio kamusi kwa ajili ya watumiaji wa

kawaida wa lugha ya Kiswahili. Kuambatanisha mbinu mbalimbali kulikuwa na lengo la kuongeza uelewa zaidi wa istilahi.

Mbinu za uundaji zilizowekwa hadharani na utafiti huu ni ukweli. Pia, watunzi wa KT nao walizitumia katika mchakato wa kuundia LL ya *KT* istilahi.Wakati kunakosekana kisawe badala ya kukopa istilahi kwa kuihamisha kama ilivyo, mbinu ya tafsiri kimaelezo inapendekeza ili imwezeshe mfasiri kuwalisisha uelewa wa kutosha. Kukopa ni mojawapo ya mbinu ya kiisimu ambayo hutumiwa na lugha zote ulimwenguni kuunda istilahi na maneno mapya ili kukidhi mawasiliano katika miktadha tofauti. Mbinu ya tafsiri sisisi inatumiwa ili miundo ya lugha iheshimiwe. Pia, ni nadra kutumia mbinu moja wakati wa kutafsiri istilahi. Kwa zile zilizotoa maana wazi, kuambatanisha na maelezo ni jambo muhimu sana. Mbinu hiyo inasaidia kupata uelewa zaidi na kujiepusha kupotosha maana ya istilahi kutoka LC. Tafsiri inatumika kama daraja wakati wa hatua za kuunda istilahi za kiufundi kama vile Tiba. Baadhi ya stilahi ni mapya katika jamii na zinahitaji tafsiri yake ili kupata maana za maneno hayo, dhima zake na asili yake ili kuweza kuyatafutia istilahi katika LL. Utafiti huu umeonyesha kuwa kipindi cha uundaji wa istilahi, tafsiri haiwezi kujitenga, mbinu za tafsiri hutumika katika kuundia istilahi za ya LC katika LL.

### 4.5. Uhusiano baina ya Matokeo na Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya UMA ya Krippendorff (2004). Kama ilivyoelezwa awali, uchanganuzi wa maudhui umemsaidia mtafiti kusoma *KT* na kuchambua maudhui yanayohusiana na uwanja ulioteuliwa kuunda data ili kumwezesha kutathmini mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa na wataalamu kuunda istilahi za KT. Baadaye kulibainishwa sababu ya matumizi ya mbinu zilizoibuliwa. Katika mchakato wa mbinu hizo, kuligundulika makundi makubwa matano ya mbinu ya ukopaji kamili au uhamishaji, utohozi, tafsiri kwa visawe, tafsiri sisisi na tafsiri kimaelezo, ukatizaji.

Hivyo, Nadharia hii ilikuwa mwongozo thabiti uliomwezesha mtafiti kupata majibu ya maswali ya utafiti huu na hivyo kukamilisha malengo yake na matokeo ya utafiti huu yenyewe yanadhihirisha uwiano wake na nadharia hii.

Nadharia ya Istilahi za Kisayansi( NIK) iliyowasilishwa na Kiingi (1992) na kuendelezwa na Mwaro(1993/2000) pia ilitumiwa .Nadharia hii inasisitiza ya kwamba katika ufufuaji ama uundaji wa msamiati ni lazima muundaji azingatie vigezo hivi vinane, hivyo inatuongoza katika kukubali au kukataa msamiati fulani wa Kiswahi1i. Istilahi zilizoundwa zilitoshezeza sifa ya kwanza muhimu kwani istilahi za LL ya KT hazina utata wa kimaana .Wakati utata ulipokaribia kutokea, tafsiri kimaelezo ilitumika na kusadia kufanikisha uelewa zaidi. Kigezo cha pili kilizingatiwa kwa kuunda istilahizisizo na maneno mengi na marefu. Kwa kutimiza lengo hili, mbinu ya ufupishaji ilitumika. Mfano unaoweza kutolewa na UKIMWI badala ya kutumia istilahi yenye maneno mengi Upungufu Kinga Mwilini. Istilahi zinaakisi uangavu kwa kutegemea muktadha wa matumizi yake.Fauka ya hayo istilahi zilizoundwa na watunzi wa istilahi za LL ya KT zinadhihirisha kuzingatiwa kwa heshima au adabu ya lugha ya Kiswahili kwa kujiepusha matumizi ya kisawe chenye uchafu . Istilahi zilizoundwa kwa kufuata utaratibu maalum wa kufufua msamiati kiasili na kuunda msamiati mpya wa Kiswahili. Msamiati wa Lugha za Kibantu ulitumiwa badala ya kukopa na kutohoa kila mara palipokosekana kisawe.Majopo yalifaninyika, kamusi mbalimbali zilitumiwa, mabingwa wengine walishirikisha. Kwa hiyo, istilahi zinazohusiana na uwanja wa magonjwa hazikuundwa kuundwa ama kufufuliwa vivi hivi . Mwisho, istilahi zilizoundwa zilipata Ukubalifu wa jamii - tumizi - lugha yenyewe.Tangu kuchapishwa kwa toleo la kwanza la *KT* mwaka 2003, hakuna toleo jingine limetokea kunapita miaka 23. Hio ni ishara inayothibisha kuwa Jamii za *KT* hakuoziona ubaya wowote katika ukopaji na zikubali msamiati au istilahi uliyokopwa.

### 4.6. Hitimisho

Sura hii imejishughulisha na uchambuzi wa data zilizokusanywa maktabani na kwa kupitia hojaji kuhusu mbinu za tafsiri zilizotumiwa katika uundaji wa istilahi za LL ya *KT*. Data hizi zilipatikana kwa kutumia mbinu za mapitio ya nyaraka na hojaji. Malengo ya utafiti huu yamezingatiwa katika uwasilishaji na uchambuzi wa data. Nadharia ya Uchambuzi wa Maudhui (UMA) na wa Nadharia ya Istilahi za Kisayansi( NIK) ziliongoza utafiti huu kwa njia ya maelezo na ufafanuzi kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Mkabala wa kimaelezo umehusika kwa sababu ya tukio la data za kiuthamano zilizowasilishwa kwa majedwali. Nadharia ya UMA iliyotumika katika utafiti huu imesaidia katika kuchanganua data na kutoa majibu kwa maswali ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.1. Utangulizi

Sura hii ina lengo la kutamatisha kwa kueleza kwa ufupi yaliyofanyika katika utafiti huu wenye mada ya "Tathmini ya Mbinu za Uundaji wa Istilahi za Uwanja wa Tiba: Uchunguzi Kifani wa Kamusi ya Tiba ,Toleo la 2003". Sura hii ambayo inaanzia kwa utangulizi imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni muhtasari na mapendekezo. Mwishoni, mtafiti ameikamilisha sura hii kwa hitimisho la utafiti kwa ujumla.

## 5.2. Muhtasari

### 5.2.1. Muhtasari kwa jumla

Utafiti huu umefanyika katika Chuo Kikuu cha Burundi kipatikanacho jijini Bujumbura. Utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani, na kwa kiasi kikubwa ulifanyika katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Burundi.. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa la kutathmini mbinu za uundaji wa Istilahi za *KT*. Malengo mahususi yalikuwa (1) Kubainisha istilahi zinazohusu magonjwa zilizomo katika LL ya *KT*, (2) Kufafanua mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa kuundia istilahi zinazohusu magonjwa zilizomo katika LL ya *KT* na (3) Kueleza sababu ya matumizi ya mbinu za kuundia istilahi zinazohusu magonjwa za tiba zilizomo katika LL ya *KT*.

Utafiti huu ulifanyika katika sura nne. Sura ya kwanza kabisa ilihusika na utangulizi wa utafiti huu. Katika sura hii kulijadiliwa usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti yakiwemo lengo kuu la utafiti na malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti. Sura hiyo iliweka bayana misingi ya utafiti huu.

Sura ya pili ilihusika na kazi tangulizi zilizotungwa na watafiti mbalimbali juu ya mada zinazojenga uhusiano wa karibu na utafiti huu. Maandiko yaliyofafanuliwa katika sura hii yanahusu mikakati na mbinu ambazo zimekuwa zikitumika katika utungaji wa kamusi za Kiingereza - Kiswahili katika nyanja mbalimbali na kwa kutumia mikabala na nadharia tofauti tofauti. Isitoshe, sura hiyo iliweka bayana kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu. Nadharia ya UMA iliyoasisiwa na Krippendorff (2004) na Nadharia ya Istilahi za Kisayansi( NIK) ambayo mwanzlishi wake ni Kiingi ( 1992) ilitumiwa ili kuchambua mbinu za uundaji istilahi na kufafanua sababu za matumizi ya mbinu hizo.

Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Mara baada ya utangulizi mfupi, kulijadiliwa eneo la utafiti na watoataarifa, sampuli lengwa ya watafitiwa na usampulishaji. Mbinu za kukusanyia data zilizotumika katika utafiti huu ni mbinu ya mapitio ya nyaraka ambayo kwa muktadha huu ni *KT*, pamoja na hojaji. Aidha, sura hii iliweka bayana mkabala wa uchanganuzi wa data uliotumika, yaani mkabala wa kimaelezo. Vilevile, sura hii imeonyesha maadili ya utafiti.Sura ya nne ilijikita katika uwasilishaji wa data na uchambuzi wake ambapo kwanza mbinu mbalimbali za uundaji wa istilahi za LL ya KT zilibainishwa kisha matumizi yake yaligundulika kwa kujishinikia kwa maoni ya watafiti mbalimbali waliovulia shati tafiti husiani.Sura ya tano ilishughulikia muhtasari wa utafiti, mapendekezo hitimisho.

**5. 2.2. Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Kutokana na data zilizokusanywa na kuchambuliwa, na malengo mahususi ya utafiti huu, kulibainika istilahi za LLya *KT* kwa kuzingatia uwanja wa magonjwa. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirika kutokana na malengo mahususi ya utafiti huu. Lengo la kwanza lilikuwa la kubaini istilahi za uwanja wa magonjwa kupitia LL ya *KT*. Uchunguzi wa *KT* uliweka bayana istilahi zinazohusiana na uwanja wa magonjwa ambao ndiyo data za utafiti huu.

Lengo la pili lilikuwa la kutathmini mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa katika kuundia istilahi za LL ya *KT* ambayo ni Kiswahili. Uchambuzi wa data ulimpeleka mtafiti kutathmini na kuhakikisha matumizi ya mbinu za uundaji wa istilahi zilizotumiwa na ambazo ni ukopaji kwa uhamishaji kamili na utohozi, uhamishaji na usawe, tafsiri sisisi, tafsiri sisisi na utohozi, tafsiri sisisi fungamanifu, tafsiri sisisi na ufupishaji, tafsiri kwa usawe amilifu na tafsiri kimaelezo.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa la kuchunguza sababu za matumizi ya mbinu za uundaji zilizotambulika na ambazo zilitumiwa kuundia istilahi za LL ya *KT*. Mbinu ya ukopaji ilitumiwa kwa sababu mbinu inasaidia katika kuziba pengo la ukosefu wa visawe vya maneno au istilahi zisizopatikana katika kamusi mbalimbali. Sababu ya tatu ni kuwa istilahi husika hazina utata wa kifonolojia na kimofolojia katika lugha ya kiswahili. Mbinu ya utohozi ilitumiwa kwa sababu tatu. Kwanza, mbinu hiyo husaidia katika kurekebisha maneno waliyokopa ili yaafikiane na muundo wa LL kifonolojia na kimofolojia. Pili, ni sifa ya lugha zote na kila lugha hukopa kwani lugha nyingi duniani zimekopa msamiati kutokana na lugha zingine. Mbinu ya Tafsiri ilitumiwa kwa sababu mbili. Kwanza KT ni kamusi ya Kiingereza Kiswahili yaani kamusi thaniya. Kwa kutumia mbinu ya tafsiri kimaelezo, watunzi wake walifanikisha kutoa uelewa zaidi wa istilahi kwa msomaji wa istilahi. Pili, ni kutokana chimbuko la misamiati mipya kila kukicha, hususan katika uga wa tiba. Tatu, ni kujiepusha istilahi ambayo ingepotosha maana ya ujumbe. Nne, Kiswahili kama lugha zingine, ina uhuru na uwezo wa kueleza dhana zilizomo katika lugha zingine. Nayo mbinu ya usawe ilitokana na sababu mbili. Kwanza, kazi muhimu ya mfasiri ni kusaka visawe katika kamusi za istilahi au kwenye wavuti mbalimbali. Pili, mbinu hiyo huwasaidia kuwasilisha kazi yao ya uundaji istilahi kulingana na muda uliokubaliwa . Wanapopata istilahi na kisawe kinacholingana kimuktadha wanazitumia mara moja. Mwishoe, lugha nyingi duniani zilitajirika kwa kuwa zilihusika na tafsiri tangu enzi za kale pakiwemo lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Kwa hiyo,

wa uundaji wa istilahi wafasiri wana uwezo wa kulinganisha istilahi kimaana na kuteua istilahi yenye maana sawa kutoka lugha ya Kiswahili au lugha nyingine za Kibantu. istilahi za LL ya *KT* zinatokana na uga wa kiufundi. Sababu hio ndiyo iliochochea matumizi ya mbinu ya tafsiri Sisisi. Pia, mbinu hio inasaidia katika kuzingatia muundo wa istilahi na dhima yake katika LL.

## 5.3. Mchango wa utafiti huu

Matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha watu wengi. Kwanza, utafiti huu uliziweka bayana istilahi zinazohusu magonjwa zipatikanazo katika *KT*. Utafiti huu tawasaidia waundaji wa istilahi na wafasiri kufahamu mbinu za uundaji istilahi zilizotumia na mabingwa wa tiba na wa uundaji istilahi na sababu zilizochochea matumizi ya mbinu hizo. Pili, utafiti huu utatoa mwanga kwa wa undaji istilahi na wafasiri ambao hawana budi ya kuudhibiti mfumko wa istilahi au msamiati unaolemea lugha ya Kiswahili. Tatu, utafiti huu utawawezesha kupata na kumudu mbinu za kuundia istilahi na kukidhi mahitaji ya kudumisha daraja la mawasiliano kati ya jamii lugha tofauti kipindi hiki cha utandawazi kilichobadili dunia katika kijiji kimoja.

Nne, utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa kwa wahudumu wa kitabibu ambao wanahitaji huduma ya tafsiri za hati za magonjwa, kuelezwa vyanzo vya magonjwa na namna ya kuyakomesha. Tano, ni mchango wa kiusomi ambao utasaidia kuchochea mjadala na mchango zaidi katika mjadala wa uundaji wa istilahi na tafsiri ya kiufundi ambao unaonekana kutoandikiwa na kutafitiwa sana. Kwa hiyo, andiko hili litakuwa ni marejereeo muhimu kwa watakaochunguza zaidi mbinu za uundaji istilahi hasa ukizingatia kwamba hili ndilo andiko la kwanza linalojadili kwa mapana mboni za uundaji istilahi za uwanja wa tiba kwa kuzingatia uwanja wa magonjwa. Aidha, ni tasnifu ya kwanza ya ngazi ya umahiri katika Chuo kikuu cha Burundi iliyojikita katika uundaji wa istilahi lililoandikwa kwa lugha ya Kiswahili nchini Burundi. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kurejelewa katika tafiti zitakazofuata. Kwa hiyo, matokeo haya ni nyongeza na yanasaidia kuziba mapengo ambayo yapo kwa ya nyaraka za

kiswahili katika maktaba ya Chuo kikuu cha Burundi. Wanaistilahi na wafasiri na watakaosoma matokeo yake watanufaika kwa kumudu mbinu za uundaji istilahi zilizotumiwa na manachuo waliotunga KT kwa kipindi cha karibu miongo miwili.

**5.4. Hitimisho.**

Matokeo ya utafiti huu yameweka bayana mbinu za uundaji wa istilahi za fani tiba kwa kizingatia uwanja wa magonjwa kupitia LL ya *KT*. Ilhali, nyanja zilizowasilishwa katika KT ni nyingi. Tafiti zingine zinahitaji kufanyika ili ziweze kudhihirisha kam ambinu zilizotumia katika mchakato wa kuunda istilahi za uwanja wa magonjwa zinafana na zile zilizotumiwa kuunda istilahi za uwanja wa madawa, operseheni, vifaa,na taaluma zihusianazo na fani ya tiba. Watungaji wa kamusi za fani zingine wanaweza kutumia mbinu za tafsiri katika mchakato wa kutunga Kamusi mbalimbali za nyuga za kiufundi kwa kuziundia istilahi za LL.

**5.5. Mapendekezo**

Katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Burundi hakuna vitabu ya isimu vilivyoandikwa katika Lugha ya Kiswahi. Kwa kuwa kulianzishwa mafunzo ya uzamili yanaohusiana na lugha ya Kiswahili, niaomba serikali ya Burundi itenge bajeti ya kununua vitabu vya Kiswahili. Watafiti wanao natija na ujuzi wa kuandika makala, vitabu nchini Burundi wanaongezeka kila kukicha, ninaomba serikali ya Burundi kuwarahisishia mazingira ya utafiti.Mazingira hayo yatawawezesha kuhudhuria vikao vya KAKAMA na MASIKIDU ili waweze kuwasilisha na kutetea matokeo ya tafiti zao.

## MAREJELEO

Adolph, E. (2014). *Utohozi wa nomino za Kiswahili na athari yake katika ngeli za Kihaya. Tasnifu ya umahiri (*Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Adolph, E. (2019). *Michakato na athari za utohozi wa istilahi za tiba na kompyuta kutoka Kiingerezawenda Kiswahili. Tasnifu ya uzamivu (Haijachapishwa).* . Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Adolph, E.& Simon, C. (2024). Mkakati wa Tafsiri Mkopo wa Istilahi za Kiingereza katika Kiswahili na Athari zake: Uchanganuzi wa Vidahizo Teule vya Kamusi ya Biolojia, Fizikia na Kemia. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 2(1), 1-9.*

Adika, S.K. (2020). Mikakati, Changamoto na Mustakabali wa Utungaji wa Kamusi za Kiistilahi za Kiswahili. *Jarida la Mnyapara*, 90-104.

Adika, S. K. (2021). Ufupishaji kama Mkakati wa Uundaji wa Istilahi za Kiswahili

Zinazotumika katika Kompyuta. Taaluma: *Jarida la CHAKITA Juzuu. 1 Namba 1*, 83-92.

Aghajani, M. and Adloo, M.( 2018). Procedures Employed in Pearsan and English Translation of the Last 16Quran onthe Basis of Vinay and Darbelnet's Model. *Journal of Applied Linguistics and Language Research, 5(5), 54-66*

Ame, P.M. (2017). *Athari za Kiisimu za Lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili SanifuKinachotumika katika Shule za Tumbatu Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Armstrong, N. (2005). *Translation, Linguistic and Culture: A French - English Handbook*.Clevedon: Multilingual Matters.

Baker, M. (1992). *In Other Words: A Coursebook on Translation*.London: Routledge. Bassnett, S. (1980). *Translation Studies*. London: Routledge.

BAKITA (1974). *Tafsiri Sanifu .Tol. la* 1, Dar es Salaam

BAKITA, (2005). *Istilahi za Kiswahili*: Dar es Salaam.

BAKIZA, (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Oxford, Kenya.

Barikore, B.( 1989). *Le journalisme burundais face aux problèes de traduction du kirundi au français*, mémoire, Bujumbura, Ecole de journalisme.

Benjoint, H. (1996). *Les dictionnaires bilingues.* Louvain- la- Neuve: Duculot,s.a.

Buliba, A., & al. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti, Mwanza*: Serengeti Educational Publishers.

Butoyi, D. (2022). *Tathmini ya Makosa ya Kisarufi ya Wanafunzi wa Kingwana Wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Uchunguzi Kifani wa Vyuo Vikuu Burundi*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Bwenge, C.M. (1996). Utafutaji, Uundaji na Utumiaji wa Istilahi katika Tafsiri.” *Mulika Juzuu* Namba 23. Kur. 56-72.

Catford, J. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. Oxford: Oxford University Press.

Chesterman,A. (1997). *Memes of Translation: The Spread of Ideas in Translation Theory*. Amsterdam: John Benjamin

Cohen, L., Manion, L. na Morrison, K. (2007). *Research Methods in Education* (Toleo la 6). New York: Routledge.

Chomsky, N. (1968). *The sound pattern of English*. [SPE] New York: Harper and Row

Chuwa, A. R. (1988) “Foreign Loan Words in Kiswahili”. Kiswahili. Juz. Na. 55(1) na 55(2): 163-172.

Dawson, C. (2007). *A Practical Guide to Research Methods* (Toleo la 3). Oxford: How to Books Ltd.

Denscombe, M. (2002). *The Good Research Guide: For Small-scale social Research Project* (Toleo la 2). Philadelphia: Open University Press.

Durrel, G. (1982). *Science Explorer: Investigations in life, Earth and Physical Science*. United States of America: Afred A Knopf Publisher.

Felber, H. (1984). *Terminology of manual*. UNESCO and Infoterm .Paris; INFOREM Series 21/Umsist.

Gambier, Y. (2011). La retraduction: ambiguïtés et défis. *Autour de la retraduction. Perspectives littéraires européennes, pp. 49-66*, sous la direction de E. Monti & P. Schnyder, 2011. Paris: Ed. Orizons

GAO-PEMD. (1996). *Content Analysis: A Methodology for Structuring and Analyzing Written Materials*. Illinois: PEMD.

Harvey, M. (2012). “A beginner’s course in Legal Translation: The case of Culture boundTerms”. Katika A.F. Guerra (2012). “Translating Culture Problems, Strategies and Practical realities”. *Juzuu la Literature, Culture and Literary*.

Hatch, J.A. (2002). *Doing Qualitative Research in Education Settings*. New York: State University of New York Press.

Havyarimana, E. (2024). L’Organisation du Marché de la Traduction au Burundi. *International Journal of Academic Multidisciplinary Reseach (IJAMR), Vol .8. 50- 63.*

Hervey, S. and Higgins, I. (1992). Thinking Translation. London: Routledge.

Holloway, I. (1997). *Basic Concepts for Qualitative Research*. Oxford: Blackwell Publishers.

Hoffer, B.L. (2005). Language Borrowing and the Indices of Adaptability and Receptivity, katika *Intercultural Communication Studies, Juzuu XIV/2: 53-72*.

Irira, S. D. (1990). *Mwongozo wa Usanifishaji Istilahi (Mimeo).* Dar-es Salaam: BAKITA

Jammal, A. (1999). Une méthodologie de la traduction médicale. *Meta Journal des traducteur,* 217–237.

Jilala, H. (2014). *Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu (Ph.D Kiswahili) (haijachapishwa).* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

*Other African Languages Vol. 2 No. 1(2)*, 31-40.

Jilala,H. (2021). Mbinu na Nafasi ya Tafsiri Katika Uundaji wa Istilahi Za Sayansi na Teknolojia:Mifano Kutoka Progaram za Klinux na . *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, 43 – 52.

Jilala,H. (2022). Tathmini ya Programu ya Tafsiri ya Google kama Zana ya Mfasiri: Changamoto na Mapendekezo. *Mwanga wa Lugha*, 131- 152.

Jilala,H. ( 2023). Mchango wa Tafsiri za J.K. Nyerere katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili . *Mwanga wa Lugha* , 75- 87.

Jilala,H. (2024). Mtazamo wa Ki-Afrika katika Nadharia za Tafsiri . *Journal of Kiswahili and*

Johnson, F. (1935). *Kamusi ya Kiswahili. Nairobi.* Oxford : Oxford University Press .

Jones, B. R. (2000). *The World Turned Upside Down?: Globalization and the Future of the State.* New York: St. Martins.Press.

Kamusi ta Tiba, (2003), TUKI

TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: TUKI

Kapinga, A. (1966). Maneno yanayofanya msamiati wa Kiswahili. Katika Z.N.Z Tumbo Massobo na J. G. Kiango (wah). *Mulika Na. 23.* Dar- es Salaam: TUKI.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Kevogo, S .A . (2000). Mikakati, Changamoto na Mustakabali wa Utungaji wa Kamusi za Kiistilahi za Kiswahili, *Jarida la Mnyampala –Juz. Na.1*

Kevogo, S .A . (2021). ‘‘Ukopaji kama Mkakati wa Kuendeleza Istilahi za TEHAMA katika Kiswahili: Uchunguzi wa Vidahizo Teule vya Kamusi Sanifu ya Kompyuta, Kiputiputi (2011)’’

Kiango, J. G. (1999) “Matatizo ya Utohozi wa Maneno kama Mbinu ya Kukopa Istilahi katika Lugha”. *Mulika, Juz. 25: 1-8.*

Kiingi, K. (1998). *A Theory of Scientific Terminology: A Thesissubmitted in fulfilment for the Degree of Doctor of Letters in Kenyatta University* (Mswada Usiochapishwa).

Kiparsky, P. (1982) "Lexical Morphology and Phonology." In *I.-S. Yang {ed.) Linguistics in the Morning Calm*. Seoul, Hanshin.

Kiparsky,P. (1982). From cyclic phonology to lexical phonology. In The structure of phonological representations (part I), *ed. Harry van der Hulst and Norval Smith, 131-175. Dordrecht: Foris*

Kiputiputi, O.M. (2011). *Kamusi Sanifu ya Kompyuta*. Dar es Salaam: TUKI.

Kothari, C.R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd

Kothari, C.R. (1990). *Research Methods: Techniques and Procedures*. Longman: University Press.

Kothari, C.R. (2013). *Research Methodology.Methods and Techniques, 2 nd Ed* . New Delhi:

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology: Methods Techniques*. Delhi: New Age International (p)

Krippendorff, K. (2004). *Content Analysis: An Introduction to its Methodology*. Califonia: Sage Publications.

Larson, M.L (1984). *Meaning Based Traslation:* A guide to cross-Language Equivalence, University Press of America Inc.

Likhako, P.I. (1991) .*Ufaaji wa Kiswahili kama lugha ya kisomo* .Tasnifu ya M.A. University of Nairobi. Haijachapishwa.

Lörschester, W.(1991).*Translation Performance, Translation Process and Translation Strategies. A Pyscholinguistics Investigation*.Tübingen. Gunter Narr.

Mabasa, T. A. (2005). *Translation Equivalents for Health/ Medical Terminology in* Xitsonga. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha of Pretoria.

Malangwa, P.S. (2010). *Handling Technical Translations: The Case of Translations of Computer Programs from English into Kiswahili*. Unpublished Ph.D Thesis, University of Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. na Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Matinde; S.R. (2012). Dafina la Lugha Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu.Tanzania: Serengeti Educational Publisher TLTD

Mdee, J.S. (Mh.). (1977). *Nadharia na Historia ya Leksikografia.* Dar es Salaam: TUKI.

Mdee, J.S. (Mh.). (1995). *Misingi ya Utungaji Kamusi.* Dar es Salaam: TUKI

Mdee, J.S. (Mh.). (1996).Dhima ya Tungo za Mifano ya Matumizi katika Kamusi.*Mulika Juzuu* Na. 23. Kur.1-11

Mlacha, S.A. (1999). *Kamusi ya Sheria*. Dar es Salaam: TUKI.

Moraa, A. (2013). *Matatizo Yanayodhihirika Katika Matini Tafsiri za Kimatibabu: Utafiti Kielelezo Katika Hospitali ya Kisii Level 5. Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Mosota, E, K. (2016). *Utohozi wa Msamiati kutoka Kiswahili hadi Ekegusii*, Nairobi, Chuo Kikuu cha Nairobi, Tasnifu ya Uzamili

Mugenda O.M. (1999). *Research Methods, Quantitative and Qualitative Approaches*, Nairobi: Acts Press

Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (2003*). Research methods: qualitative and quantitative approaches.* Acts Press Kenya.

Mukuthuria, M. (2010). Maadili ya Utafiti. African Journals online. 73(1), 61-82.

Munday, J. (2001). Introducing Translation Studies. Theories and Applications. *Southern African Linguistics and Applied Language Studies,Volume 21, Issue1-2*, 83- 85.

Munday, J. (2012). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications, Tol. 3.* . Routledge-Taylor & Francis Group. : Routledge-Taylor & Francis Group.

Mushumbwa, A. R. «Utata wa Maudhui ya Kisarufi katika Vitabu vya Kiada vya Kiswahili Kidato cha Kwanza na cha Tatu Nchini Tanzania » *Kioo cha Lugha*, Juz. 21(1) 55-74 *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili* .Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mutiso, M. (2012). *Kamusi ya Diplomasia: Kiingereza-Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI

Mwajuma, A. (2018). *Changamoto za Kutafsiri Tungo zenye Utata Kutoka Kiswahili kwende Kiingereza.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mwangi,I. (1996). *Matatizo ya Leksikografia tafsiri: Tathmini ya Kamusi ya F. Johnson (1939).* Nairobi: University of Nairobi.

Mwangomango, J. S. (1972), Kiswahili karne ya 20. Kiswahili Juzuu 51/1 na 52/2, Dar es Salaam; TUKI.

Mwansoko, H .J. M. (1990). Modernization of Swahili Technical Termilogies: An Investigation of the Linguistics and Literature Terminologies. Tasnifu ya PhD (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha York.

Mwansoko, H. J.M .(2006). *Kitangulizi cha Tafsiri:nadharia na mbinu.* Dar es Salaam: TUKI.

Mwansoko, H. J.M. (2013). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu (3rd ed.).* Dar es Salaam: TUKI.

Mwansoko, H.J. M. (2015). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu, Toleo la Nne.* Dar es Salaam: TATAKI.

Mwansoko, H.J.M. (1990). *The Modernization of Swahili Technical Terminologies: An Investigation of the Linguistics and Literature Terminologies. Tasnifu ya Uzamifu* (Ph.D) Isiyochapishwa, Chuo Kikuu cha York.

Mwansoko. (1996). *Kitangulizi cha tafsiri: nadharia na mbinu,.* Dar es Salaam: TUKI.

Mwaro-Were, A. G. (2000). *Usayansi wa istilahi za isimu ya Kiswahili. Tasnifu ya uzamivu .* Nairobi: Chuo Kikuu cha Egerton.

Mwaro-Were, A. G. (2001). Istilahi za isimu ya Kiswahili zilizobuniwa na TUKI (1990): Tathmini ya kufaa kwake. *Kiswahil*i, 64. 31-51.

Mwita ,M .A na Mwansoko, H.J.M. (2003). Kamusi ya Tiba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TUKI.

Nabhany, A. S. (1982). Barua, Maoni, Mapitio, Mashairi. Kiswahili, Juzuu 49/2. Dar-es-Salam: TUKI.

New Age International (P) Ltd.

Newman. (2006). *Social Reserch. Sixth Edition* . Boston: Pearson.

Newmark, P. (1981). *Approaches To Translation (Language Teaching Methodology Senes).* Oxford: Pergamon Press.

Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation.* Newyork: Prentice Hall.

Newmark,P. (2003). *A Texbook of Tanslation.* London: Pearson Education Limited.

Nimessi (2020). La Terminologie. Advanced School of Translators and Interpreters, University of Buea, Cameroon.

Nina, R. (2008). *"Analysis of a Medical Translation Terminology and Cultural Aspects*" Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Pretoria, ambayo haijachapishwa.

Nkurunziza, F. (2021). *The Status of the Translation Profession in Burundi*. Mémoire de master inédit. ASTI, PAUTRAIN, Université de Buea.

Nord,C .(1977). *A Fonctional Typology of Translation.* Amsterdam: John Benjamins.

Odlin, T. (1989). *Language transfer: Cross-linguistic influence in language learning*. Cambridge, UK: Cambridge University Press.

Ohiy, R. (1981). *A short Mannual of Coinage in Swahili*. Unpublished manuscript, Institute of swahili research, University of Dar es Salaam.

Okal, O. B. (2018) "Uhakiki Linganishi wa Taarifa Muhimu kuhusu Vidahizo katika *Kamusi ya Karne ya 21* na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*." *Mulika, Juz*. Na. 36: 87-100.

Omondi, A.O. (2008). *Utohozi wa Fonolojia wa Manenomkopo ya Kijaluo kutoka Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa).* Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Panou, D. (2013). Theory and Practice in Language Study. *Theory and Practice in Language Studies, 3(1), 1- 6.*

Pearson, P. (1987). *An Introduction to Acupuncture. A Practical Guide for GPs and OtherMedical personnel*. Norwell: M A MTP Press.

Pjuastuti, S. (2014). *A survery on Translation Strategies by Accounting Study Program Students in Translation Undergraduate Thesis Abstracts*. Tafsnifu ya Stashahada, Chuo Kikuu cha Bengkula.

Ponera, A.S. (2016). 'Suala la Matumizi ya Nadharia kama Kiunzi cha Tatifi za Kitaamuli: Mfano wa Matumizi ya Nadharia ya Ukanivali' katika *Journal of humanities (JH*), Chuo Kikuu cha Dodoma, Volume 3(1), kur. 128-143

Ponera, N. (2016). *The use of information and communication technologies (ICTs) in teaching and learning advanced mathematics in southern Tanzanian secondary schools: a case of one secondary school (Unpublished Master's Thesis).* Dar es Salaam: Aga Khan University

Ponera, N. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: CTP

Ramadani, A .A. (2018*). Matumizi Ya Lugha Ya Ishara Katika Nyimbo Za Taarabu: Uchunguzi Wa Nyimbo Za Mohamed Ahmed Moh'd, Tasnifu ya Uzamili*, ChuoKikuu Huria Tanzania.

Reiss, K. (1971/2000), *Moglichketeiten und Grenzen der Ubersetzungskrititik*, Munich: M. Hubeber, imetafsiriwa na E. F. Rhodes (2000), kama *Translation Criticism: Potential and Limitations*. Manchester: St. Jerome and American Bible Society.

Ruane, J.M. (2005). *Essentials of Research Methods: A Guide to Social Science Research*. Oxford: Blackwell Publishers.

Rubanza, Y.I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria

Sigh, K. (2007). *Quantative Social Methods*, New Delhi, SAGE Publication. SouthernCalifornia: Pergamon Press Inc.

Singoei, J.J., Kandagor, M., & Mohamed, M. (2020) . Namna Matumizi ya Mikakati ya Kutafsiri, Kama Uteuzi Na Mpangilio WA Maneno, Ilivyochangia katika Uandishi Upya WA Bukuit Ne Tilil. Editon Cons. J. *Kiswahili, 2(1), 136-149*

Stephano, R. (2020) "Utoshelevu wa Mawasiliano kwa Kiswahili katika Teknolojia ya SIKANU: Uchunguzi Kifani wa Whatsapp*."* *JULACE* 5(1) , 1- 14.

Stobersk , Z.(1981). IXe Congrès Mondial de la Fédération Internationale des Traducteurs et ses buts Babel, *Volume 26, Issue 4, Jan 1980, p. 194 – 196*

Taber, E. A. (1969). *The Theory and Practice of Translation (Helps for Translators Prepared Under the Auspices of the United Bible Societies, VIII).* Leiden: Brill.

TATAKI. (2010). Programu ya Digrii ya M.A (Kiswahili). Dar es Salaam: TATAKI.

Tavallaei, M. na Abu-Talib, M. (2010), "A General Perspective on Role of Theory in Qualitative Research", *The Journal of International Social Research*, Vol. 3, No. 11, 570-577

Temu, C. (1981). Uundaji wa maneno mapya ya Kiswahili – Kichocheo cha Mjadala. Makala

yaliyosomwa katika kongamano la kimataifa la Kiswahili K. K. A, Nairobi, September 1981.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 3).* Nairobi: Oxford University Press.

TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tumbo-Masabo, Z. N. Z, na Herlman,J. M. M (2008), Kiongozi: Uundaji wa Istilahi za Kiswahili. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Tumbo-Masobo, Z. na Mwansoko, H. J. (1992). Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili.

Dar-es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

UNESCO. (2024, October 3). *World-atlas-languages*. Récupéré sur The World Atlas of Languages (WAL) : **https://en.wal.unesco.org/**

Venuti, L. (2012). *The translation studies Reader* (3rd Edition). London : Routledge

Vinay J.-P. et J. Darbelnet (1958) [2004*], Stylistique comparée du français et de l'anglais: méthode de traduction*, Paris, Didier [Nouvelle édition revue et corrigée].

Wadensjo, C. (1998). *Interpreting as Interaction.* London. : Longman .

White, M.D. na Marsh, E.E. (2006). Content Analysis: A Flexible Methodology. *Library Trends* 55 (1), 22– 45

Whiteley, W. H. and M. G. Muli (1963). Loanwords in Kamba: A Preliminary Survey African Language Studies, IV.

Whiteley, W. H. and M. G. Muli, (1962). Practical Introduction to Kamba, London: Oxford University Press.

Williman, N. (2011). *Research Methods: The Basics*. New York: Routledge.